   Kitano ni senti 5, na kikumi ni senti 10.

6. Sarafu hii ndogo ya fedha ni nusu shilingi?

   Ndio, pengine watu husema ni thumuni.

7. Je, na pesa nane ni senti 25 kweli?

   Ndivyo, angalia wasikudanganye sokoni wasikuambie ni zaidi.

8. Naona kwamba sarafu za masenti zina matundu, kwa nini?

   Ili wasizipoteze, wanawake walizifunga pamoja kwa uzi.

LESSON 64


1
SOKO
BENKI
2
BARCLAYS
3
4
2
5/-
10/-
5
Kitano
=5¢ &
Kikumi
=10¢
6
Sh 0/50
"Thumuni"
7
"pesa nane" = 25 senti
SOKO
8

1. What shall I do, so I won't go to market without small change?

   Nevermind, my friend, there's a bank nearby.

2. Well, if it isn't Barclays Bank, this is very well known.

   True; say, would you like this teller to help you?

3. Yes, would he please change these notes?

   For how many pounds would you like change?

4. I have only two pounds and 5 shillings.

   O.K., here are Sh. 10/-notes and the rest in silver.

5. What value do the copper coins have?

   A "kitano" is 5 cents, and a "kikumi" 10 cents.

6. Is this small silver coin a half shilling piece?

   Yes, on the other hand people call it a "thumuni.

7. Say, and is "pesa nane" truly 25 cents?

   Yes, be careful they don't cheat you at the market and tell you it's worth more.

8. I see that the cent pieces have holes in them, why?

   So they don't lose them, women tie them together with a piece of string.

Step 1. Drills on the negative form of the Subjunctive.

1. Repetition Drill

a. Usininunulie motokaa ya thamani kubwa.

mkeka, baisikeli, shamba

b. Msiwapatie sarafu nyingine.

letea, pelekea, kupa

c. Ametuambia tusipate chenji zaidi.

toa, tuma, weka

d. Tafadhali usibadilishe pesa katika benki.

weka, toa, peleka

e. Usimpatie kitano kingine.

kikumi, noti, thumuni

f. Nimewaambia wasitumie pesa za karatasi.

pokea, ficha, toa

g. Usitupe pesa zako bure.

haribu, toa, poteza

h. Mpe sarafu zenye matundu.

tolea, tumia, lipa

i. Nipatie chenji ya pauni moja.

kupa, onyesha

2. Substitution Drill

a. msiwabadilishie: ---------- watoto noti zao.

rudishia, nyang'anya, kupa

b. usiwape: ------- wafanyi kazi mshahara leo.

nyima, lipa, patia

c. nisiweke: Wameniamrisha ------- sarafu za shaba.

tumia, chukua, toa

d. msiwalipe: ------- zaidi ya pesa nane kila mmoja.

kupa, onyesha, letea

e. awasaidie: Nitamwomba --------.

ongoza, lipa, pokea

f. wasikudanganye: Angalia sana ----------.

kupiga, ua, poteza

g. unibadilishie: Nataka ----------noti hizi.

lipa, kupa, tumia

h. asiondoke: Mwambie karani -------- sasa.

pumzika, lala, fanya kazi

i. msikaribie: Tafadhali --------- hapo.

kwenda, simama, kaa

Step 2. Language clab session (if applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the clab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue and pattern drill practice.

b. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 64

Step 1. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 2. Patterned response drill.

a. Atafanyaje ili apate pesa za kutosha?
Ni lazima afanye bidii ili apate pesa.

weka, lipa, chuma

b. Ulimwambia akubadilishie pauni ngapi?
Nilimwambia anibadilishie pauni tatu.

patia, lipia, letea

c. Wanakuomba uwape pesa ngapi?
Wananiomba niwape senti kumi kila mmoja.

lipa, pelekea, patia

d. Mtafanyaje ili wasiwadanganye?
Tutajihadhari sana ili wasitudanganye.

kamata, ona, gundua

e. Alikuambia ulipe thumuni?
La, hakuniambia nilipe thumuni.

toa, weka, tumia

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 64

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. M1ipoendelea kaskazini mliona nini?
Tulipoendelea kaskazini tuliona ziwa Victoria.

enda, elekea, safiri

b. Wanajitayarisha ili wasafiri wapi?
Wanajitayarisha ili wasafiri Kenya.

shambulia, ingia, ende

c. Walikuamrisha uongee lugha gani?
Waliniamrisha niongee Kiswahili.

soma, jifunza, andika

d. Unataka nimpe mtumishi bakshishi?
Ndio, mpe bakshishi kidogo.

patia, pelekea

e. Usipowaelezea vizuri watafanyaje?
Nisipowaelezea vizuri watanifukuza.

fundisha, ongoza, karibisha

f. Gavana atakaa hapa kwa muda gani?
Atakaa hapa kwa miaka minne.

sisi, wageni, ninyi

g. Umepata kuuona mlima Kilimanjaro?
La, sijapata kuuona mlima huo.

watu wa Unguja, vitabu vyangu, mikeka yao.

h. Unajuaje kwamba <u>wamefika</u> mjini?
Ninajua wamefika kwa sababu niliwaona.

rudi, jificha

i. <u>Jengo</u> gani lilibomolewa jana?
Jengo la Juma lilibomolewa jana.

nyumba, majengo

j. <u>Meli</u> imeingia bandarini?
La, haijaingia bandarini.

mtumbwi, mitumbwi, wanamaji

k. <u>Tutawavizia</u> adui usiku wa manane.

shambulia, teka, fukuza

l. Asipolala kifudifudi <u>ataonekana</u>.

anguka, kufa, 'mia

m. <u>Wanahewa</u> hawakushambulia kwanza.

sisi, wewe, ninyi

n. Ndege za adui <u>hazikuonekana</u>.

patikana, haribiwa, shambuliwa

o. <u>Alikana</u> mashtaka yote manne.

kubali, jibu

p. <u>Hakimu</u> alikata neno mara moja.

sisi, wageni, ninyi

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Nilipomtembelea mwenzangu kule Nairobi siku moja, nilimkuta akijitayarisha kwenda sokoni. Alinikaribisha niende pamoja naye. Nilikubali, lakini nilipoangalia mfukoni niliona ya kwamba sina pesa ndogo ndogo. Hivyo ilinibidi kufika benki kwanza kubadilisha pesa za karatasi.

Kwa sababu sijafika Nairobi, wala Afrika ya Mashariki siku nyingine bado, sikujua matumizi za pesa za huko. Hivyo tulipofika Barclays Bank, benki inayojulikana sana kule, nilionyeshwa aina za sarafu za kule. Kwanza nilitambua kwamba kuna senti mia moja katika shilingi moja. Sarafu za senti moja ni za shaba nyekundu. Ni ndogo sana na zina tundu katikati. Hata sarafu nyingine za shaba, yaani vitano na vikumi zina tundu vilevile. Wanawake wakipenda kufunga sarafu hizo salama wapitisha uzi au kamba nyembamba katika tundu na hivyo wanazifungia pamoja ili zisipotee.

Pesa nyeupe, yaani sarafu za fedha, ni zile za

shilingi moja na nusu shilingi. Nusu shilingi ni senti hamsini, na kwa watu wengi ni thumuni. Pesa za karatasi ni noti za Sh. 5/-, Sh. 10/-, Sh. 20/-, Sh. 100/-, na Sh. 1,000/-. Maandiko juu ya noti hizo ni katika lugha tatu, yaani: Kiingereza, Kiswahili (kwa mwandiko wa Kiarabu), na Kihindi.

Karani wa benki alinipa chenji ya shilingi ishirini na tano, na hapo nilikuwa tayari kufuatana na mwenzangu kule sokoni.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nilimkuta mwenzangu akifanyaje?
Nilikubali kwenda wapi?
Nilihitaji nini kwanza?
Benki ingalinisaidia kwa njia gani?
Je, nilikuwa mgeni kule Nairobi?

Nilijua matumizi ya pesa za kule?
Benki gani inajulikana sana Afrika ya Mashariki?
Sarafu za shaba ni za aina gani?
Za fedha ni za aina gani?
Noti ziko za aina na thamani gani?

Wanawake walizoea kufanya nini na sarafu za senti?
Walifanya hivyo kwa sababu gani?
Maana yake pesa nyeupe ni nini?
Maandiko juu ya noti ni kwa lugha gani?
'Pesa nane' ni nini?

18

Note: When answering these questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

I. Language Structure

The Negative Subjunctive

The negative subjunctive is formed by simply inserting the negative particle 'si' after the subject prefix. It follows also the same pattern as the negative direct command which was studied in Lesson 39.

Examples: Alisema nisiende.
(He said that I shouldn't go.)

Angalia usipotee.
(Watch out you don't get lost.)

Mwambie asivute sigara hapa.
(Tell him not to smoke here.)

Angalia kikombe kisivunjike.
(Be careful so the cup doesn't break)

The short one-syllable verbs drop the 'ku' particle in the negative subjunctive just as they did in the affirmative.

Examples: ku-la, ku-ja, ku-fa.

Mwambie asile nyama hii.
(Tell him not to eat this meat.)

Waambie wasije kesho tena.
(Tell them not to come tomorrow again)

Mtunze vizuri ili asife.
(Take good care of him so he doesn't die.)

II. Cultural Note

The money system used in East Africa is partially based on the British system in that the Pound Sterling and the shilling is basic in the system.

The Pound is equal to 20 shillings, and each shilling in turn has 100 cents. The higher currency is in the form of paper notes and these are:-

5 shillings	(5/-)
10 shillings	(10/-)
20 shillings	(20/-)
100 shillings	(100/-)
1000 shillings	(1000)

It is interesting that the inscriptions on this paper money are in three languages: English, Swahili (with Arabic script), and Hindustani (with Hindi script).

The coins are as follows:-

a. 1 shilling silver coin.
50 cent piece silver coin.

b. 10 cent piece copper coin.
5 cent piece copper coin.
1 cent piece copper coin.

The copper coins have an interesting feature in that all these coins have a hole through the center. This has practical value, especially in rural areas, or for sparsely clad individuals in that these coins can be gathered and tied together on a piece of string.

The Swahili nomenclature for various money values and coins is often based on the English.

Pound	=	pauni
Shilling	=	shilingi
Cent	=	senti
Note	=	noti
Coin	=	sarafu
50 cent piece	=	thumuni, thumni, sumni,
10 cent piece	=	kikumi
5 cent piece	=	kitano

Often heard also is 'pesa nane' which is equivalent to 25 cents.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 65

GREJI

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. Morphology: The Habitual Tense. Tense sign 'HU'.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Picture: Car brought to a garage for repairs and servicing.

b. Cultural Note: Note on garage and service stations in East Africa.

c. Lexical items:

gereji	garage
mekanika	mechanic
aminika	trustworthy, reliable
gari	vehicle, car, cart
kabureta	carburetor
beteri	battery
piga stati	start an engine
hakikisha	make sure
waya	wire
plagi	plug, spark plug
badilisha	change
mafuta	oil
injini	engine
tairi	tire
gia	gear
girisi	grease
redieta	radiator
tangi	tank
petroli	gas, petrol

1st PERIOD PERCEPTION DRILL LESSON 65

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on the 'HU' tense.

a. Motokaa huharibika.
Motokaa huwaka upesi.
Motokaa hupendeza.

b. Mekanika huaminika.
Mekanika hutengeneza.
Mekanika hufanya kazi.

c. Ndege huruka.
Ndege hula chakula.
Ndege hukaa pale.

d. Watoto hucheza.
Wanafunzi hujifunza.
Walimu hufundisha.

e. Dereva huendesha motokaa.
Mwanahewa huendesha eropleni.
Wao huendesha mtumbwi.

f. Askari hodari hupigana.
Wanyama hula majani hapa.
Simba huua swala.

2. Semantic drill on borrowed words.

a. Anasafisha karbureta.
Anasafisha plagi.
Anasafisha injini.

b. Anajaza redieta.
Anajaza beteri.
Anajaza tangi.

c. Badilisha mafuta ya injini.
Badilisha mafuta ya gia.
Badilisha mafuta ya taa.

d. Hupiga ripoti.
Hupiga stati.
Hupiga pasi.

e. Tumehakikisha.
Tumebadilisha.
Tumepima tairi.

f. Anatia girisi.
Anatia petroli.
Anatia mafuta.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Wapi gereji? Motokaa huharibika kutwa.
   Gereji ni pale, na mekanika huaminika.

2. Hamjambo? Ninyi ni mekanika hapa?
   Ndio, twafanya kazi hapa siku zote.

3. Gari langu haliendi! Tafadhali safisha kabureta.
   Vizuri, tutaangalia beteri pia.

4. Motokaa huwaka upesi ninapopiga stati.
   Lakini sasa inakataa?

5. Ndio, hakikisha kama waya na plagi ni nzuri.
   Plagi huharibika upesi siku hizi.

6. Halafu badilisha mafuta katika injini.
   Vema na tutapima tairi vilevile.

7. Badilisha mafuta ya gia na tia girisi popote.
   Vema, nitahakikisha redieta imejaa vilevile.

8. Utakapomaliza kazi, jaza tangi petroli.
   Tutatengeneza kila kitu sawasawa.

LESSON 65



1. Where's the garage? The car is continually out of order.

   The garage is over there, and the mechanic is reliable.

2. Howdy! Are you the mechanic here?

   Yes, we work here all the time.

3. My car won't run! Please clean the carburetor!

   O.K., and we'll check the battery as well.

4. The car usually starts up quickly when I start it.

   And now it won't run?

5. That's right, make sure wiring and plugs are O.K.

   The plugs get out of order quickly these days.

6. Then change the oil in the engine.

   O.K. and we'll check the tires as well.

7. Change the gear oil and grease it everywhere.

   O.K. and I'll make also sure the radiator is full.

8. When you finish the job, fill up the tank with gas.

   We'll fix everything properly.

3rd PERIOD PATTERN DRILL I LESSON 65

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Motokaa huharibika kutwa.
Motokaa huharibika kutwa.

enda, simama, tengenezwa, saidia.

b. Gari langu haliendi.
Gari langu haliendi.

simama, haribika, faa.

c. Plagi huharibika upesi.
Plagi huharibika upesi.

pasuka, vunjika, toboka.

d. Mtoto huyu huaminika sana.
Mtoto huyu huaminika sana.

fanya kazi, pumzika, lala, jifunza.

e. Mekanika hubadilisha mafuta siku zote.
Mekanika hubadilisha mafuta siku zote.

ongeza, tia, tumia, pata.

2. Substitution Drill

a. huharibika
Mashine ---------- mara nyingi.
Mashine huharibika mara nyingi.

vunjika, simama.

b. hutengeneza
Mekanika ---------- plagi siku zote.
Mekanika hutengeneza plagi siku zote.

nunua, haribu, uza, rudisha.

c. huaminika
Mtu huyu --------- kila mara.
Mtu huyu huaminika kila mara.

jifunza, fundisha, lala, pumzika.

d. huendesha
Dereva --------- motokaa kila siku.
Dereva huendesha motokaa kila siku.

nunua, leta, tumai, uza.

e. hupasuka
Plagi -------- kila mara.
Plagi hupasuka kila mara.

haribika, vunjika, chafuka.

Step 2. Language clab session (if applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the clab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue and pattern drill practice.

b. Written work based on lesson 45.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 65

Step 1. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 2. Patterned response drill.

a. 1st: Motokaa huharibika kila mara?
2nd: Ndio, huharibika kila mara.

anguka, gongana, vunjika, kutana.

b. 1st: Mashine hii huharibika saa zote?
2nd: La, huharibika mara chache tu.

simama, zunguka, pinduka, waka.

c. 1st: Mekanika huyu hufanya bidii sana?
2nd: Ndio, hufanya bidii sana.

kazana, chelewa, aminika, pumzika.

d. 1st: Redieta yako hupasuka mara nyingi?
2nd: La haipasuki mara nyingi.

vunjika, toboka, haribika.

e. 1st: Dereva hubadilisha mafuta kila siku?
2nd: Ndio, hubadilisha mafuta kila siku.

nunua, uza, pata, tafuta.

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Waislamu huabudu Jumapili?
La, huabudu Ijumaa.

kutanika, burudika, pumzika

b. Wavuvi hupenda kuvua samaki?
Ndio, hii ni kazi yao.

furahi, enda, ondoka, tamani

c. Daktari huyu hupumzika Jumapili?
Ndio, hupumzika kila Jumapili.

fanya kazi, burudika, ogelea, tembea

d. Wagonjwa hulalamika siku zote?
Wengine hawalalamiki.

umia, pata dawa, pumzika, lala

e. Adui hushambulia kila jioni?
La, hawashambulii kila siku.

ingia, tawanyika, kutamika, hama

f. Hakimu hutoa hukumu siku zote?
Siku zingine hatoi hukumu.

chelewa, rudi, jifunza, amua kesi

g. Wakulima huvuna kila mwezi?
La, hawavuni kila mwezi.

panda, lima, kata miti, fyeka.

h. Wakristo huabudu siku gani?
Wakristo huabudu Jumapili.

pumzika, omba

i. Wageni hukaa wapi?
Wageni hukaa hapa kila mara.

pumzika, jiburudisha, kula

j. Motoka huhitaji maji kiasi gani?
Huhitaji maji kidogo tu.

tumia, pata, chukua

k. Nani husafisha karbureta yako?
Mekanika husafisha karbureta yangu.

tunza, tengeneza

l. Nani huendesha motokaa kila siku.
Dereva huendesha motokaa kila siku.

tengeneza, safisha, tunza

m. Mekanika hubadilisha mafuta ya injini pia?
Ndio, hubadilisha mafuta ya injini pia.

tumia, uza, nunua

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Juzi nilisafiri kwa motokaa kuonana na daktari. Motokaa yangu ni mzee kidogo na siku hizi ilianza kufanya matata. Hivyo nilipopita mjini nilitafuta gereji. Mtu mmoja aliniambia niende kwa gereji moja hapo karibu. Alisema mekanika ni hodari na anaaminika.

Mekanika aliyekuwa hapo aliniamkia na aliuliza habari ya motokaa. Nilimwambia asafishe kabureta na ahakikishe kama waya na plagi zote ni sawasawa. Atakapomaliza kazi hiyo nilitaka abadilishe mafuta katika injini na atie girisi, vilevile aangalie redieta, beteri na tairi zote.

Mekanika alitengeneza kila kitu vizuri. Nilipopiga stati injini iliwaka maramoja. Nilifurahi, nilimpa pesa zake, na niliendelea safari kuonana na daktari kwa sababu ya ugonjwa.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nilikwenda wapi juzi?
Motokaa yangu ni mpya?
Ilianza kufanya matata?
Nilitafuta nini mjini?
Mekanika katika gereji alikuwa mtu mwema?

Nani aliniamkia?
Nilitaka mekanika asafishe nini?
Atafanya nini na plagi?
Nilitaka abadilishe mafuta?
Vilevile nilitaka aangalie nini?

Mekanika alitengeneza motokaa sawasawa?
Injini iliwaka upesi?
Nani alifurahi?
Niliendelea kuonana na nani?
Nilitaka kuonana na daktari sababu gani?

Note: When answering the above questions, students should do so by us ng complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

I. Language Structure

In this lesson we learn to use a tense and form of a verb which, in a way, is timeless. It has no past, present, or future. This is the habitual tense which is used to denote an action as being done all the time as a matter of custom, habit or inherent nature.

For example:-

Ndege huruka.
(Birds fly.)

Watoto hucheza hapa.
(The children customarily play here.)

Simba huwinda wanyama kwa chakula.
(The lion hunts animals for food.)

Wanawake huchota maji hapa.
(Women habitually draw water here.)

Note that a verb in this form has no subject prefix, and so the noun as subject has to be indicated or clearly understood.

II. Cultural Note

More modern service stations are being built everywhere in cities and smaller towns. The large oil companies such as: Shell, Standard, Texaco, BP, and others not so well known in the States operate throughout East Africa. The gallon in use there is the Imperial gallon, and not the smaller U. S. gallon. There are five U. S. gallons to 4 Imperial gallons.

When one drives up to the pump, it is a petrol pump, not a gas pump, and so one asks to have the tank filled with petrol.

In smaller villages or rural shops or trading posts, there may not be a pump, but one may be able to buy petrol in 4-gallon tins. These tins when empty are in demand in many places and are used as handy containers to carry water in, or some people buy them in greater numbers, cut them open so they can be flattened, and then they are used as a form of cheaper roofing material.

Good garages and reliable mechanics will be found only in larger towns and cities. A driver who ventures out on poorer roads, over long stretches, has to be prepared to do his own repairs - or be stuck. It is wise to know something about the engine and to carry a good set of tools along, as well as a tire repair kit.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 66

1176- 1177


E
PERZOARB
APOGEFLPQRBF
ABCDEFGHIJKL

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. Morphology: Negative Conditional or Contingent Forms.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Picture: The head and the sense organs.

b. Cultural item: A note about interpretation of senses as also reflected in the language.

c. Lexical items:

miwani	(spectacles, glasses)
midomo	(lips)
kinywa	(mouth, mouth cavity)
pua	(nose)
maarifa	(knowledge, information, senses)
sikio	(ear)
wimbo	(song)
ulimi	(tongue)
kelele	(noise, racket)
jino (pl. meno)	(tooth)
wezesha	(enable)
nusa	(small, sniff)
pimia	(measure or fit someone)
nuka	(smell (badly) stink)
nukia	(smell nicely, be fragrant)
tafuna	(chew, masticate)
tamka	(pronounce, articulate)
umbo	(shape)
kiungo	(organ of body)
milango ya maarifa	(the senses - sight, hearing, etc.)
fahamika	(recognizable, discernible)
harufu	(odor, smell)
matamshi	(pronunciation)
onja	(taste)(v)

1st PERIOD PERCEPTION DRILL LESSON 66

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drills using the Negative Contingent Tense.

a. Nisingenunua, (kama) nisingependa.
Nisingempa, (kama) nisingetaka.
Asingefanya, (kama) asingeweza.
Asingefaulu, (kama) asingejaribu.

b. (Kama) Tusingerudi, tusingemwona.
(Kama) Tusingeangalia, tusingefika.
(Kama) Wasingekula, wasingeshiba.
(Kama) Wasingemwona, wasingepata habari.

c. Singenunua, (kama) singependa.
Singempa, (kama) singetaka.
Hangefanya, (kama) hangeweza.
Hangefaulu, (kama) hangejaribu.

d. (Kama) Hatungerudi, hatungemwona.
(Kama) Hatungeangalia, hatungefika.
(Kama) Hawangekula, hawangeshiba.
(Kama) Hawangemwona, hawangepata habari.

e. Nisingalinunua, (kama) nisingalipenda.
Asingalifanya, (kama) asingaliweza.
(Kama) Tusingalirudi, tusingalimwona.
(Kama) Wasingalikula, hawangalishiba.

f. Singalimpa, (kama) singalipenda.
Hangalifaulu, (kama) hangalijaribu.
(Kama) Hatungaliangalia, hatungalifika.
(Kama) Hawangalienda upesi, hawangalimpata.

2. Drills using new expressions

a. Mtu ana milango ya maarifa.
Mlango mmoja ni kunusa kwa pua.
Mwingine ni kuona kwa macho.
Mwingine ni kusikia kwa masikio.

b. Pua ina uwezo kusikia harufu.
Pua ina uwezo kunusa.
Masikio yana uwezo kusikia sauti.
Masikio yana uwezo kusikia.

c. Macho yana uwezo kuona.
Watu wengine hawaoni vizuri.
Wao huenda kwa daktari ya macho.
Daktari atawapimia miwani.

d. Kinywani kuna meno mengi.
Meno ni ya kutafuna chakula.
Ulimi unatuwezesha kuonja chakula.
Ulimi unatusaidia kutamka maneno.

e. Harufu mbaya inanuka.
Harufu nzuri inanukia.
Masikio na macho ni viungo vya mwili.
Hata pua ni kiungo.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

2nd PERIOD SWAHILI DIALOGUE LESSON 66

1. Kichwa kina faida gani kwetu?

   Kichwani kuna viungo vya milango ya maarifa.

2. Hapo kichwani pana masikio, macho, na pua tu?

   Kuna hata kinywa pamoja na ulimi, meno na midomo.

3. Sauti zafahamika kwa njia gani?

   Masikio yetu mawili husikia sauti nyingi.

4. Macho yangu mawili yangetambua rangi tu?

   Yasingetambua rangi tu, hata umbo la vitu vingi.

5. Mtu akipata shida kuona vizuri angefanyaje?

   Asingeona vizuri, angepimiwa miwani.

6. Pua itaniwezesha kusikia harufu?

   Ukinusa kwa pua utasikia harufu mbalimbali.

7. Ikiwa harufu ni mbaya tusingesema inanukia.

   Ndio, na ikiwa harufu ni nzuri inanukia.

8. Meno kinywani yana faida gani?

   Meno ni ya kutafuna chakula na kusaidia matamshi.

9. Ulimi kinywani ni wa kuonja tu?

   La, ulimi ni msaada kwa kutamka maneno pia.

LESSON 66



1. Of what profit is the head to us?

   On the head are sense organs.

2. Are there only the ears, eyes, and nose on the head?

   There's also the mouth with the tongue, teeth and lips.

3. In what manner are the sounds comprehended?

   Our two ears can hear many sounds.

4. Would my two eyes recognize only colors?

   They wouldn't recognize just colors, but also the shape of many things.

5. If one should have trouble seeing well, what should he do?

   If he shouldn't see well, he should have glasses fitted.

6. Will the nose enable me to smell odors?

   If you smell with the nose, you'll pick up various odors.

7. If the odor is bad, we would not say it is fragrant.

   Yes, and if it is a pleasant odor, it is fragrant.

8. Of what use are the teeth in the mouth?

   The teeth are for chewing food and help in pronunciation.

9. Is the tongue only for tasting purposes?

   No, the tongue is also a help in speaking.

3rd PERIOD PATTERN DRILL I LESSON 66

Step 1. Repetition Drill

a. Kichwa kinafaida kwako.

miguu, macho, mkono

b. Sikio langu linaniuma.

masikio, viungo, mikono

c. Masikio yake yasingepona, angepelekwa hospitali.

viungo, kichwa, jicho

d. Kama sisi tusingetumia ulimi tusingetamka maneno.

wewe, mimi, ninyi

e. Usingefunua kinywa, usingeongea.

umia, imba

f. Asingekuwa na meno, asingetafuna chakula.

kula, pata, nunua

g. Kama ningesikia harufu mbaya ningeondoka hapa.

kaa, ngoja

h. Asingeondoka kwanza, angeshika ugonjwa.

pumzika, burudika, lala

i. Kama nisingeona vizuri ningetumia miwani.

nunua, pata, pimiwa

2. Substitution Drill

a. Usipotumia
---------- miwani utaharibika macho.
Usipotumia miwani utaharibika macho.

pata, pimiwa, nunua

b. wasingemwona
Kama ---------- daktari wangeumia sana.
Kama wasingemwona daktari wangeumia sana.

ita, lipa, pata

c. Usiponusa
--------- hutasikia harufu.
Usiponusa hutasikia harufu.

karibia, ngojea, inuka

d. Wasingetamka
---------- maneno vizuri tungewasaidia.
Wasingetamka maneno vizuri tungewasaidia.

jifunza, jua, elewa

e. tusingetafuna
Tusingekuwa na meno ---------- chakula.
Tusingekuwa na meno tusingetafuna chakula.

kula, pata, tumia

f. nawangaliinunua.
Wasingalitambua rangi ya nguo ----------

Wasingalitambua rangi ya nguo hawangaliinunua.

tamani, tumia, penda

g. wangaliona
Msingaliwafunga macho ---------- kila kitu.
Msingaliwafunga macho wangaliona kila kitu.

chukua, tambua, tazama

h. Harufu
------ isingalikuwa mbaya tusingalikasirika.
Harufu isingalikuwa mbaya tusingalikasirika.

wanafunzi, mtoto, vitabu

i. hatungewasaidia
Wasingeimba wimbo huo ---------- .
Wasingeimba wimbo huo hatungewasaidia.

lipa, karibisha, fukuza

Step 2. Language clab session (If applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the clab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 66

Step 1. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 2. Patterned response drill.

a. 1st: Kichwa kina faida kwako?
2nd: Ndio, kina faida sana kwangu.

mikono, masikio, jicho

b. 1st: Usingeuliza maswali ungefahamu?
2nd: La, singefahamu nisingeuliza maswali.

tosheka, furahi, elewa

c. 1st: Ikiwa waumwa na meno, utafanyaje?
2nd: Ikiwa naumwa na meno nitamwona daktari.

jicho, kichwa, viungo

d. 1st: Angepimiwa miwani angeona vizuri?
2nd: Kweli, angeona vizuri zaidi.

nunuliwa, patiwa, pewa

e. 1st: Angeng'olewa meno angetafuna chakula?
2nd: Angeng'olewa meno hangetafuna chakula.

kula, pata

Note: If facilities are available part of this period can be scheduled for a language clab session.

a. Asingetengeneza motokaa tungesafiri?
La, hatungosafiri asingetengeneza motokaa.

nunua, tayarisha, pata

b. Tusingalipimiwa miwani tungalifanyaje?
Tusingalipimiwa miwani hatungalifaulu.

tengeneza, nunua, pata

c. Walipopiga kelele aliwaambiaje?
Walipopiga kelele aliwafukuza.

vinanda, ngoma, tarumbeta

d. Tusipotamka maneno vizuri tutafaulu?
La, hatutafaulu tusipotamka maneno vizuri.

jifunza, jua, andika

e. Usipojaza pumzi katika tairi, tutaendelea?
La, hututaendelea nisipojaza pumzi katika tairi.

tia, ongeza

f. Alipoanguka alivunjika mkono?
La, hakuvunjika mkono alipoanguka.

ruka, kimbia, gongwa

g. Mekanika amesema tununue kabureta?
La, yeye hakusema tununue kabureta.

tafuta, pata, tengeneza

h. Mliponunua plagi mpya motokaa ili kwenda vizuri?
La, tuliponunua plagi mpya, motokaa haikuenda vizuri.

pata, tia, tengeneza

i. Ningekuimbia wimbo huo ungefurahi?
La, singefurahi ungeniimbia wimbo huo.

fundisha, onyesha

j. Mwala chakula gani wakati wa Krismasi?
Twala nyama na wali wakati wa Krismasi.

nunua, penda, tengeneza

k. Mwamrishe ale nyama kila siku.

onya, ambia, shauri

l. Usiwape motokaa hiyo.

onyesha, tengenezea, uzia

m. Midomo yake imejeruhiwa vibaya.

mguu, kichwa, jicho

n. Maneno yake hayafahamiki.

lugha, mafundisho, kitabu

o. Wenye maarifa watafaulu peke yao.

mali, akili, vitabu

6th PERIOD SITUATIONAL APPLICATION LESSON 66

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Mwalimu aliwafundisha wanafunzi wake juu ya milango ya maarifa. Alikuwa akiwaelezea jinsi kichwa ni sehemu muhimu sana ya mwili. Bila milango ya maarifa katika kichwa hatungeweza kuishi.

Hebu tuyachungue maarifa hayo. Kwanza kuna masikio, moja kila upande wa kichwa. Masikio yana uwezo kutambua sauti mbalimbali. Ikiwa ni sauti tamu ya nyimbo au muziki, mazungumzo ya watu, sauti za wanyama, au makelele fulani, sauti hizo zote zasikika kwa masikio. Hayo, basi, ni milango ya maarifa ya kusikia na kutambua sauti.

Baada ya hayo tuna macho mawili. Hayo yanatuwezesha kutambua rangi za kila aina. Wala si rangi tu, hata umbo wa vitu vyote. Bila macho tusingeweza kuona mahali tunapokwenda au uzuri wa maua na vitu vingi vingine. Watu wakipata shida kuona vizuri, daktari wa macho angeweza

kuwasaidia akiwapimia miwani. Kwa msaada wa miwani huweza kuona vizuri tena.

Pamoja na uwezo wa kusikia na kuona, kuna uwezo wa kunusa na kusikia harufu mbalimbali. Hapo mlango wa maarifa ni pua. Ikiwa harufu ni mbaya twasema kwamba inanuka, na kama ni nzuri kwamba inanukia.

Zaidi ya hayo katika kinywa kuna meno na ulimi. Ulimi ni msaada kwa kutamka maneno, lakini pia ni kiungo kinachotuwezesha kuonja. Hivyo twatambua kama chakula ni kikali au kitamu.

Step 2. Maswali:-

Milango ya maarifa yetu iko wapi?
Tungeweza kuishi vizuri bila msaada ya milango ya maarifa?
Kiungo ni nini?

Maelezo:-

Eleza mambo yanayohusika na masikio.
Eleza habari ya macho.
Eleza jinsi tunavyosikia harufu.
Eleza faida ya ulimi.

Step 3. Presentation of short narratives by students.

I. Language Structure

The negative contingent tenses are formed in two ways. Presently the more common form is to use affirmative subject prefixes followed by the negative particle 'si'. For example:-

a. Present negative contingent:- (si + nge)

ni - si - nge - penda, nisingependa
u - si - nge - penda, usingependa
a - si - nge - penda, asingependa
tu - si - nge - penda, tusingependa
m - si - nge - penda, msingependa
wa - si - nge - penda, wasingependa

b. Past Negative Contingent:- (si + ngali)

ni - si - ngali - penda, nisingalipenda
u - si - ngali - penda, usingalipenda
a - si - ngali - penda, asingalipenda
tu - si - ngali - penda, tusingalipenda
m - si - ngali - penda, msingalipenda
wa - si - ngali - penda, wasingalipenda

The other way which is also quite frequently used (perhaps a matter of taste or preference) is by using negative subject prefixes as we have learned to do in other negative tenses, and then omitting the negative particle 'si'. For Example:-

a. Present negative contingent:-

si - nge - penda, singependa
hu - nge - penda, hungependa
ha - nge - penda, hangependa
hatu - nge - penda, hatungependa
ham - nge - penda, hamngependa
hawa - nge - penda, hawangependa

b. Past negative contingent:-

si - ngali - penda, singalipenda
hu - ngali - penda, hungalipenda
ha - ngali - penda, hangalipenda
hatu - ngali - penda, hatungalipenda
ham - ngali - penda, hamngalipenda
hawa - ngali - penda, hawangalipenda

II. Cultural Note

This lesson deals with the sense organs, and so there is no particular cultural aspect. However, from the idiomatic or language point of view, some interesting usages should be noted.

a. There is no special Swahili word for the word 'feel'. Thus one does not feel cold, hot, hungry, or thirsty - rather one "sees" or "hears" these conditions.

e.g. Ninasikia baridi,
or: Ninaona baridi.

Anasikia njaa.
or: Anaona njaa.

b. The sense of smell is also expressed by 'hearing', thus:-

Tunasikia harufu nzuri.
Tunasikia harufu mbaya.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 67

1. LANGUAGE STRUCTURE

   a. Morphology: The MA Class of Nouns.

2. CONTENT STRUCTURE

   a. Situational picture: Various fruits growing in a field.

   b. Cultural Note: Fruit growing in East Africa.

   c. Lexical items:

ota	grow (a plant grows)
mmea	a plant
tunda	fruit
nanasi	pineapple
embe	mango
kijiji	village
chungwa	orange fruit
ua	a flower

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drill on Ma class words.

a. Shamba hili. — Mashamba haya.
Tunda hili. — Matunda haya.
Embe hili. — Maembe haya.
Chungwa hili. — Machungwa haya.

b. Soko lile. — Masoko yale.
Nanasi lile. — Mananasi yale.
Daraja lile — Madaraja yale.
Dirisha lile. — Madirisha yale.

c. Jina fupi. — Majina mafupi.
Ua zuri. — Maua mazuri.
Gari dogo. — Magari madogo.
Jeraha kubwa. — Majeraha makubwa.

d. Majani marefu.
Mavuno mengi.
Mahindi machache.
Maziwa matamu.

e. Mazoezi mengine.
Matata mabaya.
Majira mafupi.
Maisha marefu.

f. Shamba langu. — Mashamba yangu.
Tunda langu. — Matunda yangu.
Embe langu. — Maembe yangu.
Chungwa langu. — Machungwa yangu.

g. Soko lako. — Masoko yako.
Nanasi lako. — Mananasi yako
Daraja lako. — Madaraja yako.
Dirisha lako. — Madirisha yako.

h. Jina lake. Majina yake.
Ua lake. Maua yake.
Gari lake. Magari yake.
Jeraha lake. Majeraha yake.

i. Majani yetu.
Mavuno yetu.
Mahindi yetu.
Maziwa yetu.

j. Mazoezi yenu.
Matata yenu.
Majira yenu.
Maisha yenu.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Mashamba haya yote ni ya wenyeji?
   Ndio, wanapanda mimea mbalimbali.

2. Wanapanda matunda pia?
   Wanapanda matunda ya aina nyingi.

3. Mananasi yanaota vizuri hapa?
   Angalia kule, watu wanavuna mananasi.

4. Umepata kuonja machungwa yao?
   Ndio, ni matamu kweli.

5. Je, wanapanda maembe vilevile?
   Ndio, kuna mashamba mengi ya maembe.

6. Shamba hili ni la mahindi?
   Hilo ni la mahindi na maharagwe.

7. Mavuno yao wanauza wapi?
   Wana masoko madogo katika kijiji.

8. Wanauza matunda katika miji mikubwa?
   Ndio, hata katika nchi za mbali.

LESSON 67



1. Do all these gardens belong to natives?
   Yes, they grow various crops.

2. Do they grow fruit as well?
   They grow many kinds of fruit.

3. Do pineapples grow well here?
   Look yonder, people are harvesting pineapples.

4. Did you get to taste their oranges?
   Yes, they are very sweet.

5. Say, do they grow mangoes too?
   Yes, there are many fields with mangoes.

6. Is this a corn field?
   That's a field for corn and beans.

7. Where do they sell their crops?
   They have small markets in the villages.

8. Do they sell fruit in the big cities?
   Yes, even in distant lands.

3rd PERIOD PATTERN DRILL I LESSON 67

Step 1.

1. Repetition Drill

a. Mimi nina shamba.
Mimi nina shamba.

embe, nanasi, ua, tunda.

b. Wanataka kuvuna mahindi.
Wanataka kuvuna mahindi.

matunda, maua, machungwa, mananasi.

c. Tajiri aliwapa shamba hili.
Tajiri aliwapa shamba hili.

tunda, chungwa, nanasi, ua.

d. Ninauza matunda haya.
Ninauza matunda haya.

mashamba, maua, maembe, mananasi.

e. Ninataka kununua tunda lile.
Ninataka kununua tunda lile.

ua, chungwa, embe, nanasi.

f. Atapeleka mananasi yale sokoni.
Atapeleka mananasi yale sokoni.

matunda, maua, machungwa, mahindi.

2. Substitution Drill

a. ua.
Anataka kupanda --
Anataka kupanda ua.

tunda, chungwa, embe, nanasi.

b. ua zuri
Tulinunua -- ----
Tulinunua ua zuri.

embe, tunda, chungwa, nanasi.

c. mananasi makubwa.
Walivuna -------- -------
Walivuna mananasi makubwa.

maua, maembe, matunda, machungwa.

d. Tunda hilo
----- ---- linapendeza.
Tunda hilo linapendeza.

ua, nanasi, embe, chungwa.

e. mashamba haya madogo.
Watauza -------- ---- ------
Watauza mashamba haya madogo.

matunda, mananasi, maua, maembe.

Step 2. Language clab session (if applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the lab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment (recorded)

a. Dialogue and pattern drill practice.

b. Written work based on lesson 47.

c. Short narration based on the situational picture of the previous lesson.

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON 67

Step 1. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 2. Patterned response drill.

a. 1st: Wanauza mananasi matamu?
2nd: Ndio, wanauza mananasi matamu.

matunda, maembe, machungwa.

b. 1st: Tutaleta embe hili kubwa?
2nd: La, leteni lile dogo.

tunda, nanasi, embe, chungwa.

c. 1st: Maembe hayo hayatoshi?
2nd: Hayo hayatoshi kabisa.

mashamba, mahindi, maharagwe, mananasi.

d. 1st: Tunda hilo ni tamu?
2nd: Ni tamu kama sukari.

nanasi, chungwa, embe.

e. 1st: Watauza wapi maembe haya?
2nd: Watauza maembe haya sokoni.

matunda, maharagwe, maua, mananasi.

5th PERIOD RECOMBINATION DRILL LESSON 67

Note: If facilities are available this period can be scheduled for a language lab session.

a. Mnataka maziwa mazuri?
Tunataka maziwa mengi mazuri.

matunda, maji, maharagwe, mahindi

b. Alinunua tunda kubwa?
Alinunua tunda dogo tu.

manasi, shamba, embe, chungwa

c. Maadui hawa wametoka wapi?
Maadui hawa wametoka mbali.

maharagwe, maji, maua, matunda

d. Atatumia jina hili kule?
Ndio, atatumia jina hili.

tunda, nanasi, embe, chungwa

e. Ulinunua wapi maua yale?
Nilinunua maua yale sokoni.

mahindi, maziwa, matunda, maembe

f. Unauza embe lile?
Embe lile siuzi.

shamba, ua, nanasi, chungwa

g. Utapeleka maua hayo?
Sitapeleka maua hayo.

maharagwe, matunda, mananasi, maembe.

h. Ungeona <u>maembe</u> ungeyanunua?
Ndio, ningeyaona ningeyanunua.

chungwa, mkuki, chakula

i. Alipoyala <u>maembe</u> alifurahi?
Alifurahi alipoyala maembe.

nanasi, mkate, mayai

j. <u>Ungalikuwa na</u> motokaa ungalifanyaje?
Ningalikuwa na motokaa ningaliitumia.

nunua, pata

k. <u>Wanapokwenda</u> sokoni wanauza nini?

Wanapokwenda sokoni wanauza maharagwe.

ingia, fika, rudi

l. <u>Nikikuuzia</u> matunda utayanunua?
La, ukiniuzia matunda sitayanunua.

letea, patia, onyesha

m. Je unajua <u>majina</u> ya watoto hawa?
La, siyajui majina yao.

wazazi

6th PERIOD SITUATIONAL APPLICATION LESSON 67

Step 1. Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Wenyeji wengi wamepanda mimea mbalimbali katika mashamba yao. Walipanda wakati wa mvua na mimea ilotokea na kuota vizuri. Sasa wanajitayarisha kwa mavuno.

Katika shamba moja kuna mahindi na maharagwe. Wengine wanatunza matunda vilevile na kuna miti ya matunda, hasa michungwa na miembe. Kutoka miti hiyo wanavuna machungwa na maembe. Wenyeji wengine wamepanda nanasi na sasa wanavuna mananasi matamu.

Wenyeji wanakaa katika kijiji kidogo hapa karibu na wanapeleka mavuno sokoni kwa lori. Kule sokoni wanunuzi watapeleka matunda yale makubwa na mazuri katika soko kubwa la Nairobi. Labda mengine watayapeleka katika nchi ya mbali.

Step 2. Questions based on the above narration:

Nani amepanda mimea?
Walipanda mimea ya namna gani?
Walipanda wakati gani?
Mimea iliota vizuri?
Wanajitayarisha kufanya nini?

Walipanda mahindi pamoja na nini?
Kutoka michungwa watavuna nini?
Kutoka miembe watavuna nini?
Walipanda matunda gani tena?
Hayo yalikuwa matamu?

Wenyeji wanakaa wapi?
Wanapeleka wapi mavuno?
Watayapeleka kwa njia gani?
Wanunuzi watapeleka wapi matunda?
Unafikiri mengine yatakwenda mbali?

Note: When answering the above questions, students should do so by using complete sentences.

Step 3. Presentation of short narratives prepared by students.

I. Language Structure

The MA class of nouns has the following features:

a. There is no prefix in the singular, except:

i. When it is a word of one syllable, then the singular prefix would be JI.

e.g. ji-cho zuri (a good eye)
ji-we ji-pya (a new stone)

ii. When it is a word beginning with a vowel, then the singular prefix would be J.

e.g. j-ino dogo (a small tooth)
j-ino j-eupe (a white tooth)

b. In the plural the prefix is MA. Note that when the stem begins with a vowel, the two vowels will combine as follows:-

MA + E -- = ME --
MA + I -- = ME --

With the vowels A, U and O there is no vowel contraction.

MA + A -- = MAA --
MA + U -- = MAU --
MA + O -- = MAO --

e.g. Ma + ema = mema
Ma + ingi = mengi
Ma + andiko = maandiko
Ma + ua = maua
Ma + oni = maoni

c. Thus for nouns and adjectives, we can summarize as follows:-

Singular	Plural
JI (monosyllabic stem)	Ma
J (vowel stem)	Ma, Me
__ (no prefix)	Ma

d. In the case of pronouns, and words derived from pronouns, we have:-

(i) li (it), ya (they)

Thus with verbs the following constructions would be used:

Jino limevunjika.
(The tooth is broken.)
Meno yamevunjika.
(The teeth are broken.)
Tunda linapendeza.
(The fruit is pleasing.)
Matunda yanapendeza.
(The fruit (pl.) is pleasing.)

(ii) With demonstratives:-

hili (this)	haya (these)
lile (that)	yale (those)

(iii) Possessive pronouns:-

jina langu	majina yangu
jina lako	majina yako
jina lake	majina yake
jina letu	majina yetu
jina lenu	majina yenu
jina lao	majina yao

II. Cultural Note

Fruit growing has possibilities in East Africa, but so far it has not been done on an extensive scale. A few enterprising Europeans have raised pineapples, oranges, grapefruit in quantities for canning and export.

The popular tropical fruits grown by the Africans primarily, often as a staple fruit and vegetables, are bananas, of which there are many varieties. At the coast mangoes are popular, as well as coconuts and dates. Good, sweet and large sized papayas are grown everywhere.

Fruits such as apples, plums, peaches, etc., are grown only experimentally in the higher cool altitudes. They are not too successful. Much of this type of fruit used to be imported from South Africa.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 68



1214

LESSON 8

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. Morphology: Ma Class reinforcement.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational picture: Builders and carpenters at work on a building.

b. Cultural Note: East African carpenters and masons.

c. Lexical items:

msingi	foundation
sakafu	floor
ukuta	wall
paa	roof
dari	ceiling, upstairs
orofa	story (building)
sebule	vestibule
simenti	cement
jiwe (ma-)	stone
tofali (ma-)	brick
rangi	color
kupaka rangi	paint (v.)
msumeno	saw
kukata kwa msumeno	saw (v.)
randa	plane
kuranda	to plane
patasi	chisel
kutoboa kwa patasi	to chisel out
nyundo	hammer
piga kwa nyundo	hammer (v.)
msumari	nail
pigilia msumari	drive in a nail
sukurubu	screw
spana	wrench, spanner
playa, plaisi	pliers
bati (ma-)	iron sheeting
bawaba (ma-)	hinge
kufuli (ma-)	lock, padlock
bisibisi	screw driver
skru draiva	screw driver
seremala	carpenter
mwashi	mason

1st PERIOD PERCEPTION DRILL LESSON 68

Note: The situational picture will be used as an aid during this period in connection with Step 3.

Step 1. Auditory perception and comprehension.

Step 2. Oral production of minimum utterances.

1. Drills using Ma class forms.

a. Tunda hili - matunda haya.
Jina hili - majina haya.
Ua hili - maua haya.
Sanduku hili - masanduku naya.

b. Sikio lile - masikio yale.
Jicho lile - macho yale.
Jino lile - meno yale.
Jiwe lile - mawe yale.

c. Jina langu - majina yetu.
Jina lako - majina yenu.
Jina lake - majina yao.

d. Ua linanukia vizuri.
Maua yananukia vizuri.
Tunda limeiva kabisa.
Matunda yameiva kabisa.

e. Ofisa huyu - maofisa hawa.
Fundi huyu - mafundi hawa.
Seremala yule- maseremala wale.
Karani yule - makarani wale.

2. Drills using new expressions.

a. Vyombo vya seremala.
Msumeno wa kukata mbao.
Patasi la kutoboa shimo.
Nyundo ya kupigilia misumari.

b. Vyombo vingine vya mekanika.
Spana ya kukasa nati.
Playa ya kushika bolti.
Bisibisi ya kuingiza sukurubu.

c. Chumba kina sakafu.
Tena chumba kina dari.
Hata kina madirisha.
Na kina kuta nne.

d. Jengo kubwa la orofa kumi.
Mawe ya kujenga msingi.
Matofali ya kujenga ukuta.
Simenti ya kuunganisha matofali.

e. Mabati ya kuezeka paa.
Simenti ya kutengeneza sakafu.
Bawaba la kushika mlango.
Kufuli la kufunga mlango.

f. Mwashi ni fundi wa kujenga.
Seremala ni fundi wa kuranda.
Mshonaji ni fundi wa kushona.
Mekanika ni fundi wa kutengeneza motokaa.

Step 3. Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Tutajenga jengo jipya kwetu mjini.
   Hilo litakuwa jengo la biashara?

2. Ndio, litakuwa na orofa tano.
   Litakuwa jengo la mawe au matofali?

3. Jengo la matofali, na juu paa litakuwa la mabati.
   Sakafu ya kwanza itakuwa ya simenti, sivyo?

4. Ndivyo, sasa mafundi kama ishirini wamejitayarisha.
   Waashi wataweka msingi imara karibuni?

5. Ndio, na halafu wataendelea kujenga kuta.
   Maseremala wameleta vyombo vyao?

6. Wameleta misumeno, randa, patasi na nyundo.
   Watafungia milango na madirisha kwa bawaba?

7. Ndivyo, na baadaye watatia vitasa vilevile.
   Wataingiza masukurubu kwa bisibisi?

8. Hasa, na misumari hupigilia kwa nyundo.
   Haikosi mwishoni watapaka rangi vilevile.

LESSON 68



1. We'll be putting up a new building in our town.

   Will that be a business building?

2. Yes, it will be one of five stories.

   Will it be a stone or brick building?

3. A brick building, and on top it will have a corrugated iron roof.

   The first floor will be of concrete, isn't that right?

4. Yes, now about twenty craftsmen are getting ready?

   Will the masons put in a strong foundation soon?

5. Yes, and afterwards they'll put up the walls.

   Did the carpenters bring their tools?

6. They brought saws, planes, chisels and hammers.

   Will they fasten the doors and windows with hinges?

7. Yes, and afterwards they'll put in locks as well.

   Will they put in screws by means of screwdrivers?

8. Surely, and they'll drive in the nails with hammers.

   Without a doubt, at the end they'll also put on paint.

3rd PERIOD PATTERN DRILL I LESSON 68

Step 1. Repetition Drill

a. Jengo jipya limejengwa mjini.

maboma, nyumba, msikiti

b. Makufuli haya hayafai.

kufuli, spana, seremala

c. Ameuvunja msumeno wake.

playa, bisibisi, misumeno

d. Tafadhali nipatie randa mbili.

Letea, nunulia, tengenezea

e. Waashi wasipojihadhari wataanguka.

mwashi, wewe, ninyi

f. Usiweke msumari huo hapo.

pigilia, ficha, rudisha

g. Waambie wajenge nyumba ya orofa mbili.

amrisha, shauri

h. Msipake rangi milango hii.

milango, nyumba, sakafu

i. Juma alijijengea nyumba ya matofali.

sisi, walimu, mimi

2. Substitution Drill

a. maseremala
Waambie ---------- walete vyombo.
Waambie maseremala walete vyombo.

seremala, mafundi, fundi

b. Hatutajenga
---------- nyumba ya mawe.
Hatutajenga nyumba ya mawe.

nunua, hitaji, tumia

patasi
c. Mngezileta ------ zenu tungezitumia.
Mngezileta patasi zenu tungezitumia.

nyundo, mabati, misumari

d. mafundi
Tuliwaletea ------- nyundo na misumari.
Tuliwaletea mafundi nyundo na misumari.

fundi, wewe, ninyi

e. Jiwe
---- kubwa limeziba mlango.
Jiwe kubwa limeziba mlango.

mawe, tofali, bati

f. achanganye
Mwambie ---------- simenti sasa.
Mwambie achanganye simenti sasa.

leta, tayarisha, tumia

g. Waliezeka
--------- nyumba kwa matofali.

Waliezeka nyumba kwa matofali.

jenga, tengeneza

h. kijana
Mfundishe ------ kutumia patasi.
Mfundishe kijana kutumia patasi.

vijana, mimi, sisi

i. mti
Waukata --- mrefu kwa msumeno.
Waukata mti mrefu kwa msumeno.

miti, mbao, ubao

Step 2. Language clab session (If applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the clab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3. Homework assignment

4th PERIOD (First hour in the morning) LESSON [illegible]

Step 1. Recitation of the dialogue.

PATTERN DRILL II

Step 2. Patterned response drill.

a. 1st: Jengo hilo ni la mawe au ni la matofali?
2nd: Hilo ni jengo la mawe.

nyumba, ukuta, majengo

b. 1st: Wasipomaliza msingi leo, utafanyaje?
2nd: Wasipomiliza msingi leo nitawafukuza.

tengeneza, jenga, tayarisha

c. 1st: Umewaambia maseremala walete vyombo?
2nd: La, sijawaambia walete vyombo.

nunua, tumia, tafuta

d. 1st: Mafundi watatumia nini kuingiza masukurubu?
-refu (2) - tall, long
rejista (29) - register
reli (34) - railway, railroad
reli kuu (56) - main line
reli ya njia mbili (63) - 2 track railroad
ridhika (49) - (be) contented
ripoti (12) - report
risasi (16) - bullet
riziki (64) - necessities of life
robo (30) - quarter
rudi (6) - return
ruhusa (25) - permission, allow, permit
ruka (12) - jump, fly
rukia (60) - jump upon by surprise

S

saa (10) - clock, watch
saa sita usiku (30) - midnight
saba (18) - seven
sababu (13) - because
sabaini (23) - seventy
sabuni (45) - soap
safari (14) - journey
safi (10) - clean
safiri (14) - travel (v)
safirisha (35) - transport
safisha (8) - clean
sahani (48) - plate
saidia (4) - help
saidiana (40) - help each other

Sajini (12) - Sergeant
Sajini meja (12) - Sgt. Major
sakafu (68) - floor
salama (14) - safely
salamu (1) - greetings
salimia (13 - greet
samaki (26) - fish
sana (7) - very
sanduku (17) - box
sasa (3) - now
sasa hivi (18) - at once
sauti (15) - sound, voice
sawa (20) - like, same
sawasawa (10) - properly
sebule (68) - entrance hall
sehemu (33) - part
sema (3) - say, speak
senti (29) - cents
seremala (68) - carpenter
Septemba (32) - September
serikali (36) - government
shabaha (13) - target, aim
shaka (47) - fear, doubt, worry
shamba (4) - field, garden
shambulia (23) - attack
shambulio (61) - an attack
shanga (44) - beads
shaba (64) - copper, brass
shati (44) - shirt
shauri (59) - advice
shauriana (69) - consult with
sheria (25) - law, custom
shiba (55) - be full, satisfied (after a meal)
shida (33) - trouble, difficulty
shidwa (63) - be unable, be defeated
shika (7) - hold
shilingi (22) - shilling
shimo (40) - hole
shinda (28) - win
shindana (28) - compete
shindano (28) - competition
shirikiana (70) - cooperate
shirikisho (70) - cooperation
shona (8) - sew
shonea (45) - sew for someone
shuka (20) - come down
si (1) - am not, is not
siagi (48) - butter
siasa (70) - politics
sigara (8) - cigarette
sikia (13) - hear
sikiliza (39) - listen
sikio (66) - ear
siku (20) - day
sikukuu (31) - holiday
silaha (13) - weapon
simama (3) - stand
simamisha (69) - make stand, erect
simba (11) - lion
simenti (68) - cement
simu (63) - signal, wire, telegram
sindano (45) - needle
sinema (49) - cinema, movie
sisi (5) - we
sita (18) - six
sitini (23) - sixty
sivyo (14) - not so
soko (20) - market
soksi (44) - socks
soma (19) - read
songana (20) - crowded
spana (68) - wrench, spanner
staarabika (34) - be civilized
stahili (64) - deserve
starehe (49) - relax, be comfortable
stempu (29) - stamp
stesheni (53) - station, train station
stesheni ya kupokea (69) - receiving station
stesheni ya kutuma (69) - transmitter station
stoo (41) - store, storage place
subulkheri (45) - Good morning
sufuria (52) - pot, pan

sugua (54) - polish, rub
sukari (48) - sugar
sukuma (23) - push
sukurubu (68) - screw
sumu (13) - poison
suruali (44) - pants
suti (44) - suit
swala (11) - antelope
swali (62) - question
swichi (57) - switch

T

taa (57) - lamp
taabu (51) - difficulty, trouble
taa ya sitima (57) - electric light
tabia ya nchi (35) - climate of a country
tafadhali (10) - please
tafuta (4) - look for
tafuna (66) - chew, masticate
taga (58) - lay eggs
tai (44) - tie (also eagle)
taifodi (47) - typhoid
tairi (65) - tire
taja (31) - name, mention
taka (3) - want
takataka (54) - rubbish
tamaa (53) - hope, desire
tamani (59) - desire
tambua (30) - realize, recognize
tamka (66) - pronounce, articulate
tangazo (39) - sign, notice, announcement
tangi (65) - tank
tangu (36) - since
-tano (5) - five
taratibu (54) - carefully, with care
tarehe (32) - date
tarumbeta (28) - trumpet
piga tarumbeta (28) - play the trumpet
-tatu (5) - three
taulo (45) - towel
tawala (36) - rule, (v)
tayari (17) - ready
tayarisha (16) - get ready
tazama (5) - watch, look at
teka (61) - ransack, capture
teksi (53) - taxi
tele (13) - plenty
tembea (8) - walk
tembelea (42) - visit (v)
tembo (11) - elephant
tena (38) - moreover, again
tengeneza (3) - fix, repair
thamani (64) - value
thelathini (16) - thirty
theluji (34) - snow
thenashara (50) - dusk, 6. P.M.
thumni (sumni) (64) - a coin worth 50 cents
tia (8) - put
tikiti (53) - ticket
tisa (18) - nine
tisini (28) - ninety
tisha (27) - frighten, scare
tivii (69) - TV
toa (51) - to give, take out
toboka (17) - punctured
tochi (57) - torch, flashlight
tofali (ma-) (68) - brick
tofauti (26) - different
toka (6) - go out
tokea (38) - happen, to appear
tolewa (33) - issued
toroka (12) - escape, run away
tosha (9) - be enough
toshea (52) - enough for, satisfy
toza faini (53) - pay penalty
tu (9) - only
tuma (35) - send
tumaini (56) - hope, trust

tumbo (21) - stomach
tumia (20) - use
tunda (67) - fruit
tundika (54) - hang up
tunza (24) - take care of
tupa pesa (64) - squander money
twiga (11) - giraffe

U

ua (67) - a flower
ua (13) - kill
ubaguzi (70) - segregation, separation
uchafu (47) - filth, dirt
uchaguzi (70) - election, choosing
uchumi (36) - produce (n)
ufunguo (15) - key
ugali (26) - mush
Uganda (14) - Country of
ugonjwa (21) - sickness
uhuru (33) - freedom, independence
ujao (47) - next, coming
uji (50) - porridge
ukuta (68) - wall
ulimi (66) - tongue
uliza (35) - ask
umbo (66) - shape
umbali (56) - distance
umia (21) - hurt
umiza (43) - hurt, cause to hurt
uma (46) - bite
umri (32) - age
umwa (46) - be bitten
unga (55) - flour
Unguja (17) - Island of Zanzibar
upande (20) - side
upepo (32) - wind, breeze
upesi (10) - quickly
upungufu (49) - shortage
urefu (34) - length
usafi (47) - cleanliness
usiku (12) - night
usiku wa manane (30) - midnight
uso (45) - face
ustaarabu (37) - civilization
utambi (57) - wick
utaratibu (50) - routine, order
utawala (36) - rule, reign
uza (20) - sell
uzi (45) - thread

V

vaa (19) - to wear
vema (35) - good, fine
viazi (41) - potatoes
vibaya (43) - badly
viberiti (39) - matches
viburudisho (48) - refreshments
vidanganya macho (63) - camouflage
vilevile (4) - also
vizia (60) - spy on
vizuri (10) - well
-vua samaki (26) - fish (v)
-vuka (26) - cross over
vuli (32) - small rains
vuma (60) - blow, wind
vumbua (37) - discover
vumilia (53) - (be)patient
vuna (24) - reap, harvest
vunja (25) - break
vunjika (43) - break, get broken
vuta (8) - pull
vuta sigara (39) - smoke cigarette

W

Wachagga (34) - Chagga tribe
Waislamu (31) - Muslims
waka (57) - burn, be alight
wakati (15) - time
wakia (55) - ounce
Wakristo (31) - Christians
wala (32) - neither, nor

wali (19) - cooked rice
wao (5) - they
wapi? (4) - where?
washa (39) - light up
wazazi (49) - parents
waya (65) - wire
wazi (15) - open
waziri (70) - minister
waziri mkuu (70) - prime minister
waziwazi (42) - open, partly open
weka (17) - put, place
wembe (45) - razor
wewe (1) - you
weza (12) - (be) able
wezesha (66) - enable
wiki (26) - week
-wili (5) - two
wimbo- song (66)
winda (11) - hunt
woga (62) - fear

ziba (43) - stop up
zibwa (37) - stopped up, dammed up
zidi (55) - increase, be more
-zima (2) - well, whole
zimisha (39) - put out (light or fire)
-zito (27) - heavy
ziwa (26) - lake
zizi (58) - cowshed, pen, enclosure for animals
zuia (35) - hinder
zunguka (60) - go round, surround
zungumza (69) - to chat, to converse
-zuri (2) - good, nice

Y

yaani (36) - "that is", "which means"
yai (58) - egg
ya kutosha (34) - enough, sufficient
yelo-fiva (47) - yellow fever
yeye (1) - he, she
yodini (62) - iodine
yule (4) - that

Z

zaa (24) - bear, give birth
zaidi (38) - more
zamani (36) - long ago
zawadi (28) - reward, prize
pata zawadi (28) - get a reward
toa zawadi (28) - give a reward

EDO 325546

DEFENSE LANGUAGE INSTITUTE

SWAHILI

BASIC COURSE

VOLUME VI
LESSONS 71-84

AL 002 124

DEPARTMENT OF DEFENSE

S W A H I L I

Basic Course

Volume VI

Lessons 71 - 84

April 1966

DEFENSE LANGUAGE INSTITUTE

PREFACE

The Swahili Course, consisting of 145 lessons in 10 volumes, is one of the Defense Language Institute's Basic Course Series. The material was developed at the Defense Language Institute and approved for publication by the Institute's Curriculum Development Board.

The course is designed to train native English language speakers to Level 3 proficiency in comprehension and speaking and Level 3 proficiency in reading and writing Swahili. The texts are intended for classroom use in the Defense Language Institute's intensive programs employing the audio-lingual methodology. Tapes accompany the texts.

All inquiries concerning these materials, including requests for authorization to reproduce, will be addressed to the Director, Defense Language Institute, U. S. Naval Station, Anacostia Annex, Washington, D. C. 20390.

C. W. CHANEY
Colonel, U.S. Army
Director

C O N T E N T S

	Page
LESSON 71	1283
LESSON 72	1301
LESSON 73	1317
LESSON 74	1339
LESSON 75	1359
LESSON 76	1375
LESSON 77	1397
LESSON 78	1417
LESSON 79	1439
LESSON 80	1459
LESSON 81	1477
LESSON 82	1495
LESSON 83	1511
LESSON 84	1527
SOME NOTES ON COMPOUND TENSES . . .	1544
VOCABULARY LIST - LESSONS 71-84 . . .	1549

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 71

1. Language Structure

   a. The Relative Pronoun as an infix with the three primary tenses.

      Refer to Generalization for explanation of structural features in this lesson.

2. Content Structure

   a. Situational Setting: An outdoor organizational meeting.

   b. Cultural Note: Organization of societies.

   c. Lexical Items:

hudhurungi	(brown)
hutubu	(give a speech)
kaa kimya	(keep quiet or still)
kutanika	(assemble, gather together)
masharubu (pl)	(moustache)
mkutano	(gathering, meeting)
mwandishi	(secretary)
mwandishi mdogo	(2nd secretary or under-secretary)
mwenye kiti	(chairman)
nyamaza	(shut up)
paaza sauti	(raise voice)
tangulia	(precede, go on ahead)
tawanyika	(scatter)
umati	(crowd)

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features in this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on personal relative pronouns.

a. Anayevaa shati
Aliyeketi
Atakayesimamama

b. Wanaofanya
Waliopigana
Watakaopata

c. Mti unaoanguka
Mti uliosimama
Mti utakaopandwa

d. Miti inayoanguka
Miti iliyosimama
Miti itakayopandwa

e. Kikombe kinachojaa
Chakula kilichotosha
Kidonda kitakachopona

f. Vikombe vinavyofaa
Vitu vilivyopotea
Vyakula vitakavyokwisha

g. Kazi inayofaa
Ramani iliyotolewa
Taa itakayong'aa

h. Ndizi zinazoanguka
Nguo zilizopasuka
Taa zitakazong'aa

i. Jina linaloitwa
Jiwe lililoanguka
Tunda litakalopendeza

j. Maji yanayozibwa
Madirisha yaliyovunjika
Majengo yatakayojengwa

2. Semantic drills.

a. Mwenye kiti
Mwenye kusema
Mwenye sauti

b. Mwandishi
Mwandishi mdogo
Mwandishi anaandika

2. Semantic drills continued:

c. Umati wa watu
Umati mkubwa
Umati wa wanachama

d. Fungua mkutano
Ongoza mkutano
Komesha mkutano

e. Sauti kubwa
Sauti ndogo
Paaza sauti

f. Watu waliotangulia
Watu walionyamaza
Watu waliokaa kimya

g. Shati ya hudhurungi
Suti ya hudhurungi
Viatu vya hudhurungi

h. Alihutubu
Mwenye kiti alihutubu
Rais alihutubu

Step 3
Hatua ya 3 Association of utterances with their referents, (situational stimuli). Further imitation and repetition.

The above drills will now be given with the aid of the situational picture.

1. Watu wanaokutanika pale wanangojea nini?
   Wanamngojea mwenye kiti wa chama chao.

2. Yule anayevaa shati ya hudhurungi ni nani?
   Huyo ni mwandishi wa chama.

3. Viongozi wanafika, watakaohutubu ni nani?
   Watakaohutubu wanashika viti vyao sasa.

4. Atakayefungua mkutano ni nani?
   Mwenye kiti atafungua mkutano.

5. Ni yeye aliyefungua mkutano Jumapili iliyopita?
   Ndio, mwangalie vizuri, ana masharubu marefu.

6. Mkutano unaanza; wanaopiga kelele watanyamaza?
   Wote watakaa kimya baada ya dakika chache.

7. Baada ya mkutano umati utatawanyika?
   Ndio, wanachama waliotoka mbali watarudi kwao.

8. Wengine watabaki mjini?
   Watakaobaki mjini wataondoka kesho.

LESSON 71



1. What are those people who are gathering there waiting for?
   They are waiting for the chairman of their society.

2. Who is that fellow wearing a brown shirt?
   That's the secretary of the society.

3. The leaders are arriving; who will be the speakers?
   The speakers are taking their seats now.

4. Who will open the meeting?
   The chairman will open the meeting.

5. Is it he who opened the meeting last Sunday?
   Yes, look at him well, he has a long moustache.

6. The meeting is beginning; will those noisy ones shut up?
   All will keep quiet after a few minutes.

7. Will the crowd scatter after the meeting?
   Yes, the members who came from far away will return home.

8. Will others remain in town?
   Those who stay over in town will leave tomorrow.

Step 1.
Hatua ya 1.

1. Repetition Drill

a. Kijana anayekuja ni mwalimu.
Kijana anayekuja ni mwalimu.

lima, simama, soma, kimbia

b. Watu wanaopigana ni askari.
Watu wanaopigana ni askari.

rudi, tembea, ingia, ondoka

c. Daktari aliyeondoka amerudi.
Daktari aliyeondoka amerudi.

faulu, anguka, toroka, hutubu

d. Viongozi waliohutubu wameondoka.
Viongozi waliohutubu wameondoka.

simama, kuja, pumzika, fanya kazi

e. Mwanamke atakayelima anaongea.
Mwanamke atakayelima anaongea.

shindana, saidia, fagia, andika

2. Substitution Drill

a. waliongojea
Wakulima ---------- watafaulu.
Wakulima waliongojea watafaulu.

kutanika, hutubu, andika, burudika.

b. atakayechelewa
Mvuvi ---------- ataonekana.
Mvuvi atakayechelewa ataonekana.

iba, toroka, lalamika, rudi

c. anayefundisha
Mwalimu ---------- ni mkubwa.
Mwalimu anayefundisha ni mkubwa.

lala, kagua, winda, ngoja

d. waliorudi
Wanawake ---------- wataondoka.
Wanawake waliorudi wataondoka

pumzika, pika, shindana, tazama

e. wanaowinda
Wenyeji ---------- wanafurahi.
Wenyeji wanaowinda wanafurahi.

cheza, safari, saidia, simama

Step 2
Hatua ya 2 Language clab session (if applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the clab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3
Hatua ya 3 Homework assignment

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 71

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 71

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the dialogue

PATTERN DRILL II - MAZOEZI

Step 2
Hatua ya 2 Patterned response drill

a. 1st: Wanachama waliokutanika walisongana?
2nd: Walisongana sana.

ingia, sikiliza, simama, keti

b. 1st: Atakayefungua mlango ni nani?
2nd: Atakayefungua mlango ni mpelelezi.

vunja, funga, bomoa, choma

c. 1st: Mswahili anayeketi ni Ali?
2nd: Mswahili anayeketi si Ali.

lima, lala, tazama, kimbia

d. 1st: Wakulima watakaorudi watafurahi?
2nd: Ndio, watafurahi.

burudika, abudu, safiri, faulu

e. 1st: Ulimwona simba aliyekufa?
2nd: Ndio, nilimwona huyo.

kimbia, ruka, simama, lala

90.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 71

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 71

Note: If facilities are available, this period can be scheduled for a language clab session.

a. Nani aliyekupiga?
Aliyenipiga ni mwivi.

tuma, ita, taja, fuata

b. Watakaoshindana wamefika?
Hawajafika wote.

safiri, shambulia, winda, fanya kazi

c. Watoto wanaosoma ni wavivu?
Watoto wanaosoma si wavivu.

cheza, kimbia, lala, piga kelele

d. Watu walioshindwa wameondoka?
Walioshindwa wameondoka wote.

iba, lala, pumzika, shinda.

e. Mwandishi atakayefaulu anasoma?
Ndio, anasoma sasa.

ondoka, pumzika, hutubu, fika

f. Mtu anayelala ni mwalimu?
Ndio, ni mwalimu.

simama, kimbia, cheka, tembea

g. Mwivi aliyetoroka ni huyu?
Ndio, ni huyo.

iba, ingia, ruka, jificha

h. Kikombe kinachofaa ni hiki?
Ndio, ni hicho.

vitu, kazi, barua, mkeka

i. Ungependa kutazama miti iliyoanguka?
Ndio, ningependa kuitazama.

watoto, mlango, matunda, jengo

j. Watu waliojadiliana wamerudi?
Ndio, walirudi jana.

viongozi, wanachama, Mawaziri, wanafunzi

k. Watoto waliopotea wameonekana?
Ndio, walionekana juzi.

ramani, viatu, kijana, mtumbwi

l. Mwenye kiti atakayehutubu amesimama?
Ndio, amesimama sasa.

Walimu, Rais, Kiongozi, Jemedari

m. Nguo zilizopasuka ni zako?
Ndio, ni zangu.

karatasi, bahasha, kanga, suti

6TH PERIOD | SITUATIONAL APPLICATION | LESSON 71

KIPINDI CHA 6 | HADITHI | SOMO LA 71

Step 1
Hatua ya 1 Presentation of a narrative based on the dialogue. The situational picture will be used.

Tazama umati mkubwa wa wanaume na wanawake kule kiwanjani. Wamekutanika leo kumsikiliza kiongozi wa chama. Watu waliokutanika ni wanachama wa chama cha biashara. Sasa wanamngojea mwenye kiti afungue mkutano.

Yule anayeketi sasa ni mwenye kiti. Yeye ni kiongozi hodari. Mwandishi ni yule anayevaa shati ya hudhurungi. Wengine wanaosimama karibu ni viongozi wengine wema.

Wote wanaosema kwa sauti kubwa na kupiga kelele sasa, watanyamaza. Watakaa kimya, mwenye kiti atakapofungua mkutano, na atakapopaaza sauti yake.

Baada ya mkutano, watu waliotoka mbali watabaki na watalala mjini usiku. Wanaokaa karibu watatangulia kuondoka leo. Hivi wote watatawanyika upesi. Mwandishi, aliyeandika habari za mkutano kitabuni, atabaki kusema na mwenye kiti.

Step 2
Hatua ya 2 Questions based on the above narration:

6TH PERIOD | SITUATIONAL APPLICATION | LESSON 71

KIPINDI CHA 6 | HADITHI | SOMO LA 71

Waliokutanika ni nani?
Umati wa watu ni watu wachache?
Watu wamekutanika wapi?
Wanamngojea nani?

Mwenye kiti atafanya nini?
Anayeketi ni nani?
Nani hodari?
Nani anavaa shati ya hudhurungi?
Wanaosimama karibu ni nani?

Watu wanasema kwa sauti ndogo?
Watanyamaza baadaye?
Nani atapaaza sauti?
Waliotoka mbali watalala wapi?
Mwandishi atafanyaje?

Step 3
Hatua ya 3 Presentation of short narratives prepared by students.

I. LANGUAGE STRUCTURE

1. The Relative Pronoun "who" or "which" is expressed in Swahili by the letter "o" combined with the subject prefix. This then becomes a new infix which is inserted into the verb form right after the tense sign as explained in paragraph #2.

Study the following table carefully:-

	Sing.	Plur.
Wa or Living Class	yu + o = ye*	wa + o = o
Mi Class	u + o = o	i + o = yo
Ki Class	ki + o = cho	vi + o = vyo
N Class	i + o = yo	zi + o = zo
Ma Class	li + o = lo	ya + o = yo

From the above you will have noted that the Living Class singular* "ye" is irregular. Here are a few examples showing how these relative infixes are used:-

Singular: Wa Class

Mtu anayesimama	=	A person who is standing
Mtu aliyefika	=	A person who came
Mtu atakayekwenda	=	A person who will go

Plural: Wa Class

Watu wanaosimama	=	People who are standing
Watu waliofika	=	People who came
Watu watakaokwenda	=	People who will go

Singular: Mi Class

Mti unaosimama	=	The tree which is standing
Mti uliovunjika	=	The tree which broke
Mti utakaopandwa	=	The tree which will be planted

Plural: Mi Class

Miti inayosimama	=	The trees which are standing
Miti iliyovunjika	=	The trees which broke
Miti itakayopandwa	=	The trees which will be planted

Singular: Ki Class

Kitu kinachopendeza	=	The thing which is pleasing
Kitu kilichovunjika	=	The thing which broke
Kitu kitakachoanguka	=	The thing which will fall

Plural: Ki Class

Vitu vinavyopendeza	=	The things which are pleasing
Vitu vilivyovunjika	=	The things which broke
Vitu vitakavyoanguka	=	The things which will fall

Singular: N Class

Nyumba inayobomoka	=	The house which is broken down
Nyumba iliyofaa	=	The house which was suitable
Nyumba itakayouzwa	=	The house which will be sold

Plural: N Class

Nyumba zinazobomoka	=	The houses which are broken down
Nyumba zilizofaa	=	The houses which were suitable
Nyumba zitakazouzwa	=	The houses which will be sold

Singular: Ma Class

Shamba linaloharibika	=	The field which is ruined
Shamba lililofaa	=	The field which was suitable
Shamba litakalotosha	=	The field which will be big enough

Plural: Ma Class

Mashamba yanayoharibika	=	The fields which are ruined
Mashamba yaliyofaa	=	The fields which were suitable
Mashamba yatakayotosha	=	The fields which will be big enough

2. The use of the relative as an infix is limited to the three primary tenses: Present (NA), Past (LI) and Future (TA>TAKA). With other tenses, and also negative tenses, the relative is expressed in a different way. This we shall learn in the next few lessons.

3. Remember that the object prefix can be used in a verb construction containing a relative in the normal way.

e.g. Ni yeye aliyenipiga = It is he who hit me

II. CULTURAL NOTE

Various organizations,unions, political parties, etc. are organized with a Chairman or President, Vice-President, Secretary, sometimes an Under-Secretary, and a Treasurer. Thus a pretty universal pattern is followed in the organizational set-up. These organizational patterns have been accepted as a contribution from other progressive nations.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 72

1. Language Structure

   a. The Relative Pronoun with AMBA.

      Refer to the Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. Content Structure

   a. Situational Setting: A Tropical Storm

   b. Cultural Note: Reactions to tropical storms

   c. Lexical Items:

baridi kali	(frosty, fierce cold)
dhoruba	(storm)
furika	(flow over, flood)
hali ya hewa	(weather)
imara	(strong)
jua kali	(hot and sunny)
jua kali leo	(a hot sunny day today)
kuna shwari leo	(it's calm today)
kuna upepo leo	(it's windy today)
maiti	(corpse, dead body-human)
marasharasha	(slight drizzle)
mawimbi	(waves)
mawingu	(clouds)
mvua ya mawe	(hail)
mvuke (mi)	(steam, also the hot sun after a rain)
mzoga (mi)	(cadaver, dead animal)
ngurumo	(thunder)
ota (ku) jua	(to bask in the sun)
radi	(bolt of lightning)
shukrani	(thanks, gratitude)
ukungu	(fog)
umeme	(lightning)
vumbi	(dust)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILL | LESSON 72

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 72

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills with 'Amba':

a. Mgeni ambaye alirudi.
Mtoto ambaye alizama.
Mvulana ambaye anajenga.
Msichana ambaye anastahili.

b. Watu ambao huogopa.
Vijana ambao husaidia.
Wavulana ambao hucheza.
Wasichana ambao hushona.

c. Shamba ambalo limeharibika.
Daraja ambalo lilibomoka.
Jina ambalo linapendeza.
Boma ambalo lilianguka.

d. Mashamba ambayo yameharibiwa.
Mavumbi ambayo yamelala.
Majina ambayo yanapendeza.
Maua ambayo yananukia.

e. Kitu ambacho kinapendeza.
Chakula ambacho kinafaa.
Chombo ambacho kimepotea.
Choo ambacho kinanuka.

f. Vitu ambavyo vinafaa.
Viatu ambavyo vitaletwa.
Vyombo ambavyo vimepotea.
Vyakula ambavyo vimeletwa.

g. Nyumba ambayo imebomoka.
Mvua ambayo ilinyesha.
Maiti ambayo haikutambulika.
Radi ambayo ilitisha.

h. Nyumba ambazo zilibomoka.
Barua ambazo zilifika.
Bunduki ambazo zilipotea.
Motokaa ambazo ziliharibika.

Note: The above drills should be presented also in the negative form.

2. Semantic drills:

a. Kufurika
Mto ulifurika
Mito ilifurika

b. Ngurumo
Ngurumo ya radi
Alisikia ngurumo ya radi

c. Umeme
Umeme ulimulika
Umeme ulinitisha

d. Hali ya hewa
Kuna hali gani ya hewa leo?
Kesho hali ya hewa itakuwaje?

e. Kuna upepo leo
Kuna shwari leo
Kuna mawingu leo

f. Kutakuwa baridi kali
Kutakuwa ukungu
Kutakuwa marasharasha

1. Mwangi, mvua nyingi ilinyesha usiku!
   Kweli, Kamau, mito ambayo ilifurika iliharibu mashamba.

2. Mashamba yote ambayo yako mabondeni yameharibiwa?
   Ndio, kuna uchafu na takataka ambayo inanuka popote.

3. Daraja lile la mbao lilibomoka vilevile?
   Limebomoka, lakini vijana wa skuli wanajenga kivuko.

4. Wavulana na wasichana hawa wanastahili shukrani yetu.
   Kweli! Je, ulisikia ngurumo ya radi usiku?

5. Ndio, radi imebomoa majengo ambayo hayakuwa imara.
   Umeme ambao ulimulika ulitisha watu wengi.

6. Watu ambao huogopa umeme walitetemeka sana.
   Kuna jirani ambaye alikufa wakati huo?

7. Wamepata maiti mbili majini ambazo hazitambulikani.
   Sasa jua linang'aa, hakuna mawingu wala mvua.

8. Mavumbi yamelala, na mvuke unaonekana.
   Hata moshi huko na huko huonyesha watu wamewasha mioto.

LESSON 72



2ND PERIOD | ENGLISH DIALOGUE | LESSON 72

KIPINDI CHA PILI | SOMO LA 72

1. Mwangi, it rained a lot last night.

   True, Kamau, the rivers which overflowed damaged the gardens (fields).

2. Were all the fields in the valleys damaged?

   Yes, there is much filth and rubbish everywhere which stinks.

3. Did that wooden bridge break down too?

   It's broken down, but school youths are building a ford (crossing).

4. These boys and girls deserve our gratitude.

   To be sure! Say, did you hear the thunder claps during the night?

5. Yes, lightning destroyed some buildings which were not firm.

   The lightning flashes scared many people.

6. The people who fear lightning were badly shaken.

   Is there a neighbor who died at that time?

7. They found two corpses in the water which are not recognizable.

   Now the sun is shining, there are no clouds nor rain.

8. The dust has settled, and the mist is appearing.

   Even smoke here and there shows that people have lit fires.

Step 1
Hatua ya 1

1. Repetition Drill

a. Alichungua daraja ambalo halikubomoka.
Alichungua daraja ambalo halikubomoka.

nyumba (pl), mtumbwi, kibanda

b. Tunatazama mashamba ambayo yaliharibiwa.
Tunatazama mashamba ambayo yaliharibiwa.

majengo, madaraja, chakula

c. Jirani ambaye aliondoka amerudi.
Jirani ambaye aliondoka amerudi.

wasichana, wavulana, mpishi, swala.

d. Maiti ambazo hazitambulikani zimeletwa.
Maiti ambazo hazitambulikani zimeletwa.

wadudu, mnyama, nyoka (pl), ndege

e. Kinywaji ambacho ulinipa si kizuri.
Kinywaji ambacho ulinipa si kizuri.

vinywaji, samaki (pl), punda, mzigo

f. Wamemwona mvuvi ambaye alianguka.
Wamemwona mvuvi ambaye alianguka.

wavulana, miamba, meli

2. Substitution Drill

Mwamba
a. ------ ambao ulivunjika ni mkubwa.
Mwamba ambao ulivunjika ni mkubwa.

nyumba, madaraja, mtumbwi, mitego.

mashamba
b. Waliona -------- ambayo yaliharibiwa.
Waliona mashamba ambayo yaliharibiwa.

mgahawa, ..ijiji, hoteli (pl), matunda

Abiria
c. ------ ambaye aliumia amerudi.
Abiria ambaye aliumia amerudi.

simba (pl), wasichana, punda, wanachama.

Maiti
d. ----- ambayo ilijulikana imezama.
Maiti ambayo ilijulikana imezama.

meli, kifungu, vifaa, mashua

mvuvi
e. Tunamwona ----- ambaye alianguka.
Tunamwona mvuvi ambaye alianguka.

ng'ombe (pl), Jemedari, vijana, kitano

Step 2
Hatua ya 2 Language clab session (if applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the clab use will be made of the dialogue and pattern drill.

Step 3
Hatua ya 3 Homework assignment

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 72

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 72

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the dialogue

PATTERN DRILL II

Step 2
Hatua ya 2 Patterned response drill.

a. 1st: Ulisikia radi ambayo ilinguruma?
2nd: Ndio, niliisikia.

simba, wanyama, mizinga.

b. 1st: Kuna jirani ambaye aliumia?
2nd: Jirani ambao waliumia ni wengi.

msichana, wanyama, mzazi, wapishi

c. 1st: Daraja ambalo limeanguka ni kubwa?
2nd: Ndio, daraja ambalo limeanguka ni kubwa sana.

majengo, mzigo, paketi, sanduku

d. 1st: Maiti ambazo zilionekana ni hizi?
2nd: Ndio, ni hizi.

mitumbwi, wavuvi, mvulana, wevi.

e. 1st: Kinywaji ambacho ulinipa ni kizuri?
2nd: La, si kinywaji kizuri.

jembe, kiatu, mashamba, mitumbwi.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 72

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 72

Note: If facilities are available, this period can be scheduled for a language clab session.

a. Wamepata vikombe ambavyo wanavitaka?
La, hawajavipata.

mitego, kikombe, vinywaji, samaki

b. Ulinunua mizigo ambayo imeoza?
La, mizigo hiyo haijaoza.

tunda, vyakula, ndizi, maembe

c. Mahali ambapo ulipanunua ni pazuri?
Mahali hapo ni pazuri kweli.

kiatu, vitu, mkeka, matunda

d. Wamtafuta mwivi ambaye haonekani?
Ndio, namtafuta huyo.

kijiko, nyumba, wanyama, vitu

e. Aliona kipande ambacho alikitaka?
La, hakukiona hicho.

mahali, mbwa, wadudu, ng'ombe

f. Mwataka redio ambayo imevunjika?
La, hatuitaki hiyo.

mkuki, viko, majembe, kidude

g. Wapenda kinywaji ambacho nilikupa?
Ndio, nakipenda sana.

vinywaji, shamba, meli, mkuki

Step 1
Hatua ya 1 Presentation of the narrative

Bwana Kamau anaishi Nairobi. Yu tajiri sana. Ana nyumba yake kubwa na huvaa suti malidadi. Anafanya kazi ya mtangazaji wa redio, na kila asubuhi saa moja hutangaza hali ya hewa.

Leo kabla ya kuondoka kwenda kazini alitazama nje, aliona ya kuwa kuna shwari leo. Alimwambia mkewe, "Kutakuwa jua kali leo alasiri. Lakini nakumbuka sivyo pepote. Mahali nilipojifunza, kwa kawaida kulikuwa ukungu na marasharasha. Hatukuweza kuota jua hata kidogo."

Sasa na tufuatane na Bwana Kamau kazini kusikiliza idhaa yake ya redio. Anaanza kusema:

"Leo ni Jumatano, tarehe 12 mwezi wa Mei. Karibieni wasikilizaji nyote na nitawapasha habari.

Kwanza kuna habari ya msiba mkubwa uliotokea jana karibu na kijiji kidogo, jina lake Kabete. Tunajua ya kuwa ni majira ya masika, na kwa muda wa siku nyingi mvua imekuwa ikinyesha sana hata mito imejaa maji na kufurika. Jana maji yalifunika mashamba mengi bondeni na kuleta takataka. Hata daraja dogo la mbao lilibomoka na kuchukuliwa na maji. Watoto wa skuli, wavulana na wasichana, hawakuweza kufika skulini. Hivi vijana na wanafunzi wengine walitumia akili na walitengeneza kivuko

cha kufaa kwa muda. Hivyo wenzao walipita salama, kuendelea na masomo yao. Kweli wanafunzi hao, wenye akili, wanastahili shukrani kwa matendo yao ya kusaidiana.

Shida nyingine ilitukia sababu ya ngurumo kubwa ya radi. Nyumba nyingine zilibomoka. Watu wengine waliogopa sana umeme uliomulika, walitetemeka. Watu wawili walichukuliwa na maji, na walizama. Maiti zao zilionekana chini ya daraja. Wanyama wengine walikufa mjini vilevile na wenyeji walisikitika kuona mizoga ya ng'ombe na ya mbuzi. Dhoruba imeleta hasara sana kwa watu wengi.

Ingawa sisi hapa Nairobi tulipata mvua jana, haikunyesha sana kama mahali pengine. Leo hali ya hewa ni nzuri, kuna jua kali bila mawingu. Furahini leo, kwa sababu kesho kutakuwa na mvua tena.

Sasa kwa herini, wasikilizaji, mpaka saa tatu."

Step 2
Hatua ya 2 The students will write a short summary in English of what they understood of the narrative.

Step 3
Hatua ya 3 Presentation of short narratives prepared by the students.

I. LANGUAGE STRUCTURE

1. The Relative Pronoun with AMBA

In the previous lesson we learned to use the relative pronoun as an infix of a verb construction in the three primary tenses. There is an alternative way of expressing the relative pronoun, and that is by the use of AMBA to which the relative particle has been attached.

Thus:- Atakayekwenda. He who will go.

or

Ambaye atakwenda He who will go.

Amba + is used as a separate word, and the big advantage of this form is that it can be used with other tenses, including the negative.

e.g.	Ambaye amemaliza.	He who has finished
	Ambao wangalipenda	Who would have liked
	Ambavyo havikufika	Which did not arrive
	Ambaye haandiki	Who doesn't write
	Ambacho hakitafaa	Which will be of no use.

2. Notice that when the relative pronoun refers to the object, the corresponding object prefix is generally inserted also.

e.g. Kitabu anachokisoma = The book which he is
Kitabu ambacho anakisoma reading.

Kazi ambayo hukuifanya jana. = The work which you did not do yesterday.

Wamepata vikombe ambavyo wanavitaka = They have received the cups which they want.

II. CULTURAL NOTE

A thunderstorm accompanied by lightning and a heavy tropical downpour can be a frightening and a damaging experience. A flash flood can do considerable damage, flood the fields, wash away bridges, etc. When lightning strikes a tree or building, it can demolish it. The above experience is not uncommon in Africa.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 73

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The KA tense

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from a folk tale: "Three Men and a Lion".

b. Cultural Note: Teaching through stories.

c. Lexical Items:

baradhuli	(simpleton, dupe)
bure	(for nothing)
hai	(alive)
uhai	(life)
hatuna budi	(we must - we have no alternative)
hekima	(wisdom)
jamani	(as an address:- you folks)
mfalme	(king)
mfupa (mi)	(bone)
miongoni mwa	(among, in the midst of)
mjinga	(ignorant, simpleton)
ngozi	(skin)
sultani (ma)	(sultan)
tulia	(relax, be calm, be quiet)
uganga	(medical skill, including use of magical charms)
uhodari	(bravery, skill)
utoto	(childhood)
uzima	(life, well being)
yatupasa	(it is proper for us)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 73

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 73

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances.

1. Drills on the KA tense:

a. Nikasoma
Ukatazama
Akafuata

b. Tukarudi
Mkacheza
Wakapeleka

c. Alikwenda sokoni, akanunua ndizi
Nilirudi nyumbani, nikapumzika.

d. Tulimwona, tukamfuata.
Walifanya kazi, wakapata pesa.

e. Nenda ukasafishe nyumba.
Nendeni mkasafishe nyumba.

f. Tulitafuta kazi, tusipate.
Aliomba msaada, asipate.

2. Drills using new expressions:

a. Ana hekima.
Wana hekima.
Hawakuwa na hekima.

b. Baradhuli
Walikuwa mabaradhuli.
Kidogo walikuwa mabaradhuli.

c. Yatupasa.
Yatupasa kwenda.
Yatupasa kungoja.

d. Tulia.
Alitulia.
Alitulia kimya.

e. Miongoni.
Miongoni mwa watu.
Miongoni mwa wale waliokuwa na maarifa.

f. Hatuna budi.
Hatuna budi kufuatana naye.
Hatuna budi kumpa sehemu ndogo.

g. Kuwa hai.
Kuwa hai kama kwanza.
Kama alipokuwa hai.

h. Zaidi ya hayo.
Zaidi ya hayo, walikuwa wenye maarifa.
Zaidi ya hayo, walikuwa wenye maarifa ya namna mbalimbali.

2ND PERIOD

SWAHILI NARRATIVE

LESSON 73

KIPINDI CHA PILI

SOMO LA 73

MARAFIKI WATATU NA SIMBA

I

Hapo kale palikuwa na watu watatu waliokuwa marafiki wakubwa sana. Zaidi ya hayo, walikuwa wamesoma sana na kuwa wenye maarifa ya namna mbalimbali, lakini hawakuwa na hekima. Kidogo walikuwa mabaradhuli. Watu watatu hao walikuwa na rafiki yao mmoja ambaye hakusoma sana, lakini alikuwa na hekima nyingi.

II

Safari moja, mmoja wao akawaambia wenziwe, "Jamani, na tusafiri twende nchi ya mbali. Faida gani kukaa hapa na kupoteza maarifa yetu bure tu? Yatupasa kwenda mbele ya wafalme na masultani, nasi kwa uhodari wetu, tutaweza kufanya mambo makuu ya ajabu na kupata mali nyingi sana."

III

Basi wote wanne wakaondoka wakaenda zao. Yule aliyetoa shauri la kuondoka alisema, "Huyu rafiki yetu wa nne heri abaki nyumbani. Yeye hana maarifa kama sisi, wala hataweza kuchuma mali yo yote."

I

II

III

IV

Mtu wa pili akakubali, akasema, "Kweli, heri uende nyumbani rafiki yetu. Wewe si hodari kama sisi."

V

Lakini mtu wa tatu akasema, "Sisi sote tumekuwa marafiki tokea utoto wetu, nasi tumeshirikiana kila kitu pamoja. Tusimwache peke yake, heri afuatane nasi mpaka mwisho wa safari yetu. Ingawa yeye si hodari, lakini hatuna budi kumpa sehemu ndogo ya mali tutakayochuma."

VI

Basi wale wengine wawili wakakubali shauri hili, kwa hiyo wote wanne wakafuatana pamoja. Njia yao iliongoza porini. Walipokuwa katikati ya pori, wakaona mifupa na ngozi ya simba aliyekufa.

IV

V

VI

VII

Mmoja miongoni mwa wale waliokuwa na maarifa mengi akasema, "Sasa na tuonyeshe uhodari wetu, zaidi katika mambo ya uganga. Na tumfanye simba huyu kuwa hai tena kama kwanza. Mimi nitaiweka mifupa yake yote mahali pake kama alipokuwa hai."

VIII

Mtu wa pili akasema, "Mimi nitamtia nyama, damu na ngozi nzuri."

Mtu wa tatu akasema, "Vizuri sana. Kama mtafanya hivyo, basi mimi nitamrudishia uzima wake."

IX

Mtu wa nne, ambaye hakuwa na maarifa mengi, lakini alikuwa na hekima, akawaambia, "Ngojeni kwanza! Kama mtamfanya simba huyu kuwa hai kama kwanza, bila shaka atatuua." Lakini wale wengine wakamwambia, "wewe ni mjinga, hatuwezi kuyashika maneno yako. Lazima tutumie maarifa yetu."

Yule mtu akawajibu, "Vema, lakini kabla hamjaanza kazi yenu, tafadhalini ningojeni nipande juu ya mti kwanza."

Basi akapanda juu ya mwembe uliokuwa karibu pale.

VII

VIII

IX

X

Mtu wa kwanza akaiweka mifupa yote mahali pake. Mtu wa pili akaitia nyama na ngozi nzuri. Mtu wa tatu akamtia uhai.

XI

Pale pale yule simba akawa mzima, tena mkali sana. Akasimama na kuwaua wale watatu mara moja. Ukawa ndio mwisho wa maarifa yao.

XII

Yule mwenzao aliyekuwa na hekima alitulia kimya juu ya ule mwembe mpaka simba alipokwisha ondoka na kwenda zake moja kwa moja. Kisha akashuka na kurudi kwao.

X

XI

XII

Step 1
Hatua ya 1 Drills on the use of 'KA' tense.

1. Repetition Drill

a. Alikwenda akalala nyumbani.

ingia, ngoja, kaa

b. Nendeni mkachome majani.

leta, chukua, peleka

c. Kamwambie atusaidie.

omba, shawishi

d. Mama amerudi ili akakaange nyama.

nunua, leta, choma.

e. Tazama, Usije ukawapiga watoto.

adhibu, umiza, dhuru

f. Alimtafuta akamkosa.

pata, ona, kamata

2. Substitution Drill

a. akawaamuru
Alikwenda ---------- wasilale.
Alikwenda akawaamuru wasilale.

ambia, omba, shauri

b. wakaukata
Walichukua kisu --------- mti.
Walichukua kisu wakaukata mti.

angusha, katakata

c. mkawasalimie
Nendeni ---------- wenzenu.
Nendeni mkawasalimie wenzenu.

tembelea, saidia, fundisha

d. Kamwamrishe
---------- aondoke.
Kamwamrishe aondoke.

lazimisha, omba

e. akachelewa.
Mwambie asije ----------.
Mwambie asije akachelewa.

ngoja, linda zamu, vunja sheria

f. asifaulu
Alijaribu sana --------.
Alijaribu sana asifaulu.

shinda, pita mtihani

Step 2
Hatua ya 2 Language clab session (if applicable)

This will be a 10 to 15 minute session in the clab after the drills. In the clab use will be made of the story and pattern drill.

3RD PERIOD	PATTERN DRILL I	LESSON 73
KIPINDI CHA 3	MAZOEZI	SOMO LA 73

Step 3
Hatua ya 3 **Homework assignment**

Read and learn the story in order to be able to retell it.

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 73

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 73

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the Story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILL | LESSON 73

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 73

Note: If facilities are available, part of this period can be scheduled for a language clab session.

a. Alikuita akakuambia nini?
Aliniita akaniambia nisiende.

amrisha, lazimisha, omba

b. Walipokukamata ulifanyaje?
Niliwasihi wakaniachilia.

hurumia, samehe

c. Mbona walimfunga mtu yule?
Walimfunga asije akawapiga.

chokoza, shambulia, teka

d. Ulimtafuta kwa muda mrefu?
Ndio, nilimtafuta nisimwone.

pata, kuta

e. Ulimwambiaje mtoto?
Nilimwambia akamtazame ndugu yake.

salimia, ona, fundisha

f. Aliwashika akawapiga?
Ndio, aliwashika akawapiga.

funga, onya, chokoza

g. Mama atakutuma wapi?
Atanituma nikapeleke shoka.

leta, nunua, tafuta

h. Kijana aliyechaguliwa yuko wapi?
Yuko hapa.

kiti, mananasi, vikombe

i. Unaogopa nini?
Ninaogopa nisije nikaanguka.

chelewa, umia, adhibiwa

j. Waliondoka wakaenda zao?
Ndio, walienda zao.

safiri, tulia, choma mali

k. Hatuna budi kufuatana naye?
Ndio yatupasa kufuatana naye.

saidiana, shirikiana, tumia maarifa

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 73

SOMO LA 73

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

I. LANGUAGE STRUCTURE

The KA tense

1. This tense is often called a narrative tense as it occurs in story telling and narrations. It is a past tense, substituting for the LI tense and the conjunction 'na'. Compare the following two sentences:

   a. Alikwenda mjini na alimkuta rafiki yake, na alimwambia habari zote na rafiki alifurahi.

   b. Alikwenda mjini, akamkuta rafiki yake, akamwambia habari zote, rafiki akafurahi.

   The above two sentences mean the same thing, namely: "He went into town and met his friend, and then he told him all the news, and then the friend was glad." You will notice that in the second one the repetition "and then" is eliminated, and with the help of the KA tense we get a much smoother and more idiomatic expression. Watch for the use of the KA tense in all your reading from now on.

2. There is another use of this tense, and that is with the subjunctive form to express the idea of "go and." e.g.

   Tuliwaambia wakanunue chakula mjini.
   (We told them to go and buy food in town)

   Often the verb "go" is understood, as we also noted in the above sentence. In ordinary speech there are shortened forms as well. Note the following:-
   e.g.

   Nenda ukampe chakula.
   (Go and give him food.)

   This can be shortened by omitting 'nenda' as being understood:
   e.g.

   Ukampe chakula. or Kampe chakula.

There is no exact equivalent of the KA tense in the negative, but the negative subjunctive can be used to express the idea:-
e.g.

Alikwenda kutafuta kazi asipate.
(He went to look for work and didn't find any.)

II. CULTURAL NOTE

Fables and folk tales, especially involving animals, are used to teach many truths, and sometimes to express the Africans' philosophy. It therefore pays to take a closer look at such stories. The animals and other creatures are personalized, and sometimes by their characteristics portray certain types or personalities. For instance, the hare or rabbit is always the clever one who outwits the others, the hyena is the cowardly one, and so on.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 74

VOLUME VI

KITABU CHA VI

BLUE PRINT

LESSON 74

SOMO LA 74

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The Relative Pronoun with negative tenses.

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from a folk tale: "Rats to Rats."

b. Cultural note: None

c. Lexical Items:

afadhali	(rather, preferably)
dini	(religion, creed)
funika	(to cover)
fukua	(to dig out)
kaa raha mstarehe	(to live in perfect comfort and peace.)
kupita kiasi	(beyond measure)
mgongo (mi)	(back, backbone of man or animal)
mtawa	(hermit, recluse)
mwewe	(hawk)
papasa	(stroke, rub lightly)
ponyoka	(to slip)
sali	(pray)
ujumbe	(message)
unyevunyevu	(dampness)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 74

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 74

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances.

1. Drills using the Relative Pronoun with Negative tenses:-

a. Ambaye hapendi
Ambao hawapendi

b. Ambaye hakufika
Ambao hawakufika

c. Ambaye hatasoma
Ambao hawatasoma

d. Ambaye hajaleta
Ambao hawajaleta

e. Ambaye asingesoma
Ambao wasingesoma

f. Ambacho hakifai
Ambavyo havifai

2. Drills using new expressions:-

a. Aliponyokwa
Aliponyokwa na panya
Mwewe aliponyokwa na panya.

b. Kupita kiasi
Joto kali kupita kiasi
Jua lina joto kupita kiasi

c. Unyevunyevu
Wingu lina unyevunyevu
Wingu jeusi lina unyevunyevu.

d. Kuliko
Mkuu kuliko yeye
Mkuu zaidi kuliko yeye

e. Mstarehe
Raha mstarehe
Wakakaa raha mstarehe

f. Usemayo
Hayo usemayo
Hayo usemayo ni sheria

g. Wakati mwingi
Aliyetumia wakati mwingi
Aliyetumia wakati mwingi katika kusali

h. Mtawa
Mtawa alisoma vitabu vya dini
Mtawa alimwabudu Mungu

i. Kufukua
Panya huweza kufukua
Mlima akamjibu, "Panya huweza kunifukua."
"Panya huweza kunifukua na kuchimba shimo ndani yangu."

2ND PERIOD | SWAHILI NARRATIVE | LESSON 74

KIPINDI CHA PILI | SOMO LA 74

PANYA KWA PANYA

I

Karibu na mto mmoja palikuwa na mtawa mmoja aliyetumia wakati wake mwingi katika kusali, kusoma vitabu vya dini na kumwabudu Mungu mchana na usiku. Kila siku alikuwa akioga katika mto ule.

Siku moja, mara baada ya kumaliza kuoga, mwewe mmoja aliponyokwa na mtoto wa panya, naye akaangukia juu ya mgongo wa yule mtawa. Lakini yeye akamchukua na kumpapasa polepole.

II

Kisha baada ya kufanya uganga wake, akamgeuza yule panya kuwa mtoto mwanamke. Akamchukua mpaka nyumbani kwake, akampa mkewe. Mkewe alifurahi mno kwa sababu hawakuwa na mtoto hata mmoja.

III

Basi msichana yule alipokuwa mkubwa, yule mkewe mtawa akasema, "Mume wangu, yafaa sasa huyu binti yetu aolewe. Huna budi kumtafutia mume."

Mumewe akamjibu, "Hayo usemayo ni sheria; nimeyakubali kabisa. Naye amekwisha fundishwa yote yampasayo msichana kuyajua. Aweza kupika chakula, kutunza nyumba, kushona na mengine mengi. Pia anajua kusoma na kuimba na kuhesabu. Sasa wakati wake wa kuolewa umekwisha fika, lakini twataka awe na mume mwema kwa kila neno. Afadhali tumwoze Jua."

I

II

III

IV

Basi yule mtawa akapeleka ujumbe kwa Jua, nalo mara likaja. Likamwambia, "Kwa nini umeniita?"

Yule mtawa akajibu, "Nimekuita kukuuliza kama utapenda kumwoa binti yetu."

Basi Jua likakubali kwa furaha. Kisha yule mtawa akamwita yule kijana mwanamke na kumwuliza kama atapenda kuolewa na Jua.

Yule kijana akajibu, "La, baba sitaki. Yeye ana joto kali mno kupita kiasi. Siwezi kuolewa naye. Tafadhali nichagulie mume aliye mkuu zaidi kuliko Jua."

V

Basi yule mtawa akaliuliza Jua nani aliye mkuu zaidi kuliko yeye. Jua likamjibu, "Wingu ni mkuu kuliko mimi, maana likiufunika uso wangu, hufichwa juu ya uso wa dunia."

Basi Wingu likapelekewa habari. Yule msichana alipoulizwa kama atakubali kuolewa na Wingu, akasema, "La, sitaki. Wingu ni jeusi sana tena lina unyevunyevu. Simpendi mume huyo hata kidogo."

VI

Basi yule mtawa akaliuliza Wingu ni nani aliye mkuu zaidi kuliko yeye. Wingu likamjibu, "Ni Upepo. Yeye ni mkuu zaidi kuliko mimi kwa sababu anapokasirika na kuvuma, hunifukuza na kunitawanyatawanya."

Basi yule mtawa akauita Upepo, akauuliza kama utapenda kumwoa binti yake. Lakini yule kijana mwanamke akakataa katakata kuolewa na Upepo. Akasema, "Sitaki kuolewa na Upepo, maana mtu hawezi kumjua mahali alipo. Nitafutie mume mwingine aliye mkuu zaidi kuliko yeye."

IV

V

VI

VII

Yule mtawa akauuliza Upepo, "Je, yuko mwingine aliye mkuu zaidi kuliko wewe?"

Upepo ukamjibu, "Ndiyo, bwana, Mlima ni mkuu zaidi kuliko mimi kwa sababu ninapovuma kwa nguvu, siwezi kumwa-ngusha."

Yule mtawa akamwuliza yule kijana mwanamke kama atapenda kuolewa na Mlima. Lakini yeye alikataa sana, akamwambia, "Ha-pana, baba; yeye ana moyo wa jiwe!"

VIII

Basi yule mtawa akauuliza Mlima kama yuko mwingine aliye mkuu zaidi. Mlima ukamjibu, "Panya ni mkuu zaidi kuliko mimi kwa sababu huweza kunifukua na kuchimba shimo ndani yangu. Nashindwa kumzuia."

Basi panya akaitwa, na yule kijana alipomwona, aka-mwambia baba yake, "Baba, kama utanigeuza kuwa panya, nita-kubali kuolewa naye, nami nina hakika tutakuwa na furaha nyumbani mwetu."

IX

Basi yule mtawa akamgeuza yule kijana mwanamke kuwa panya, naye akaolewa na yule panya mwingine. Wakakaa raha mstarehe mpaka mwisho wa maisha yao.

VII

VIII

IX

3RD PERIOD | PATTERN DRILL I | LESSON 74

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 74

Step 1
Hatua ya 1

1. Repetition Drill

a. Mtu ambaye hana hekima amerudi.
Mtu ambaye hana hekima amerudi.

watu, wafalme, Sultani.

b. Vitu ambavyo havileti faida vitaondolewa.
Vitu ambavyo havileti faidi vitaondolewa.

kitu, mgahawa, duka

c. Kiumbe ambacho hakitakufa.
Kiumbe ambacho hakitakufa.

watu, mimea, mti

d. Ngozi ambayo haikauki si nzuri.
Ngozi ambayo haikauki si nzuri.

ngozi (pl), koti, viatu

e. Kijana ambaye hatulii atapigwa.
Kijana ambaye hatulii atapigwa.

vijana, mtoto, mbwa

f. Vitu ambavyo havifai vitarudishwa.
Vitu ambavyo havifai vitarudishwa.

tumia, uza, pendeza.

2. Substitution Drill

a. kazi
Wamepewa ---- ambayo haitoshi.
Wamepewa kazi ambayo haitoshi.

chakula, maji, nguo

b. Kitabu
------ ambacho hakikupatikana si changu.
Kitabu ambacho hakikupatikana si changu.

mtoto, vyombo, mzigo.

c. hawatakula
Wale ambao ---------- watakufa.
Wale ambao hawatakula watakufa.

jificha, toroka, pigwa sindano.

d. Mikate
------ ambayo inaanguka itaokotwa.
Mikate ambayo inaanguka itaokotwa.

vikapu, matunda, ua

e. Motokaa
------- ambayo haiendi itatengenezwa.
Motokaa ambayo haiendi itatengenezwa.

gari, magari, eroplani (pl)

f. hawako
Wale ambao ------ hawahesabiwi.
Wale ambao hawako hawahesabiwi.

kuja, fanya kazi, lima

Step 2
Hatua ya 2 Language clab session (if applicable)

After the drills there will be a 20 minute clab session, during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework assignment

Read and learn the story in order to be able to retell it.

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 74

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 74

Step 1
Hatua ya 1 Retelling of the story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | DRILLS | LESSON 74

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 74

Note: If facilities are available, part of this period can be scheduled for a language clab session.

Step 1
Hatua ya 1 Patterned response drill

a. 1st: Wageni ambao walifika wako wapi?
2nd: Wako hapa.

mtu, mizigo, gari

b. 1st: Umeleta vibuyu ambavyo havikusafishwa?
2nd: Ndio, nimevileta.

kisu, nguo, msumeno

c. 1st: Meza ambayo ilivunjika iko wapi?
2nd: Iko hapa.

mkuki, mishale, sahani

d. 1st: Maji ambayo yalimwagika yalitoka wapi?
2nd: Yalitoka pale.

unga, maziwa.

e. 1st: Watu ambao hawatarudi watakaa wapi?
2nd: Watakaa mgahawani.

pumzika, fanya kazi, cheza

Step 2
Hatua ya 2 Recombination drill

a. Watu ambao hawaridhiki watafungwa?
Ndio, watafungwa.

tii, tosheka, lala

b. Vitu ambavyo havikuhesabiwa vimerudishwa?
La, havijarudishwa.

mateka, misumari, pesa

c. Motokaa ambazo zilipinduka ziliharibika?
La, hazikuharibika.

gongana, anguka

d. Kalamu ambayo ilivunjika ni yako?
La, si yangu.

viti, mlango

e. Wanafunzi ambao walifaulu wameondoka?
La, hawajaondoka.

motokaa, vijana, mtoto

f. Mtawa ambaye hasali anafanya nini?
Mtawa ambaye hasali anasoma vitabu.

walimu, mvulana

g. Vitabu ambavyo vinasomwa ni vya dini?
Ndio, ni vya dini.

gazeti, maelezo

h. Yule ni msichana ambaye hataki kutunza nyumba?
Ndiye yeye.

kasirika,kaa, raha, mstarehe

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 74

SOMO LA 74

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

I. LANGUAGE STRUCTURE

In lesson 72 you learned how to use the word AMBA plus the relative pronoun. You learned that AMBA could be used with various tenses in the affirmative, and mention was made of its use with the negative. In this lesson we will concentrate on its use with negative tenses:

Pres.	Ambaye hasomi.	He who doesn't read.
Past.	Ambaye hakusoma.	He who didn't read.
Fut.	Ambaye hatasoma.	He who will not read.
Perf.	Ambaye hajasoma.	He who has not read.

Conditional Tenses:

Ambaye hangeweza or	He who would not be able.
Ambaye asingeweza	He who would not be able.
Ambaye hangaliweza	He who would not have been able.
or	
Ambaye asingaliweza	He who would not have been able.

With nouns of other classes, the same construction is followed:

e.g. Kitu ambacho hakifai - The thing which is not suitable.

Kitu ambacho hakikufaa - The thing which was not suitable.

Kitu ambacho hakitafaa - The thing which will not be suitable.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 75

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The relative pronoun with the Verb "To Be".

b. The relative pronoun with the indefinite time, affirmative and negative.

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from folk tale: "The Goat, the Leopard, and the Frog."

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

-bichi	(unripe, green)
chura (pl. = vyura)	(frog)
epuka	(avoid, separate from)
jiepusha	(keep oneself from)
jilaza	(lay oneself down)
koroma (ku)	(snort)
kuna (ku)	(scratch)
kwa kasi	(speedily, hastily)
kwato	(hoof)
ladha (n.)	(taste)
machukio	(anger, hate)
magoti	(knees)
kwenda kwa maringo	(walk with a swagger)
mbingu	(sky, heaven)
mkia (mi)	(tail)
mradi	(plan, intention)
mshangao (mi)	(alarm, amazement)
mustarehe	(comfortably settled)
ncha	(point, tip)
nyie watu	(you people)
nyufa za macho	(slits of eyes)
piga teke (ku)	(kick)

c. Lexical items continued:

shibisha	(fill up - feed to satisfaction)
shughulika	(be occupied)
tetemeka	(tremble)
tikisa	(shake)
thubutu	(dare)
utosi (pl. = tosi)	(crown of head)
ukingo (pl. = kingo)	(bank, edge - river)
utomvu	(sap, juice)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 75

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 75

Note: Refer to the Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on Relative pronoun with the Verb "To Be".

   a. Aliye mrefu
      Asiye mrefu

   b. Kitu kilicho kizuri
      Kitu kisicho kizuri

   c. Tulio walimu
      Tusio walimu

   d. Nguo zilizo mpya
      Nguo zisizo mpya

   e. Mkulima aliyekuwa hodari
      Mtawa atakayekuwa mwema

2. Drills on Relative particle with indefinite time.

   a. Mtu aletaye
      Watu waletao

   b. Kitu upendacho
      Vitu upendavyo

   c. Tunda lipendezalo
      Matunda yapendezayo

   d. Sahani ivunjikayo
      Sahani zivunjikazo

3. Drills using new expressions.

   a. Majani mabichi
      Majani mabichi na yenye utomvu
      Majani mabichi katika kingo za mto.

   b. Maringo
      Kwenda kwa maringo
      Chui alikuja akienda kwa maringo

c. Alipiga teke kwa miguu
Alipiga teke kwa miguu ya mbele
Alipiga teke kwa miguu ya nyuma

d. Alikuna
Alikuna magoti
Alikuna magoti kwa meno yake

e. Mustarehe
Alikaa mustarehe
Chui alikaa mustarehe katika miguu yake

f. Alikuwa mradi
Alikuwa mradi haondoi macho yake
Alikuwa mradi haondoi macho yake kwa chui

g. Hajui la kufanya
Hajui la kusema
Hakujua la kufanya
Hakujua la kusema

h. Ufa wa jicho
Nyufa za macho
Aliwaangalia katika nyufa za macho

i. Alitetemeka
Alitetemeka kwa woga
Sauti ilitetemeka kwa woga

j. Aliepuka hatari
Chura alijiepusha
Alijiepusha taratibu
Alijiepusha taratibu kama alivyoweza.

I

Siku moja Bwana Mbuzi alikuwa akila majani katika kingo za mto ambamo majani yalikuwa mabichi, mazito na yenye utomvu. Alifurahi sana.

Bwana Chui alikuja akienda kwa maringo sana, akamwita: "Bwana Mbuzi, unafanya nini huko?" Bwana Mbuzi alitazama kwa mshangao: "Kwa nini? Ninakula majani mazuri yenye utomvu. Yapendeza. Njoo ule kidogo."

Bwana Chui alikoroma kwa machukio: "Kula mwenyewe, Bwana Mbuzi, kula majani, ukiisha kushibisha tumbo lako vema, nitakula wewe, utakuwa na ladha nzuri kama ile uionayo katika majani."

II

Bwana Mbuzi hakujua la kufanya. Alitazama mbinguni, chini duniani, na kila pembe apate kuona kama kuna msaada wowote wa kupatikana, asione kitu. Alitikisa mkia wake mdogo, akajaribu kutafuna majani, lakini alitetemeka sana hata hakuweza kuyauma. Alipiga teke kwa miguu yake ya mbele, lakini hakuna msaada uliokuja; alipiga teke kwa miguu yake ya nyuma, lakini pia hakuna msaada ujao. Alikuna magoti yake kwa meno yake, naye aliweza kusikia maji yakinguruma ndani ya tumbo lake.

III

Bwana Chui alikaa mustarehe katika miguu yake, wala hakumwondolea macho yake Bwana Mbuzi kabisa. Bwana Mbuzi alitaka kujilaza chini, lakini hathubutu, alitamani kugeuka, lakini hathubutu. Alikuwa mradi haondoi macho yake kwa Bwana Chui.

Fikira za Bwana Mbuzi zilikimbizana kwa upesi toka kwenye kwato zake mpaka utosi wa kichwa chake, kujaribu kutunga ni sehemu yake ipi Bwana Chui ataanzia, na namna atakavyomla.

I

II

III



IV

Bwana Chui akasema: "Utamaliza lini kula majani yako, ili niweze kukula?"

Kabla Bwana Mbuzi hajaweza kumjibu mzee mmoja wa chura mwema alitokea mtoni akaruka juu ya ukingo. Aliuliza: "Nyie watu mnasema nini hapa?" Bwana Chui akasema: "Ndiyo, nilikuja nikamkuta Bwana Mbuzi anakula majani, nikamwambia kuwa aishapo kula majani yake nami nitamla."

V

Bwana Chura akasema: "Ndiyo hasa, ndiyo, mle, na ukiisha kumla, nitakula wewe. Hii ni haki kabisa, ama sivyo, Bwana Mbuzi?"

Sauti ya Bwana Mbuzi ilitetemeka kwa woga, akasema: "Ndiyo, bwana, ndiyo Bwana Chura; itakuwa haki kabisa." Bwana Chui alitazama kila upande naye hakuweza kufikiri la kusema. Alitazama kila upande, akiwaangalia Bwana Mbuzi na Bwana Chura katika nyufa za macho yake.

VI

Bwana Chura na Bwana Mbuzi walizidi kuendelea kuzungumza kwa furaha. Bwana Chui alipoona kuwa wameshughulika sana wala hawawezi kumwangalia, alijiepusha taratibu kama alivyoweza, na akakimbia kwa kasi sana.

Mara Bwana Chura na Bwana Mbuzi waligeuka wakasema: "Yuko wapi Bwana Chui? Sikumwona akienda." Walimtafuta mahali pote, lakini hawakumwona hata ncha ya mkia wake. Walimwita, lakini hakuitika.

Basi hivyo ndivyo Bwana Chura alivyookoa maisha ya Bwana Mbuzi akamzuia Bwana Chui asimwue. Hivyo ndivyo marafiki wawezavyo kusaidiana kama vile na Bwana Chura alivyomsaidia Bwana Mbuzi.

IV



V

VI

3RD PERIOD | PATTERN DRILL I | LESSON 75

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 75

Step 1
Hatua ya 1

1. Repetition and Substitution drills

a. Simama karibu na mti ulio mrefu.

miti, mtu, mwanafunzi, daraja

b. Karani aliye Mkikuyu aliandika kitabu.

Bwana, mimi, waziri, wewe

c. Nilinunua vitabu vilivyo ghali.

kiti, nyumba, kitabu, milango, matunda

d. Mtu asiye tajiri hawezi kununua nyumba.

watu, mimi, mkulima, wewe, ninyi

e. Macho yaliyo mazuri yanaweza kuona mbali.

vitu, vyote, maandiko

f. Mtumishi atorokaye hawezi kupata kazi tena.

mwalimu, watu, mvuvi, wenyeji, waashi

Step 2
Hatua ya 2

1. Homework: Preparation of the story for retelling.

4TH PERIOD (First Hour in the morning) LESSON 75

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 75

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the Story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 75

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 75

Step 1
Hatua ya 1

1. Repetition of phrases from the stories, showing use of the Relative Pronoun.

   a. Utakuwa na bahati nzuri kama ile uionayo sasa.

   b. Hakuna msaada ujao.

   c. Aishapo kula majani yake nitamla.

   d. Hivyo ndivyo marafiki wawezavyo kusaidiana.

   e. Hapo kale palikuwa na watu watatu waliokuwa marafiki.

   f. Wakaona mifupa na ngozi ya simba aliyekufa.

   g. Akapanda juu ya mwembe uliokuwa karibu pale.

   h. Nichagulie mume aliye mkuu kuliko Jua.

   i. Mtu hawezi kujua mahali alipo.

   j. Usimdhuru mbwa aliye rafiki ya watu.

   k. Hatuna budi kumpa sehemu ndogo ya mali tutakayochuma.

   l. Mmoja miongoni mwa wale waliokuwa na maarifa mengi akasema, "Tuonyeshe uhodari wetu."

   m. Hayo usemayo ni sheria.

   n. Amekwisha fundishwa yote yampasayo msichana kuyajua.

Step 2
Hatua ya 2

The above phrases may be given at random in English, to check the student's ability and and speed in giving the Swahili equivalent.

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 75

SOMO LA 75

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

I. LANGUAGE STRUCTURE

1. Verb "To Be" - KUWA with the relative pronouns.

a. Note that in the present tense there are irregularities. An old form "LI" (which is not to be confused with the past tense sign "LI") is used only in conjunction with the relative pronouns. Thus we get:

(mimi)	niliye	=	I who am
(wewe)	uliye	=	You who are
(yeye)	aliye	=	He who is
(sisi)	tulio	=	We who are
(ninyi)	mlio	=	You who are (pl.)
(wao)	walio	=	They who are

b. In the other noun classes the same pattern is followed.

Mti ulio mrefu.	=	The tree which is tall.
Miti iliyo mirefu.		The trees which are tall.
Kitu kilicho kizuri	=	The thing which is good.
Vitu vilivyo vizuri	=	The things which are good.
Nyumba iliyo mpya.	=	The house which is new.
Nyumba zilizo mpya.	=	The houses which are new.
Tunda lililo tamu.	=	The fruit which is sweet.
Matunda yaliyo matamu	=	The fruits which are sweet.
Mahali palipo pazuri.	=	The place which is nice.

c. The negative form of the above is achieved simply by substituting "si" for "li". Thus:-

Affirm:	Niliye tajiri	=	I who am rich.
Neg:	Nisiye tajiri	=	I who am not rich.
Affirm:	Kitu kilicho rahisi	=	The thing which is easy
Neg:	Kitu kisicho rahisi	=	The thing which is not easy.

d. Note that this form of the Verb "To Be" is used in the concept of denoting existence, state or condition, and not in the sense of an auxiliary verb.

e.g. Let's look at the following two sentences in English.

1. The man who <u>is</u> good. (main verb)

2. The man who <u>is</u> eating. (auxiliary)

In Swahili these two sentences would be rendered differently. Study the differences carefully.

1. Mtu aliye mwema.
   Verb "To Be" with the relative expressing the state or condition of being good.

2. Mtu anayekula.
   Here the present tense sign NA is used with the relative pronoun. The verb is "to eat."

2. In all other tenses the verb "Kuwa" is used regularly like any other monosyllabic verb.

Affirmative:	e.g.	Past:	Mtu aliyekuwa mwema.
		Fut:	Mtu atakayekuwa mwema.
Negative:		Past:	Mtu ambaye hakuwa mwema.
		Fut:	Mtu ambaye hatakuwa mwema.

3. The relative particle is used <u>as an ending</u> with the <u>irregular</u> form of the verb "To Be" only in the <u>present tense.</u> Similarly, it can be used with other verbs as well. Note that only the subject prefix without a tense sign is used because it does not define time.

e.g. Hayo usemayo - What you say
Fanya upendavyo - Do as you wish
Nitafanya niwezavyo- I'll do as I can

For practical purposes it can be regarded as a short form of the previously learned longer form with the "NA" tense. See the comparative table below:-

	Long Form	Short Form
Mtu Watu	anayepita wanaopita	apitaye wapitao
Mkuki Mikuki	unaopendeza inayopendeza	upendezao ipendezayo
Kisu Visu	kinachokata vinavyokata	kikatacho vikatavyo
Kazi Kazi	inayolipwa zinazolipwa	ilipwayo zilipwazo
Tunda Matunda	linalooza yanayooza	liozalo yaozayo

In the negative the relative particle is not an ending, but is attached to the negative particle "si". This again is done only in the present tense. If in doubt, use "amba" with negative forms.

e.g. Affirmative		Negative
atakaye		asiyetaka
	or	ambaye hataki
kipendezacho		kisichopendeza
	or	ambacho hakipendezi

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 76

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The relative pronoun with the Verb "To Have."

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from a folk tale: "Man and the Leopard".

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

ajali	(accident, also fate, destiny, appointed end)
Alhamdulilahi	(Allah be praised!)
chinja	(butcher, kill)
chui	(leopard)
dhuru	(hurt, harm)
elewa	(comprehend)
fadhili	(kindness, favor)
hasira	(anger)
hasha!	(certainly not!)
hurumia	(have pity or mercy)
kamwe	(never - always used with negative preceding - "Singethubutu kamwe".)
kawaida	(habit, custom)
kisa (vi)	(story)
kivuli	(shade)
kiumbe	(creature)
kokotea	(haul for, drag for)
lia (ku)	(cry)
makaa	(coal)
maulana	(Lord, master)
mpumbavu	(fool, dupe)
mwembe	(mango tree)
naswa	(get caught)
ndipo	(there and then)

nguruma (ku)	(growl, roar)
nung'unika	(grumble, complain)
sihi	(plead, beg)
tatanisha	(complicate, puzzle)
udhia	(trouble, annoyance)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 76

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 76

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills using the Relative Pronoun with the Verb "To Have."

   a. Mtu anaye watoto
      Watu wanao watoto

   b. Mtu aliye na watoto
      Watu walio na watoto

   c. Askari ambaye hana kibuyu
      Wapelelezi ambao hawana kiongozi

   d. Mlinzi atakayekuwa na bunduki
      Vijana watakaokuwa na vitabu

   e. Mwandishi aliyekuwa na kalamu
      Wafalme waliokuwa na nchi

2. Drills using new expressions

   a. Alinaswa
      Alinaswa katika mtego
      Mtego uliokuwa kama sanduku
      Alinaswa katika mtego uliokuwa kama sanduku

   b. Kamwe
      Singethubutu kamwe
      Singeelewa kamwe

c. Akajaribu kumsihi
Akajaribu kumsihi asimdhuru

d. Kumlipa mwenzio mabaya
Kumlipa mwenzio mabaya kwa mema
Kumlipa mwenzio mabaya kwa fadhili

e. Kukokota magari
Kuwakokotea magari

f. Hayo yaliyokupata
Ndiyo hali ya dunia
Hayo yaliyokupata leo ndiyo hali ya dunia

g. Kivuli changu
Wanadamu huja chini ya kivuli changu
Wanadamu huja chini ya kivuli changu kupumzika

I

Safari moja chui mmoja mkubwa tena mkali sana alinaswa katika mtego mkubwa uliokuwa kama sanduku. Akawamo ndani yake akinguruma na kurukaruka huko na huko akitafuta njia ya kutokea nje lakini asifaulu hata kidogo.

II

Kwa bahati akaja mtu mmoja pale pale karibu na ule mtego. Yule chui alipomwona akamwambia yule mtu. "Tafadhali sana nifungulie mlango wa mtego huu, bwana mkubwa!" Yule mtu akajibu akamwambia, "La, la, la rafiki yangu, ukitoka humo humo utanirukia na kunila." Chui akasema, "La, hasha, mimi si mtu wa kufanya mambo kama hayo, wala singethubutu kamwe."

III

Basi yule chui alipokuwa akihangaika na kulia, yule mtu akamhurumia. Mwishoni akakubali kumfungulia mlango wa mtego ule. Mara ile yule chui akatoka kwa nguvu na kumkamata yule mtu, akamwambia, "Kweli, tangu kuzaliwa kwangu sijaona mtu mpumbavu na mjinga kama wewe! Nitazuiwa na nini sasa nisikule? Kwanza leo hivi yapata siku ya tatu sijatia riziki yoyote tumboni mwangu. Njaa imenishika sana."

I

II

III

IV

Yule mtu akajaribu kumsihi asimdhuru, lakini wapi! Hakumsikiliza. Basi mwishoni ch[illegible] akamwambia, "Tuendelee mbele, na kwa viumbe vitatu vya kwanza tutakavyovikuta tutaeleza habari hii. Watakavyosema ndivyo nitakavyotenda, wala sitabadili."

V

Kwanza wakaukuta mwembe, wakaeleza habari yote. Yule mtu akauuliza mwembe, "Ati, Bwana Mwembe, mtu akikutenda mema, ni haki kumlipa mabaya?" Akaeleza tena habari yao, kati yeye na chui. Mwembe ukajibu ukamwambia, "Kweli si haki kumlipa mwenzio mabaya kwa mema, lakini ninyi wanadamu, je, hamfanyi hivyo?"

VI

Tazama, Bwana Chui, mimi huwapa hawa wanadamu maembe yangu wakala, na wakati wa jua kali huja chini ya kivuli changu kupumzika. Lakini juu ya fadhili zote hizi ninazowatenda havitoshi, mwishoni hunikatakata na kunichoma makaa, basi hii ni haki? Hata wewe mwenyewe yapime."

Chui akamwambia yule mtu, "Je, mwanadamu, unasikia huko?" Yule mtu akajibu akamwambia, "Nasikia sana, lakini na tuendelee mbele tu."

IV

V

VI

VII

Mbele zaidi wakakutana na ng'ombe. Mwanadamu akamwambia, "Ati bwana, mtu kama akikutendea fadhili, ni haki kumlipa mabaya?" Ng'ombe akamwuliza, "Kuna nini?" Ndipo yule mtu akamsimulia kisa chote kati ya yeye na chui.

VIII

Ng'ombe akajibu akamwambia, "Ni kweli kabisa si haki kumlipa mwenzio mabaya ikiwa amekutendea fadhili njema, lakini katika viumbe wa kutenda mema, ninyi wanadamu hamko. Tazama, Bwana Chui, mimi huwapa hawa wanadamu maziwa yangu wakanywa, pengine huwakokotea magari na kulima mashamba yao. Lakini hivyo vyote kwao havitoshi, mwishoni hunichinja na kunila nyama." Akamwambia yule mwanadamu, "Usinung'unike, baba, amka! Hayo yaliyokupata leo ndiyo hali ya dunia!"

IX

Walipoendelea mbele zaidi wakamwona mbwa ambaye alikuwa rafiki yake huyu mwanadamu. Akamweleza kisa chote kama alivyomweleza mwembe na ng'ombe.

VII

VIII



IX

X

Mbwa akasema, "Habari hii inanitatanisha sana, wala siwezi kuelewa nayo vyema mpaka sisi wote watatu tuende kwenye huo mtego." Basi wakaenda. Walipofika yule mtu akarudia tena habari ile yote toka mwanzo mpaka mwisho.

Mbwa akasema, "Kwani mambo yenyewe yalianzaje hasa? Yaani wewe ulikuwamo mtegoni, na chui akaja karibu, au sivyo?"

XI

Chui akajibu akasema, "La, la, la, sivyo ilivyokuwa hata kidogo. Wewe mjinga, nini? Mimi ndiye niliyekuwamo mtegoni." Mbwa akasema, "Aaa sasa nimeelewa. Yaani mimi mbwa ndiye niliyekuwamo mtegoni, na wewe chui ukaja karibu na mtego, au sivyo?" Chui akajibu kwa hasira akamwambia, "La, huelewi? Sivyo hivyo hata kidogo. Tazama ilikuwa hivi: Unaona--mimi ni chui." Mbwa akamwambia, "Haya, vyema, endelea." Kamwambia tena, "Mimi, nilikuwamo mtegoni--unaelewa?"

XII

Mbwa akajibu, "Hasa, lakini, uliingiaje katika mtego huu?" Chui akajibu akamwambia, "Kwa nini waniuliza hivyo? Si kama kawaida ya watu waingiavyo katika matundu?" Mbwa akamwuliza tena, "Tafadhali, maulana, usikasirike, kawaida hivyo ni ipi?"

Basi kusikia maneno haya, chui akaruka kwa sauti kubwa, "Namna hii! Je, sasa umekwisha elewa jinsi mambo yenyewe yalivyokwenda?" Mbwa akafunga mlango wa ule mtego upesi sana, akamjibu, "Hasa! Nimekwisha elewa kabisa, nami naona heri uzidi kukaa mumo humo mpaka ikutokee ajali yako." Kisha akamwambia yule mtu, "Haya, twende zetu, Alhamdulilahi, sasa udhia wote umekwisha."

X

XI

XII

Step 1
Hatua ya 1

1. Repetition and substitution drills

a. Mtu aliye na nguvu amefika.

Alternate form:-

Mtu anaye nguvu amefika

Substitute: Watumishi, kiongozi, mkulima, fundi, kikosi

b. Wanafunzi walio na vitabu waingie skulini

Alternate form:-

Wanafunzi wanao vitabu waingie skulini

Substitute: Walimu, ninyi, mtoto, wakaguzi

c. Miti niliyo nayo nitakupa.

Miti niliyokuwa nayo nilikupa.

Miti nitakayokuwa nayo nitakupa.

Substitute: Vitabu, kitu, msumeno, shoka, chandalua, fanusi

d. Mwanafunzi ambaye hana vitabu hawezi kujifunza.

Wanafunzi ambao hawakuwa na vitabu hawakuweza kujifunza.

Wanafunzi ambao hawatakuwa na vitabu hawataweza kujifunza.

Substitute: vijana, msichana, askari, daktari, mekanika, wapishi

3RD PERIOD | PATTERN DRILL I | LESSON 76

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 76

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session, during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework:- Learning of story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 76

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 76

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 76

KIPINDI CHA 5 | SOMO LA 76

Step 1
Hatua ya 1

a. Msumeno alio nao ni wake?
Ndio msumeno alio nao ni wake.

nyumba, punda, matunda

b. Watu ambao hawatakuwa na nyumba, watakaa wapi?
Watakaa hapa pamoja na sisi.

Walimu, mwandishi, mwananchi

c. Mtoto aliye nyumbani ni wako?
Ndio mtoto huyo ni wangu.

vitabu, mfuko, kibuyu

d. Chui alinaswa katika mtego mkubwa?
Ndio, alinaswa katika mtego uliokuwa kama sanduku.

kiumbe, mbuzi, kifaru

e. Ningeweza kutazama vitu ulivyo navyo dukani?
Ndio, karibu ukavitazame vyote.

sahani, suti, matunda

Step 2
Hatua ya 2 Written exercise

The student will write a brief synopsis of the story in his own words.

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 76

SOMO LA 76

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

I. LANGUAGE STRUCTURE

1. Verb "To Have" - KUWA NA with the relative pronoun. Present tense.

   a. Note that in Swahili verb "To Have" (KUWA NA) is not used as an auxiliary to another verb as it is in English.

      e.g. I have eaten = Nimekula
      In Swahili a tense sign is used.

   b. With the relative pronoun in the present tense the verb "To Have" (KUWA NA) follows the same pattern as explained in Lesson 75 under the verb "To Be".

      e.g. Affirm: Mtu aliye na mali
      The person who has property.

      Neg: Mtu ambaye hana mali or asiye na
      The person who has no property.

   c. There is also a shorter alternate form in the present affirmative.

      Mtu anaye mali

      Watu wanao mali

   d. When the object possessed precedes this verb structure, then the relative particle is attached to both parts.

      e.g. Affirm: Kitu alicho nacho
      The thing which he has.

   e. In the negative present with "amba" the relative particle is attached only to "amba".

      e.g. Kitu ambacho hana.
      The thing which he doesn't have.

But without "amba" the present tense negative would be:-

e.g. Kitu asicho nacho = The thing which he doesn't have.
(This is the preferable form)

2. The following are the constructions for the future and past tenses:

a. Future affirmative:

Watu watakaokuwa na vitabu = The people who will have books.

Vitabu watakavyokuwa navyo = The books which they will have.

b. Future negative:

Watu ambao hawatakuwa na vitabu = People who will not have books.

Vitabu ambavyo hawatakuwa navyo = Books which they will not have.

c. Past affirmative:

Watu waliokuwa na vitabu = People who had books.

Vitabu walivyokuwa navyo = Books which they had.

d. Past negative:

Watu ambao hawakuwa na vitabu. = People who did not have books.

Vitabu ambavyo hawakuwa navyo. = The books which they did not have.

It will be noticed from the above that "na" cannot stand alone, but must be followed either by a noun, or by the relative particle.

Use of the relative particle with present tense forms: a summary.

As there are irregularities in the present tense, especially with the verb 'To Be' and 'To Have', and as there are also alternatives, the following diagram may be helpful to the student.

Affirmative	Negative
1. Regular Verb (penda)	
(he who likes)	(he who doesn't like)
apendaye (short) anayependa (long) ambaye anapenda	asiyependa ambaye hapendi
2. Monosyllabic Verb (kula)	
(he who eats)	(he who doesn't eat)
alaye (short) anayekula (long) ambaye anakula	asiyekula ambaye hali
3. Verb 'To Be' (kuwa)	
(he who is)	(he who is not)
awaye (hardly ever used) aliye (based on old form) ambaye ni	asiyekuwa asiye ambaye si
4. Verb 'To Have' (kuwa na)	
(he who has)	(he who has not)
anaye (regular) aliye na (based on old form) ambaye ana	asiyekuwa na asiye na ambaye hana

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 77

1396-1397

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. Nouns of the U class.

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational setting: Series of scenes from a folk tale: "Lutembe".

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

akina	(generalized plural - tribe, family, etc.)
asi (ku)	(to rebel)
baadhi ya	(some of)
badala ya	(in place of, instead of)
binadamu	(human beings)
changarawe	(grit, small stones, fine gravel)
daka	(seize)
hukumiwa	(be judged, sentenced)
jasho	(sweat, perspiration)
jongea	(make a move, either of approaching or going away)
kabila (ma)	(tribe)
kifo	(death)
maarufu	(well known, famous)
mamba	(crocodile)
mzimu (mi)	(spirit of dead person, spirits of ancestors or native place of worship)
pishana	(allow each other to pass)
sadaka	(sacrifice)
shinda	(a. overcome, conquer, b. surpass,excel, win, c. pass time, keep on, stay for a time)

sumbua	(annoy, trouble, vex, torment)
tambaa	(creep, crawl)
tambika	(to make an offering to the spirits)
tambiko (ma)	(offering made to the spirits of the dead)
toswa	(be plunged into water, caused to sink)
ukarimu	(generosity, hospitality)
ukatili	(cruelty, bloodthirstiness)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 77

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 77

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills using "U" class nouns

   a. Usiku huu
      Usiku ule

   b. Ubao mwembamba
      Mbao nyembamba

   c. Ubao mrefu ule
      Mbao ndefu zile

   d. Uso wake
      Nyuso zao

   e. Wembe wangu umepotea
      Nyembe zangu zimepotea

   f. Ukubwa wa Uingereza
      Urefu wa ukuta

   g. Ukatili wa Mfalme
      Ukatili wa waziri

2. Drills using new expressions

a. Baadhi ya
Baadhi ya mateka
Baadhi ya mamba

b. Badala ya
Badala ya watu
Afadhali kumtupia samaki badala ya watu.

c. Kudaka
Wadakwe na mamba
Wakasukumwa majini wadakwe na mamba

d. Walioasi
Walioasi wakahukumiwa.
Walioasi wakahukumiwa kifo.

e. Makabila mengine
Kama watu wa makabila mengine

f. Kama walivyotambika
Kama walivyotambika kwenye mizimu

g. Kutendewa ukarimu
Akitendewa ukarimu hugeuka kuwa rafiki.
Mnyama ye yote akitendewa ukarimu hugeuka kuwa rafiki.

2ND PERIOD | SWAHILI NARRATIVE | LESSON 77

KIPINDI CHA PILI | "Lutembe" | SOMO LA 77

Mamba aliye rafiki ya watu
Katika nchi ya Uganda

I

Hapo zamani, kabla Wazungu hawajafika katika nchi ya Uganda, mfalme wa nchi alifuata desturi hii: Baada ya kupigana na maadui zake aliwaleta mateka, akachagua baadhi ya mateka hao kuwa sadaka. Lakini sadaka haikuwa kwa miungu au mizimu fulani, bali ilikuwa kwa mamba walioishi katika ziwa Viktoria. Mateka walipelekwa juu ya mwamba mrefu na hapo walisukumwa majini ili wadakwe na mamba.

II

Sadaka iliyotolewa kwa mamba haikuwa ya mateka wa vita tu, lakini hata watu walioasi na waliohukumiwa kufa walipelekwa kwa muda mrefu sana. Baadaye kuwatolea mamba sadaka ya watu kulihesabiwa kuwa tambiko la mfalme, jinsi hata makabila mengine walivyotambika mizimu na kuwaabudu kama wenye uwezo mwingi.

III

Hivyo mamba walizoea kufika chini ya mwamba mara walipoposikia sauti za watu, na walitumaini kupewa kitoweo chao. Lakini sasa Wazungu walipofika na kuanza kustaarabisha nchi, hawakupendezwa na mambo hayo ya ukatili. Hivyo wakakomesha desturi hiyo na mamba hawakupata kitoweo chao tena. Mamba wengine walipokuja mara nyingi wasione kitu walikata tamaa na hawakuja tena.

I

II



III

IV

Mamba mmoja wao hakuweza kusahau shibe ile, na hivyo aliendelea kufika kila siku akitumaini kupata chakula. Mfalme aliposikia habari hizo alimhurumia mamba huyo na aliwaweka watu kumvulia mamba samaki, na kumtupia badala ya watu.

V

Twajua hakika kwamba mamba huishi pamoja na samaki kule majini. Mamba huhangaika kufukuzana na samaki majini na ana shida kujipatia chakula cha kutosha. Akikosa samaki au nyama nyingine hulazimishwa kujitafutia chakula katika changarawe na uchafu mle ziwani. Hivyo mamba alifurahi sana kulishwa hivyo kwa msaada wa watu.

VI

Watu wale walimlisha mamba huyo kwa muda mrefu sana, hata mamba akawazoea watu na kufanya urafiki nao. Mwishowe akapewa jina "Lutembe."

Watu walipomletea Lutembe samaki, na walipoona kwamba hayuko, walimwita kwa jina lake hivi:- "Lutembe, Lutembe, njoo ule!" Lutembe akisikia sauti hiyo wakati wa matembezi yake, huja mbio sana kwenye mahali sauti ilipotokea ili apokee zawadi yake.

IV

V

VI

VII

Kwa muda wa miaka mingi Lutembe alilishwa na watu, na hata sasa yu hai angali rafiki wa watu. Wavuvi wanaovua upande ule wa ziwa Lutembe anakokaa, wakipenda kumfurahisha, humwita mpaka aje kwenye nchi kavu na kumpa samaki. Karibu wavuvi wote wa upande ule wanampenda Lutembe kwa sababu hasumbui watu wanapokwenda kuvua samaki.

VIII

Lutembe ni maarufu sana. Watu wengi waliotoka Ulaya, wakipata bahati kusikia sifa za Lutembe, huenda kumtazama katika ziwa. Wasipomwona wafikapo, watu husema kwamba amekwenda kutembea. Wageni wakitaka kumwona, basi humwita kwa sauti kubwa, naye Lutembe akisikia sauti zao huja upesi. Huendelea kumwita mpaka atoke majini ili wageni wapate kumwona vizuri. Pengine mtu mmoja hushika kipande cha samaki na kukipigapiga chini, naye Lutembe hujongea hata karibu kabisa na kutambaa pwani. Siku hizi Lutembe ni mzee sana, lakini bado anazo nguvu zake.

IX

Siku moja Lutembe alipokwenda kutembea alirudi na mwanawe, lakini walianza kumtupia mawe. Hivyo alifikiri kwamba rafiki zake kati ya watu hawampendi mwanawe, na hivyo alimrudisha asimlete tena. Lakini yeye mwenyewe tu hufika kuwaamkia rafiki zake na kupata chakula.

Mamba ni mnyama mkali na ni adui ya binadamu, lakini mnyama yeyote, hata awe mkali, akitendewa ukarimu pengine hugeuka kuwa rafiki ya wanadamu.

VII

VIII

IX

3RD PERIOD | PATTERN DRILL I | LESSON 77

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 77

Step 1
Hatua ya 1 Repetition and Substitution drills

1. Repetition drills

   a. Kenya imepata uhuru wake.

   b. Urefu wa mlima ni futi kama 19,000.

   c. Uingereza ni nchi ya Waingereza.

   d. Mara kwa mara uzuri wa uso unaweza kudanganya.

   e. Ugomvi ni ujinga mtupu.

   f. Kuta zina nyufa.

   g. "Usipoziba ufa utajenga ukuta".

2. Substitution drills

   (Change underlined words to plural and make other changes as necessary in the sentences.)

   a. Waimbaji waliimba <u>wimbo mmoja</u>.

   b. Bwana amepoteza <u>wembe wake</u>.

   c. <u>Ufunguo</u> huu si wangu.

   d. <u>Taa hii</u> yataka utambi mpya.

   e. <u>Mtu</u> huyu ana ugonjwa mbaya.

   f. Uso wa <u>mwanamke</u> una huzuni.

   g. <u>Ukuta</u> wa nyumba umebomoka.

3RD PERIOD | PATTERN DRILL I | LESSON 77

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 77

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework: Preparation of the story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 77

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 77

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 77

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 77

Step 1
Hatua ya 1

1. Recombination response drills

a. Ufagio uko wapi?
Ufagio uko nyumbani.

b. Nenda ukaniletee kuni ndefu.
Ninakwenda sasa kuzileta.

c. Kule Uingereza watumia lugha gani?
Kule Uingereza watumia Kiingereza.

d. Unga ulitosha kwa mikate?
Ndio ulitosha kwa mikate mitatu.

e. Uji una moto?
Ndio uji una moto na upo mezani.

f. Wanafunzi wanaimba nyimbo?
La, wanapiga kelele tu.

g. Mwuzaji yupo mlangoni?
Ndio, na anauza fagio.

h. Nilete kuni kesho?
Usilete kesho, labda kesho kutwa.

Step 2
Hatua ya 2 The students will retell in brief form the story of "Three Men and a Lion." The lexical items of Lesson 73 should first be reviewed briefly.

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 77

SOMO LA 77

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

I. LANGUAGE STRUCTURE

The U class of nouns has the following features:

a. Many U class nouns are abstract - that is they denote qualities and states. They are formed from adjectives by prefixing "u" and from nouns by changing the class prefix to "u", or to "w" before a vowel.

e.g. ukubwa = size
urefu = length
wizi = theft

b. Names of countries are U class words:

e.g. Uingereza = England
Ureno = Portugal

c. Some U class nouns are names of objects:

e.g. Ubao = a plank
Ukuta = a wall
Wembe = a razor

d. Formation of the plural:

1. Most abstract nouns in the U class do not take a plural.

2. Names of objects in the U class take a plural following the rules of the N class plural. (Review Lesson 29)

e.g.

Singular	Plural
u-devu - a single hair of beard	n-devu - beard
w-imbo - a song	ny-imbo- songs
u-bao - a plank	m-bao - planks
u-fagio- a broom	fagio - brooms
u-kuni - a stick of firewood	kuni - firewood

3. When the noun has only one syllable after the "u" prefix, the "ny" plural is prefixed to the whole word:

   e.g. u-so - a face nyuso - faces

4. Notice 2 other sound changes:

   n + w = mb u-wati = a hut-pole mbati = hut poles
   n + l = nd u-limi = a tongue ndimi = tongues

e. Adjectives:

1. In the U class the adjective prefix of the singular is "m" before consonants and "mw" before vowels.

   e.g. ubao mrefu ukuta mweupe
   ulimi mkali ukuta mwembamba

2. To form the plural of adjectives qualifying nouns of the "U" class, follow the rules of the N class.

   e.g. mbao ndefu = long planks
   nyimbo mbili = two songs

3. Notice that some U class words take a MA class plural, in which case the MA class plural is also used for the adjective. There are very few of these words.

   e.g. Ugonjwa mbaya = a bad disease.
   Magonjwa mabaya = bad diseases.

f. In the case of pronouns and words derived from pronouns, the U class is the same in the singular as the M-MI class, and in the plural as the N class.

1. Possessives:

   e.g. ufagio wangu — fagio zangu

2. Demonstratives:

   e.g. wembe huu — nyembe hizi
   wembe ule — nyembe zile

3. Pronoun prefixes with verbs:

   Subject: Ufunguo umepotea — funguo zimepotea

   Object: Nimeuona — nimeziona

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 78

1416- 1417

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The Passive Verb form WA (iwa, ewa, liwa, lewa).

Refer to Generalization for explanation of structural features in this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational setting: Series of scenes from folk tale: "The Punishment of the Man Who Had No Gratitude". Part I

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

adhabu	(punishment)
andalia	(prepare for)
daima	(permanently)
dhiki	(distress)
farasi	(horse)
kito (vi)	(precious stone)
kwenda shoti	(to gallop)
laani (ku)	(to curse)
matofaa	(fruit of the rose-apple tree)
mfua dhahabu	(goldsmith)
mhunzi	(blacksmith)
mkufu (mi)	(light ornamental chain)
mkungu (mi)	(Indian almond tree)
mwovu	(a wicked person)
piga yowe	(to shout)
sadiki	(believe)
shughuli	(business)
shukrani	(gratitude)
sikitika	(be sorry)
sonara	(jeweller, silversmith)
tumbili	(small light colored monkey)
tumbukia	(tumble into)
uhunzi	(work of a smith)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 78

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 78

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on the Passive form of the verb.

a. Juma aliandika barua
Barua iliandikwa na Juma

b. Mtoto alivunja kikombe
Kikombe kilivunjwa na mtoto

c. Tuliamkia wageni
Wageni waliamkiwa na sisi

d. Kapteni alitoa amri
Amri ilitolewa na kapteni

e. Adui waliharibu mji
Mji uliharibiwa na adui

f. Juma alioa binti yule
Binti yule aliolewa

g. Asha alichukua mzigo
Mzigo ulichukuliwa na Asha.

2. Drills using new expressions

a. Kuwa na shukrani
Mtu asiyekuwa na shukrani
Adhabu ya mtu asiyekuwa na shukrani

b. Kiumbe cho chote
Kiumbe cho chote kisichokuwa na shukrani

c. Lo lote atakalosema
Kusadiki lo lote atakalosema
Haifai kusadiki lo lote atakalosema

d. Hatari yo yote
Utakapotokewa na hatari yo yote

e. Msaada wo wote
Ukitaka msaada wo wote

f. Sauti ya dhiki
Akasikia sauti ya dhiki
Akasikia sauti ya dhiki ya kuomba msaada.

g. Kulaani daima
Mungu atanilaani daima.

h. Shughuli zake
Alipokwisha maliza shughuli zake.

i. Kwenda shoti
Farasi alikwenda shoti.
Alikwenda shoti hata alimtupa chini mwana wa sultani.

2ND PERIOD SWAHILI NARRATIVE LESSON 78

KIPINDI CHA PILI SOMO LA 78

ADHABU YA MTU ASIYEKUWA NA SHUKRANI

I

Safari moja, mtu mmoja alikuwa akisafiri katika pori. Baada ya muda mfupi, akasikia sauti ya dhiki ya kuomba msaada. Basi alifuata upande ule aliosikia sauti, naye alipofika, aliona shimo kubwa sana, na ndani yake mmetumbukia simba, tumbili, nyoka na mwanadamu.

II

Simba alipomwona yule mwanadamu, akasema, "Rafiki yangu, tafadhali nitoe katika shimo hili!"

Lakini yule mwanadamu akamwambia, "Nasikitika sana, simba, naogopa kukutoa nje. Nikikutoa hakika utanila."

Simba akajibu, "Kufanya hivyo ni kutokuwa na shukrani. Na kama nikifanya hivyo, Mungu atanilaani daima. Usiniogope, rafiki yangu. Tafadhali unihurumie."

Basi yule mtu akatafuta kamba, akamtoa yule simba nje ya lile shimo.

III

Kisha tumbili naye akamwomba yule mtu msaada kama simba. Kwa hiyo akamtoa naye pia.

Nyoka akamwambia, "Nitoe na mimi pia."

Mwanadamu akamwambia, "Niko tayari kukutoa nje ya shimo, lakini huna budi kuniahidi kwamba hutaniuma."

Nyoka akamwambia, "Sitathubutu hata kidogo. Mungu hapendezwi na kiumbe cho chote kisichokuwa na shukrani."

I

II

III

IV

Basi yule mtu akamtoa nyoka nje ya shimo. Kisha wale wanyama watatu--simba na tumbili na nyoka wakamwambia yule mtu, "Hala hala usimtoe yule mwanadamu nje ya shimo hili, mwache mle mle. Yeye ni mwovu sana, tena haifai kusadiki lo lote atakalosema."

V

Halafu simba akasema, "Mimi nakaa juu ya mlima ule. Nitafurahi sana kama utakuja kunitazama kule. Natumaini nitaweza kukulipa fadhili zako hizi za leo."

Tumbili akasema, "Mimi nakaa karibu na simba huyu, lakini nyumba yangu ni juu ya mkungu. Ukienda kwa simba, kisha njoo na kwangu mimi vile vile."

VI

Nyoka naye akasema, "Utakapotokewa na hatari yo yote, basi nikumbuke, nami nitakujia mara moja."

Kisha wale wanyama watatu waliondoka na kwenda zao.

IV

V

VI

VII

Wakati ule ule, yule mtu aliyekuwamo ndani ya shimo aliendelea kupiga yowe la kuomba msaada tu. Ingawa wale wanyama walimwambia asimwokoe yule mwanadamu mwenziwe, lakini huruma zikamjia, naye akaona si vema. Wanadamu kwa wanadamu hawana budi kusaidiana. Akawaza, "Leo kwa mwenzangu, kesho kwangu." Basi akamtoa nje ya lile shimo.

VIII

Yule mtu aliyeokolewa akasema, "Asante sana kwa msaada wako. Mimi kazi yangu ni ya uhunzi na sonara. Nina duka langu mjini. Ukitaka msaada wo wote juu ya vito vya dhahabu, basi njoo nyumbani kwangu au dukani." Kisha yule mtu akaenda zake, na yule msafiri akaendelea na safari yake.

IX

Yule msafiri alipokwisha maliza shughuli zake, na sasa anarudi nyumbani kwake, akawakumbuka wale wanyama aliowatoa nje ya shimo, kwa hiyo akafanya shauri aende kwa tumbili.

Alipofika, tumbili akampa embe, ndizi, machungwa na matofaa. Matunda hayo yalimburudisha sana. Kutoka kwa huyo, akaenda zake mpaka kwa simba, pale pale karibu.

VII

VIII

IX

X

Simba alipomwona alifurahi sana, akasema, "Nimekuwa nikikutazamia sana. Imekuwa vema umekuja, maana nina zawadi za kukupa." Simba akatoa mkufu wa dhahabu na vito vingi vya thamani, akaeleza jinsi alivyovipata. Akasema, "Safari moja farasi mmoja alikuwa amemchukua mwana wa sultani. Alikuwa anakwenda shoti sana hata mwishowe akamtupa chini yule mwana wa sultani na kumwacha pale pale peke yake. Basi mwana wa sultani alijipiga na mwamba akafa pale pale.

XI

Mtu yule alishukuru sana kwa kupata bahati ya vitu vya thamani. Kisha akaendelea na safari yake.

Alipokuwa njiani akawaza, "Ah, nitakwenda kwa yule mfua vyombo vya dhahabu, yule sonara niliyemtoa shimoni, nami nitamwomba aniuzie vitu hivi."

Basi akamwendea, naye akamkuta yumo kazini. Yule sonara akamkaribisha vizuri, akamwandalia wali kwa nyama, akamtengenezea kahawa na kila kitu cha kumburudisha.

XII

Baada ya hayo, yule mtu akamwonyesha yule sonara vile vitu vya thamani, akamwomba amwuzie.

Kumbe, vitu vile vilikuwa vya mwana wa sultani wa mji ule ule aliokuwa akikaa sonara. Tena vilitengenezwa na sonara yule yule, kwa hiyo aliweza kuvitambua upesi.

X

XI

XII

3RD PERIOD | PATTERN DRILLS | LESSON 78

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 78

Step 1
Hatua ya 1 Drills on the Passive Verb form - WA.

1. Repetition drills

a. Barua ilisomwa na mwalimu.

andika, chukua

b. Shauri lilikubaliwa na wazee.

kataa, sahihi

c. Nguo zimeharibiwa na watoto.

rarua, peleka

d. Mtumishi atapewa mshahara.

kazi, nyumba

e. Machungwa haya yalinunuliwa lini?

uza, chuma

f. Je, kuku wamelishwa?

funga, pika

g. Ni vigumu kuonyesha jinsi tulivyotendewa vyema.

karibisha, safirisha

2. Transformation drills - Supply suitable verb form.

a. Wazee walitengeneza pombe.
Pombe _____na wazee.

b. Juma alijenga nyumba.
Nyumba_____na Juma.

c. Msichana yule ataolewa na mwenzetu Ali.
Mwenzetu Ali_____msichana yule.

d. Baba hajayalipa madeni.
Madeni_____na Baba.

e. Mtumishi alisafisha taa.
Taa_____na mtumishi.

f. Koti hili lilishonwa na fundi.
Fundi_____koti hili.

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework: Study of the story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 78

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 78

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story.

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 78

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 78

1. Comprehension drills - These will be read orally, or on tape, and the student's comprehension will be checked.

   a. Huna budi kuniahidi kwamba hutaniuma.

   b. Mungu hapendezwi na kiumbe cho chote kisichokuwa na shukrani.

   c. Mateka waliotakiwa kutolewa sadaka walipelekwa juu ya mwamba mrefu, wakasukumwa majini wadakwe na mamba.

   d. Nchi ilipoingiwa na Wazungu na kuanza kustaarabishwa, mambo ya ukatili yalikomeshwa.

   e. Lutembe ni maarufu sana; watu wengi waliotoka Ulaya, wakipata bahati ya kusikia sifa zake huenda kumtazama katika ziwa.

   f. Utakapotokewa na hatari yo yote, basi nikumbuke, nami nitakujia mara moja.

   g. Alipokuwa njiani akawaza, "Ah, nitakwenda kwa yule sonara, nami nitamwomba aniuzie vitu hivi."

   h. Nyie watu, mnasema nini hapa?

   i. Kisha msichana aliulizwa kama atakubali kuolewa naye.

   j. Tangu kuzaliwa kwangu sijaona mtu mpumbavu kama wewe. Nitazuiwa na nini sasa nisikule?

   k. Yule mtu aliyeokolewa akasema, "Asante sana kwa msaada wako."

   l. Kumbe, vitu vile vilikuwa vya mwana wa sultani wa mji ule ule. Tena vilitengenezwa na sonara yule yule, kwa hiyo aliweza kuvitambua upesi.

2. Following the comprehension drill, the instructor will give the English of the above sentences and the student will give the Swahili equivalent.

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 78

SOMO LA 78

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

DERIVED FORMS OF VERB - GENERAL INTRODUCTION

1. The student has learned about the many prefixes in the Swahili language. It is now time to study some of the endings, or suffixes, expecially the various endings pertaining to derived forms of the verb. These derived verb forms do not express personal prefixes nor tenses, but rather special characteristics in meaning.

   e.g. Here are some of the common forms:-

pita	- pass	(simple)	
pitia	- pass through	(Prepositional	- (A)
pitisha	- make it pass	(Causative	- (SHA)
pitika	- passable	(Stative	- (KA)
pitiwa	- be passed	(Passive	- (WA)
pitana	- pass each other	(Reciprocal	- (ANA)

   The addition of these endings colors the basic meaning of the word, and often changes it quite a bit. It is wise to consult the dictionary when in doubt.

2. The addition of these endings usually requires the use of a phonetic link between the stem and the ending. These links are:- I, E, LI, or LE, depending on the nature of the vowels in the next-to-last syllable. The student will also learn and appreciate the many ways shades of meaning can be expressed by not only using these basic derived forms, but also combining and building one form on top of the other. More reading and use of Swahili will acquaint the student with these forms, and reference to the dictionary is advisable.

   e.g. acha - leave, let alone
   achia - leave to someone, bequeath
   achilia - forgive
   achiliwa- be forgiven

A.

Verb stems with 1 vowel endings and penultimate being:	have as a link	Sample verbs with prepositional (A) ending:
A		fany-i-a > fanyia
I	I	pit-i-a > pitia
U		fung-i-a > fungia
And penultimate being:		
E	E	tend-e-a > tendea
O		som-e-a > somea

B.

Verb stems with 2 or more vowel endings and penultimate vowel being:	have as a link	Sample verbs with ending:
A (AA)	LI	(kaa) ka-li-a > kalia
I (IA)		(tia) ti-li-a > tilia
U (UA)		(fungua) fungu-li-a > fungulia
And penultimate vowel being:		
E (EA)	LE	(pendea) pende-le-a > pendelea
O (OA)		(toa) to-le-a > tolea

VOLUME VI | GENERALIZATION | LESSON 78

KITABU CHA VI | SOMO LA 78

1. The WA and KA forms of the verb.

In this and the following lesson we shall learn the Passive (WA) and the Stative (KA) forms of the verb.

Notice the following:

Doer	Receiver	Result of Action
Action	Passive (WA)	Stative (KA)

Alivunja kikombe
Kikombe kilivunjwa na mtoto. (Passive)
Kikombe kimevunjika. (Stative)

2. In this lesson we shall pay special attention to the Passive form.

a. The Swahili passive is formed by putting W between the verb stem and the final vowel A.

e.g. Kupiga - to hit Kupigwa - to be hit
Kupenda - to love Kupendwa - to be loved

b. Verbs in this form take exactly the same person and tense signs, for all classes, as they do in the simple form.

e.g. Active	Passive
Ninapiga-I am hitting	Ninapigwa-I am being hit.
Nitapiga-I shall hit	Nitapigwa-I shall be hit.
Sipigi-I do not hit	Sipigwi-I am not hit.

c. To express BY or WITH after the passive, the words NA and KWA are generally used.

e.g. Alipigwa na baba yake - He was beaten by his father.

Mkate ulikatwa kwa kisu - The bread was cut with a knife.

d. Note: Verbs ending in 2 or more vowels (aa, ia, ua, oa) form their passive by using the link LI or LE before the suffix. (Study again the pattern diagram in the General Introduction to the Derived Forms of the Verb.)

e.g.	Kuvaa	Passive -	Kuvaliwa
	Kuoa		Kuolewa
	Kuchukua		Kuchukuliwa

e. There are 2 irregular passives:

Kuua	Passive -	Kuuawa
Kusahau		Kusahauliwa

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 79

VOLUME VI | BLUE PRINT | LESSON 79

KITABU CHA VI | SOMO LA 79

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The Stative verb form KA (ika, eka, lika, leka).

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from folk tale: "The Punishment of the Man Who Had No Gratitude". Part 2

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

banwa	(be squeezed)
fariki dunia	(die, depart this life)
gusa (ku)	(to touch)
hekaheka	(confusion, much noise)
husu	(to concern, apply to)
kata roho	(die)
kitanzi	(noose)
malkia	(queen)
marehemu	(the deceased, the late)
mbashiri	(fortune teller)
mchawi	(witch)
mhalifu	(one who breaks the law)
mnara (mi)	(tower, lighthouse)
nyongwa	(to be harassed)
nyosha	(stretch out)
pigwa marungu	(to be beaten with a knobkerry)
shoka (ma)	(axe)
staajabu	(to be astonished or surprised)
subiri	(wait patiently)
tia gerezani	(put in prison)
twangwa kinuni	(be pounded in a mortar.)

c. Lexical items continued

uawa	(to be killed)
upanga	(sword)
waama	(moreover, then)
zahama	(confusion, noise)
zikwa mzima	(be buried alive)
zuka	(suddenly appear, pop up)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 79

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 79

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on the Stative form of the verb.

   a. Kikombe kimevunjika.
      Vikombe vimevunjika.

   b. Nguo hizi zavalika.
      Nguo hizi hazivaliki.

   c. Matunda mabivu yaonekana leo.
      Matunda mabivu hayaonekani leo.

   d. Njia hii yapitika.
      Njia hii haipitiki.

   e. Siwezi kufunga mlango.
      Mlango haufungiki.

   f. Siwezi kufungua mlango.
      Mlango haufunguki.

2. Drills using new expressions

   a. Kutoswa baharini
      Kutupwa kutoka juu ya mnara
      Kuchomwa moto

   b. Kushindishwa na njaa
      Kunyweshwa sumu
      Kukalishwa juu ya kiti cha moto

c. Kubanwa na chuma
Kukokotwa na farasi
Kukatwa kichwa kwa upanga

d. Kutiwa kitanzi na kutundikwa
Kukatwa kwa msumeno katikati ya mwili
Kutupwa mbele ya wanyama wakali

e. Kutwangwa kinuni
Kuzikwa mzima
Kupigwa marungu mpaka ufe

f. Kuhukumiwa na kuchunguzwa
Kuhukumiwa na kuchunguzwa kama ni mhalifu

g. Tayari kwa kuuawa
Awekwe tayari kwa kuuawa
Sultani aliamuru awekwe tayari kwa kuuawa.

h. Namna utakavyopenda kuuawa
Uchaguo wa namna utakavyopenda kuuawa
Nitakupa uchaguo wa namna utakavyopenda kuuawa.

i. Akatiwa gerezani
Akisubiri kunyongwa
Akatiwa gerezani akisubiri kunyongwa.

j. Mara kukazuka zahama.
Mara kukazuka zahama katika nyumba.

k. Marehemu
Marehemu mwanangu
Vito vya thamani vya marehemu mwanangu

XIII

Basi sonara alijifanya kama kwamba anakwenda kutafuta mnunuzi, kwa hiyo akamwacha yule mgeni wake nyumbani kwake, akamwambia amngojee. Lakini yeye hakwenda kutafuta mnunuzi, bali alikwenda moja kwa moja mpaka kwa Sultani. Na kumbe sultani mwenyewe alikwisha tangaza kwamba ikipatikana habari yo yote inayomhusu mwanawe aliyepotea, basi itatolewa zawadi kwa yeye atakayemwarifu.

XIV

Sultani akamwuliza yule sonara, "Vitu vya thamani hivi umevipata wapi?"

Akajibu, "Amekuja mtu mmoja kwangu, naye ameniomba nimwuzie, kisha fedha nimpe. Lakini nimeona heri kwanza nikuletee upate kuviona."

Sultani akamwambia, "Bila shaka yeye ndiye aliyemwua mwana wangu ili avipate. Kamlete upesi!"

XV

Basi yule mtu alikamatwa na kuletwa mbele ya sultani. Bila kuhukumiwa na kuchunguzwa vema kama ni mhalifu hasa au siyo, sultani aliamuru awekwe tayari kwa kuuawa baada ya siku chache.

XIII

XIV

XV

XVI

Basi yule mtu maskini akatiwa gerezani, akisubiri kunyongwa. Akasema, "Waama sasa nimo katika hatari kubwa ya kuitoka dunia. Natumaini yule nyoka ataweza kunisaidia sasa!" Katika kusema hivi, mara nyoka akatokea pale pale. Akasema, "Rafiki yangu, nikutendee nini sasa?"

Yule mtu akasimulia kisa chote, tangu mwanzo wake mpaka mwisho.

XVII

Yule nyoka akamwambia, "Nisikilize. Sasa nitakwenda kumwuma malkia wa sultani. Waganga, wanajimu, wachawi na wabashiri wote wataitwa kufanya maarifa yao ili wamponye, lakini nina hakika watashindwa. Hawataweza kumponya malkia. Lakini wewe utakapofika na kumgusa kwa mkono wako, basi atapona mara moja."

XVIII

Kisha yule nyoka alitoka na kwenda zake. Mara kukazuka zahama katika nyumba ya sultani, maana malkia alikuwa amekwisha umwa na yule nyoka. Ikawa heka heka, malkia yumo katika hatari ya kufa. Watu wakafanya yote waliyoweza ili kumponya, lakini wapi! Kila mmoja alishindwa.

Sultani alipeleka habari mjini upesi upesi na kuwaambia watu kwamba ye yote atakayeweza kumponya malkia, atapewa zawadi kubwa sana hata watu wote watastaajabu.

XVI



XVII

XVIII

XIX

Yule mtu kule gerezani akawaambia askari walinzi kwamba yeye ataweza kabisa kumponya malkia. Kwa hiyo akapelekwa kwa sultani upesi kabla malkia hajakata roho bado.

Alipofika, sultani akamwingiza katika chumba alichokuwamo yule malkia. Wakati huu fahamu yote ilikuwa imekwisha mtoka, na ilikuwa bado dakika chache tu kwa kufariki dunia.

Basi yule mtu akanyosha mkono wake na kumgusa yule malkia. Mara pale pale aliinuka akaanza kucheka na kuzungumza. Akawa mzima kabisa kama zamani.

XX

Pale pale sultani akampa yule mtu aliyemponya malkia zawadi nyingi sana za kila namna. Kisha akamwambia, "Sasa niambie jinsi ulivyoweza kupata vito vya thamani vya marehemu mwanangu."

Yule mtu akamsimulia kisa chote tangu mwanzo mpaka mwisho.

XXI

Basi sultani akamwita yule sonara, akamwambia, "Sasa nimepata hakika ya mambo yote jinsi yalivyokwenda. Waama wewe ni mwovu sana. Ulitaka kuitoa roho ya mwenzio bure naye ni mtu aliyekusaidia ulipokuwa katika hatari! Sasa yeye atafunguliwa na kuachwa huru, na wewe utauawa sasa hivi mbele ya watu wote wa mji.

XIX

XX

XXI

XXII

Kwa huruma zangu, nitakupa uchaguo wa namna utakavyopenda kuuawa. Je, utapenda uuawe namna gani? Kukatwa kichwa kwa upanga au shoka, kutiwa kitanzi na kutundikwa, kukatwa kwa msumeno katikati ya mwili, kutupwa mbele ya wanyama wakali kama vile chui, simba au mbwa wa mwitu, kutwangwa kinuni, kuzikwa mzima, kupigwa marungu, mawe, mishale, au mkuki mpaka ufe.

XXIII

Au utapenda kuuawa kwa kutoswa baharini, kutupwa kutoka juu ya mnara mrefu, kuchomwa moto, kushindishwa n[illegible] njaa, kunyweshwa sumu, kukalishwa juu ya kiti cha moto, kubanwa na chuma au utapenda kufungwa na kukokotwa na farasi anayekwenda shoti? Haya chagua upesi!"

XXIV

Yule mtu akachagua kukatwa kichwa kwa upanga.

Basi baada ya watu wote kukusanyika pamoja, sultani akamwamuru askari mmoja alete upanga mkali akamkate kichwa upesi. Yule mtu akakatwa kichwa pale pale mbele ya watu wote. Basi hii ndiyo adhabu aliyopewa kwa kutokuwa na shukrani ya fadhili aliyotendewa na mwenziwe.

XXII

XXIII



XXIV

3RD PERIOD | PATTERN DRILLS | LESSON 79

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 79

Step 1
Hatua ya 1 Drills on the Stative Verb Form

1. Repetition and Substitution drills.

a. Koti langu limeraruka.

kanzu, shati, suruali

b. Askari amesumbuka kwa maneno ya kapteni.

huzunika, kasirika

c. Chakula hiki hakiliki.

matunda, mkate

d. Nionyeshe njia inayopitika, hii haipitiki.

ambia, pitisha

e. Vitabu hivi vyasomeka.

magazeti, barua

2. Pattern response drills

a. Bwana ameshughulika sasa?
Ndio Bwana ameshughulika.

b. Umefunga mlango?
La, mlango huu haufungiki.

c. Tafadhali fungua madirisha.
Madirisha haya hayafunguki.

d. Jinsi gani nguo zimeharibika?
Zimeharibiwa na mvua.

e. Umepewa fedha na baba yako?
Ndio baba yangu alinipa fedha.

f. Makosa yetu yamesahaulika?
Ndio, tumeyasahau yote.

g. e, Mtumishi, kazi hii yafanyika?
La, Bwana, kazi hii haifanyiki.

h. Maneno haya yameandikwa na nani?
Yameandikwa na Rais.

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework: Study of the story for retelling.

4TH PERIOD (First Hour in the Morning) LESSON 79

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 79

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story.

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

1. Comprehension Drills

These will be read orally, or on tape, and the student's comprehension checked.

a. Yule mtu alikamatwa na kuletwa mbele ya sultani. Bila kuhukumiwa na kuunguzwa vema kama ni mhalifu hasa au siyo, sultani aliamuru awekwe tayari kwa kuuawa.

b. Wakati huu fahamu yote ilikuwa imekwisha mtoka, na ilikuwa bado dakika chache tu kwa kufariki dunia.

c. Kisha wale wanyama watatu waliondoka na kwenda zao.

d. Mnyama ye yote na awe mkali atakavyokuwa, akitendewa ukarimu bila shaka hugeuka kuwa rafiki ya wanadamu.

e. Aliona shimo kubwa sana, na ndani yake wametumbukia simba, tumbili, nyoka na mwanadamu.

f. Haifai kusadiki lo lote atakalosema.

g. Leo kwa mwenzangu, kesho kwangu.

h. Yule mtu akasimulia kisa chote, tangu mwanzo wake mpaka mwisho.

i. Mara kukazuka zahama katika nyumba.

j. Baada ya watu wote kukusanyika pamoja, sultani akamwamuru askari mmoja alete upanga mkali aka-mkate kichwa upesi.

2. Following the comprehension drill, the instructor will give the English of the above sentences and the student will give the Swahili equivalent.

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 79

SOMO LA 79

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

1. The Stative (KA) form of the Verb.

The characteristic ending of the Stative form of the verb is KA. Refer again to the Pattern Diagram in the General Introduction to the Derived Forms, to make sure that you understand the formation of the phonetic links between the stem and the ending.

e.g. Kata - Katika
Vunja - Vunjika
Sema - Semeka
Soma - Someka
Twaa - Twalika

2. The Stative form is used for 2 purposes:

a. To express a resulting state or condition after an action.

e.g. Aluvunja kikombe, sasa kikombe kimevunjika.
He broke the cup, now the cup is broken.

Notice again that **no one** is named as having broken the cup. If someone is named, then the passive is used.

e.g. Sahani imevunjwa na mtoto.
The plate was broken by the child.

Sahani imevunjika.
The plate broke.

Maji yalimwagwa na fulani.
The water was spilled by so-and-so.

Maji yalimwagika.
The water got spilled.

b. The Stative form is also used to express the idea of possibility, i.e. be edible, be passable, etc.

e.g. Kupita - To pass Kupitika - To be passable
Kula - To eat Kulika - To be edible

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 80

1458-1459

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The Prepositional verb form A. (ia, ea, lia, lea).

Refer to Generalization for explanation of structural features in this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from a story "Zerubabeli". Part I

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

akida (ma)	(leader, commander)
ambatana	(cling together)
angamia	(be destroyed, perish)
bembeleza	(coax, soothe)
changamko (ma)	(entertainment, amusement)
dalili	(sign, token)
deni	(debt)
enzi	(power)
fahari	(grandeur, glory)
hatamu	(bridle)
huzuni	(grief)
jimbo (ma)	(district, province, state)
kadhalika	(in like manner, likewise)
kilemba (vi)	(turban)
kitani	(flax, linen)
kodolea macho	(stare at)
kwaa (ku)	(to stumble)
lea	(rear, bring up)
levuka	(get sober)
liwali (ma)	(governor, headman)
madaha	(airs, graces)
mto	(cushion, pillow)
mvinyo	(wine, spirits)
nena	(speak, utter)
nyara	(booty, spoils, plunder)

piga chuku	(exaggerate)
rukwa na akili	(lose one's head)
suria	(concubine)
-taalamu	(educated, scholarly, well-informed)
taji	(crown)
tia muhuri	(seal, confirm, sign)
tokeza midomo	(pout)
towesha (ku)	(ruin)
toza kodi	(collect taxes)
Uajemi	(Persia)
ufafanuzi (ma)	(explanation, interpretation)
ukunjufu	(cheerfulness, good temper)
urujuani	(violet (color)
yatima	(orphan)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 80

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 80

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on the Prepositional forms of the verb.

   a. Aliandika barua.
      Aliniandikia barua.

   b. Nilipika chakula.
      Niliwapikia chakula.

   c. Mwanafunzi alisoma kitabu.
      Mwanafunzi alinisomea kitabu.

   d. Mtumishi alifagia nyumba.
      Mtumishi alinifagilia nyumba.

   e. Alinipatia kisu.
      Kisu cha kukatia nyama.
      Alinipatia kisu cha kukatia nyama.

2. Drills using new expressions

   a. Kukodolea macho
      Kwa nini unanikodolea macho?
      Usinikodolee macho.

b. Kurukwa na akili zao.
Ni wengi waliorukwa na akili zao.
Ni wengi waliorukwa na akili zao kwa ajili ya wanawake.

c. Kinywa wazi
Akamtazama kinywa wazi.

d. Kutokeza midomo
Mtoto alitokeza midomo.

e. Kubembeleza
Mama amembembeleza mtoto.
Kumbembeleza ili aridhie

f. Kupiga chuku
Alipiga chuku katika mambo yote.

2ND PERIOD | SWAHILI NARRATIVE | LESSON 80

KIPINDI CHA PILI | SOMO LA 80

KISA CHA ZERUBABELI

SEHEMU YA KWANZA

I

Hapo kale mfalme Dario alifanya karamu kubwa. Aliwaalika wakuu wa Umedi na Uajemi. Hao walikuwa maakida na majemadari, na wengine walikuwa maliwali katika nchi mbalimbali kutoka Bara Hindi mpaka Etiopya. Wote walifika karamuni, wakala, wakanywa, wakashiba, baadaye wakarudi kwao tena. Mfalme Dario akapumzika, akaingia chumbani mwake akalala usingizi.

II

Mfalme alipokuwa akilala, vijana watatu walimtumikia chumbani kwake na kumlinda mfalme. Hao walianza kuongea, wakasema: "Haya, tushindane. Kila mmoja wetu ataje kitu aonacho kina nguvu kupita vingine vyote, na aandike maoni yake juu ya karatasi. Halafu mfalme atakapoamka apewe maandiko yetu ayasome. Yule atakayeshinda apewe zawadi na heshima kubwa kutoka mfalme, kama:-

Kuvikwa mavazi ya urujuani,
Kupata kunywa kutoka kikombe cha dhahabu,
Kukilalia kitanda kizuri sana,
Kuchukuliwa katika gari na farasi wenye hatamu za dhahabu,
Kuvaa mkufu wa dhahabu shingoni mwake, na kadhalika.
Zaidi ya hayo aketi karibu na mfalme Dario na kuheshimiwa kama jamaa yake.

Basi wakaandika kila mtu neno lake, wakatia muhuri, wakaweka yote chini ya mto wa Dario. Wa kwanza aliandika: "Mvinyo ina nguvu kupita vyote." Wa pili akaandika: "Mfalme ndiye ana nguvu kabisa." Na wa tatu aliandika: "Wanawake ndio wenye nguvu nyingi zaidi, lakini kupita yote ukweli hushinda.

III

Mfalme alipokwisha kuamka, vijana walimletea maandiko yao wakampa. Mfalme alipokwisha kuyasoma alistaajabu sana, na hivyo aliwakusanya wakuu, madiwani na maakida wake waje kusikiliza vijana wakieleza kila mtu neno lake. Ndipo waamue ufafanuzi wa fikira za vijana na kumchagua mshindi.

LESSON 80-a

IV

Kijana wa kwanza aliyeandika kwamba "Mvinyo ina nguvu kupita vyote," akaeleza:- "Mabwana, mvinyo ina nguvu nyingi ajabu. Inawafanya wote watakaoinywa kufanya makosa. Kumbe, hufanya akili ya yatima hata ya mfalme kuwa sawa. Vivyo hivyo inawatendea watumwa na walio huru, maskini na tajiri, ikiwachafua akili zao na kuyageuza mawazo yao kuwa makunjufu na machangamko wasikumbuke deni wala huzuni. Watu wanapolewa kwa mvinyo pia husahau upendo wao kwa rafiki au ndugu, hata wavute upanga. Baada ya kulevuka hawawezi kukumbuka waliyo-yafanya. Je! si kweli, mabwana, ya kuwa mvinyo ina nguvu kupita vyote?" Naye alipokwisha kunena, akanyamaza.

V

Kisha yule wa pili aliyetaja kwamba "Mfalme ndiye ana nguvu kabisa," alipaaza sauti yake akasema:- "Mabwana, wale wenye nguvu hasa ambao wanatawala bahari na nchi na vitu vyote vilivyomo, si wanadamu? Lakini mfalme huzidi kwa nguvu. Ndiye bwana wao na huwatawala. Kwa mambo yote hutii kwa jinsi anavyoamuru. Akiwaamuru wapigane, wao hupigana; aki-waamrisha kupambana na adui, huenda na hushambulia maboma na ngome kuu. Kuua, wako tayari kuuawa, wala hawaihalifu amri ya mfalme. Ikitokea wameshinda, humletea mfalme vitu vyote vilivyotekwa vitani. Kadhalika wale wasio askari na kazi yao ni ukulima, pia humletea mfalme sehemu ya mavuno yao, na hutozwa kodi kwa ajili ya mfalme.

VI

Naye mfalme ni mtu mmoja tu; akisema, Ua, huua; aki-sema, Achilia, huachilia; akisema, Piga, hupiga; akisema, Jenga, hujenga; akisema, Kata, hukata; akisema Panda, hu-panda. Hivyo watu wote na majeshi yake yote humtii. Ikiwa mfalme analala, anakula, anakunywa, au anapumzika, wengine wanahudhuria na kumlinda. Hakuna awezaye kuondoka na ku-fuata shughuli zake mwenyewe. Basi, mabwana, yawezaje kuwa mfalme siye mwenye nguvu kupita wote ikiwa hutiiwa hivyo?" Naye pia akanyamaza.

LESSON 80-b



KIPINDI CHA PILI SOMO LA 80

VII

Ndipo kijana wa tatu aliyetaja kwamba, "Wanawake ndio wenye nguvu nyingi zaidi, lakini kupita yote ukweli hushinda," akasimama akasema:- "Mabwana, mlisikia habari za nguvu za mfalme, hata nguvu za mvinyo, lakini ni nani basi wanaotawala hata hao? Je, si wanawake?

Wanawake ndio waliomzaa mfalme na watu wote wanaotawala bahari na nchi. Ni wanawake waliowalea, waliowafanyizia wanaume mavazi yao na kuwaletea fahari yao. Pasipo wanawake wanaume hawawezi hata kuwapo. Zaidi ya hayo, ikiwa wanaume wamekusanya dhahabu na fedha, na wakimwona mwanamke mwenye madaha na sura nzuri ya kutamani, huacha vyote ili wamwachamie na wamkodolee macho. Kweli humtamani yeye kuliko dhahabu au fedha au vitu vingine.

VIII

Mwanamume humwacha baba yake aliyemlea, hata na nchi yake, ili aambatane na mkewe. Hakawii ili apate kuishi siku za maisha yake na mkewe, wala hakumbuki tena wazazi wala nchi yake.

Haikosi mtafahamu ya kwamba ndio ni wanawake wanaotawala mkifikiria haya:

Je, hamjibidishi kufanya kazi ili mletee mwanamke mapato yenu? Tena pengine mtu huchukua upanga wake akaenda kushambulia, kunyang'anya, na kuiba kwa ajili yake. Au husafiri juu ya bahari na mito, yu tayari kupambana na simba, kupitia nchi zenye giza, ili amletee mpenzi wake mapato yake. Hivyo mtu humpenda mkewe kuliko baba au mama. Naam, ni wengi waliorukwa na akili zao kwa sababu ya wanawake. Je, ninyi bado hamsadiki hayo?

IX

"Mwangalieni mfalme katika nguvu zake, na jinsi wote katika majimbo humwogopa hata kumgusa. Walakini juzi juzi nilimwona Apame, suria ya mfalme, jinsi alivyokuwa ameketi mkono wa kuume wa mfalme, akiitwa taji kutoka kichwa cha mfalme, akaiweka juu ya kichwa chake mwenyewe. Naam, hata akathubutu kumpiga mfalme kwa mkono wake wa kushoto. Ingawa mfalme alishtuka, alimtazama tu kinywa wazi. Suria akimchekea, naye hucheka pia; akimkasirikia naye hufanya bidii kumbembeleza ili amridhie tena. Ee mabwana, kweli kweli si dhahiri ya kuwa wanawake wana nguvu nyingi zaidi wakiweza kufanya hivyo?"

LESSON 80-C

3RD PERIOD | PATTERN DRILLS | LESSON 80

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 80

Step 1
Hatua ya 1 Drills on the Prepositional Verb Form

1. Repetition drills

a. Utanichagulia askari wanne kulinda zamu.

b. Mpishi atawapikia askari chakula chao.

c. Utakapofika kwako, nisalimie baba.

d. Kesho askari watahamia kambi nyingine.

e. Tuliwatafutia wagonjwa maua mazuri.

f. Bwana huwalipia watumishi wake mshahara wao.

g. Nipe fedha ili nikununulie chakula.

h. Nenda kaninunulie kisu cha kukatia nyama.

i. Viondolee mbali vitu hivi, sivitaki tena.

j. Rafiki yangu aliniandikia barua.

2. Pattern response drills

a. Watu wale wanamngojea nani?
Wanamngojea Sajini.

b. Ali amewajengea wazazi wake nyumba?
Ndio amewajengea wazazi wake nyumba mjini.

c. Serikali huwalipia walimu mshahara wao tarehe gani?
Serikali huwalipia walimu mshahara wao mwisho wa mwezi.

d. Nikuletee nini, bwana?
Tafadhali niletee maji ya baridi kunawia mikono.

e. Wanafunzi watatuimbia nyimbo?
Ndio watatuimbia nyimbo baadaye kidogo.

f. Nani amemlimia shamba lake?
Rafiki yake amemlimia shamba lake.

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework: Preparation of the story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 80

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 80

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story.

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 80

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 80

1. Comprehension drills - These will be read orally, or on tape, and the student's comprehension will be checked.

   a. Mtoto atakuchukulia mzigo wako.

   b. Tulinunua mitego ya kukamatia panya.

   c. Mawe haya hayafai ya kujengea nyumba.

   d. Yafaa sasa binti yetu aolewe. Huna budi kumtafutia mume.

   e. Lakini yule kijana mwanamke akakataa katakata kuolewa na Upepo. Alisema, "Nitafutie mume mwingine aliye mkuu zaidi kuliko yeye."

   f. Mwishoni akakubali kumfungulia mlango wa mtego.

   g. Ni kweli si haki kumlipa mwenzio mabaya ikiwa amekutendea fadhili njema.

   h. Walijijengea nyumba na kujilimia mashamba.

   i. Mfalme alifanya karamu kubwa kwa raia zake wote, na wote waliozaliwa nyumbani mwake.

   j. Basi ikawa, mfalme alipokwisha kuamka, walichukua maandiko wakampa, naye akayasoma.

   k. Akina bwana, wale wenye nguvu hasa, ambao wanatawala bahari na nchi na vitu vyote vilivyomo, si wanadamu?

   l. Naam, ni wengi waliorukwa na akili zao kwa ajili ya wanawake, hata kuuingia utumwa kwa ajili yao.

2. Following the comprehension drill, the instructor will give the English of the above sentences and the student will give the Swahili equivalent.

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 80

SOMO LA 80

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

1. The Prepositional Form of the Verb.

When a preposition like TO is used in English, the Prepositional Form of the Verb is used in Swahili. This is obtained by adding a vowel I or E between the stem and the final vowel. Study again the pattern diagram in the General Introduction, which gives the use of the phonetic link in the Prepositional Form of the Verb.

This gives us a form which means to do something for, to or with somebody or something, either for their advantage or for their disadvantage.

e.g. Alinileteа kofia - He brought me a hat.
Niletee chakula - Bring me food.
Aliniibia nguo - He stole clothes from me. (He stole my clothes)

Note that the object prefix must also be used.

2. Another use of the prepositional form of the verb is to show purpose.

e.g. Kisu cha kukatia nyama - A knife to cut meat with.
Masikio ya kusikilia - Ears to hear with.
Nyumba ya kukalia - A house to live in.

3. The Prepositional form of the verb can be used to express motion towards an object or place.

e.g. Mtoto alimkimbilia mama yake.
The child ran to his mother.

Mfalme alimgeukia mtumishi wake.
The king turned to his servant.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 81

1476 - 1477

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The Causative verb form ending in SHA or ZA.

Refer to Generalization for explanation of structural features in this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from a story, "Zerubabeli". Part 2

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

ahimidiwe Mungu	(God be praised!)
aidha	(further, moreover)
busu (ku)	(to kiss)
busu (ma)	(kiss)
dhabihu	(sacrifice)
diwani (ma)	(councillors)
elekea	(point or face toward)
hekalu (ma)	(temple)
konde (ma)	(cultivated piece of ground)
kuhani (ma)	(priest)
madhabahu	(place of sacrifice)
madhali	(since, because, seeing that)
milele	(always)
milki	(dominion, kingdom)
nadhiri	(vow, solemn promise)
pasha habari	(spread the news)
rushwa	(bribe)
thabiti	(firm, constant)
timiza	(fulfill, complete)
twaa	(take)
udhalimu	(injustice, tyranny)
ujenzi (ma)	(construction, building operations)
upendeleo (ma)	(favoritism)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 81

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 81

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on the Causative Verb Form

   a. Sahani imeanguka.
      Mtumishi aliangusha sahani.

   b. Watoto wameamka.
      Mama aliamsha watoto.

   c. Alinikataza kuingia.
      Walitukataza kwenda.

   d. Nilikujulisha habari.
      Ningependa kukujulisha rafiki yangu.
      Ningependa kujijulisha kwako.

   e. Dada alisafisha nyumba, sasa nyumba ni safi.
      Nimetayarisha chakula, sasa chakula ni tayari.

2. Drills using new expressions

   a. Kupasha habari
      Alipasha habari po pote.
      Akawapasha habari ndugu zake.

b. Udhalimu
Hamna udhalimu
Ndani yake hamna udhalimu.

c. Wanadamu wote ni dhalimu.
Matendo yao ni dhalimu.

d. Nadhiri
Akatoa nadhiri
Akatimiza nadhiri

e. Thabiti
Kweli hukaa thabiti

f. Hakuna upendeleo.
Hakuna upendeleo wala rushwa.

KISA CHA ZERUBABELI

SEHEMU YA PILI

I

Baada ya kueleza nguvu za wanawake, mfalme na madiwani walianza kutazamana, na hapo Zerubabeli aliendelea kutoa maoni yake juu ya Ukweli, akasema:- "Je, mabwana, wanawake si wenye nguvu? Basi na dunia ni kubwa, na mbingu ni juu, na jua laonekana kwenda mbio katika njia yake, mradi huzunguka mbinguni na kuparudia mahali pake katika siku moja. Je, yeye aliyeweka mpango kama huo ulimwenguni mzima siye mkuu? Ukweli wake ni mkuu, na una nguvu kupita mambo yote. Dunia hutafuta ukweli huo, na mbingu huibariki. Viumbe vyote hutetemeka mbele yake kwani haumo udhalimu ndani yake. Ila hapa duniani mvinyo ina udhalimu, mfalme aweza kuwa na udhalimu, wanawake huwa na udhalimu, kweli wanadamu wote ni dhalimu na matendo yao huonyesha hali ya udhalimu, wala hakuna ukweli ndani yake."

II

"Bali ukweli hudumu, daima u thabiti, huishi na kushinda hata milele. Kwake hakuna upendeleo wala rushwa; hutenda yaliyo haki na hupinga udhalimu wote na ubaya wote. Matendo yake huheshimiwa na wanadamu wote. Katika hukumu zake hakuna uovu, ni milki, uwezo na enzi siku zote hata milele. Abarikiwe Mungu wa Ukweli!" Ndipo akanyamaza, ilakini watu walipaaza sauti, wakasema: "Ukweli ndio ulio mkuu na una nguvu kupita mambo yote."

III

Hapo mfalme akamwambia Zerubabeli, "Omba lolote utakalo, hata zaidi kuliko yale yaliyoandikwa, nawe utapewa, maana umeonekana kuwa mtaalamu. Utaketi karibu nami na kuheshimiwa." Zerubabeli akamjibu mfalme: "Kumbuka nadhiri yako uliyoitoa siku ile uliposhika ufalme wako, ulipo ahidi kuujenga tena mji wa Yerusalemu uliobomolewa, na kuvirudisha vyombo vyote vilivyochukuliwa kutoka Yerusalemu. Pia uliahidi kuijenga tena hekalu iliyoteketezwa na Waedomi wakati nchi ya Yuda iliposhambuliwa na kuharibiwa na Wakaldea. Hivyo sasa nakusihi, ee mfalme, nionyeshe ukarimu wako wa kifalme na uitimize nadhiri ile uliyoitoa mbele za Mfalme wa Mbinguni kwa kinywa chako mwenyewe."

LESSON 81-a



IV

Ndipo mfalme Dario alisimama akambusu Zerubabeli. Halafu akaandika barua kwa ajili yake kwa watunza hazina wote, na kwa maliwali, na majemadari na maakida ili wamsaidie kufika Yerusalemu salama pamoja na wote watakaofuatana naye kwenda kuujenga tena mji wa Yerusalemu. Tena akawaandikia maliwali wote waliokuwako huko katika nchi ya Shamu, na Foiniki, na Lebanoni makusudi waipeleke mierezi ya Lebanoni mpaka Yerusalemu, na pia washirikiane naye katika kazi za kuujenga mji. Zaidi ya hayo aliandika kwa ajili ya Wayahudi wote waliokaa katika majimbo yake kwamba wapewe uhuru kurudi nchi ya Uyahudi. Alitoa amri wasitozwe kodi, na aliwaamrisha Waedomi waitoe miji ya Wayahudi waliyoishika wakati ule.

V

Pia aliamuru talanta ishirini zitolewe kila mwaka kwa ujenzi wa Hekalu; na siyo kwa ujenzi tu, lakini talanta hizo zitolewe hata wakati Hekalu itakapokwisha kujengwa. Zaidi ya hayo talanta nyingine kumi zitolewe kila mwaka kulipa gharama za dhabihu zitakazotolewa madhabahuni kila siku. Na makuhani wapewe posho yao na mavazi ya ukuhani watakayoyavaa wakati wa kuhudumu. Tena akaamuru kwamba wote walioulinda mji wapewe makonde na mshahara. Tena vyombo vyote vya Hekalu vilivyochukuliwa Babeli na mfalme Kiro sasa virudishwe vyote kule Yerusalemu tena.

VI

Hapo yule kijana, yaani Zerubabeli, akauinua uso wake mbinguni, akamhimidi Mfalme wa Mbinguni, akasema: "Ndio kwako Wewe hutoka ushindi, hekima na ukweli. Utukufu una Wewe, nami ni mtumwa wako. Umehimidiwa Wewe uliyenipa hekima, nami nakushukuru Wewe, Mungu wa baba zetu." Hivyo Zerubabeli, aliyekuwa mshindi katika mashindano kati ya vijana hao watatu, hakujitafutia heshima na utajiri kwake mwenyewe, lakini alikumbuka akina watu wake waliokuwa utumwani, na aliwaombea uhuru kwa mfalme Dario. Alipofaulu kwa kuwapatia uhuru na kupata msaada kuujenga upya mji wa Yerusalemu pamoja na Hekalu, alifurahi sana na kumshukuru Mungu katika hayo yote.

LESSON 81-b



Step 1
Hatua ya 1 Drills on the Causative Verb Form

1. Repetition and substitution drills

a. Niamshe saa kumi na mbili asubuhi.
O7OO hrs., O745 hrs., O815 hrs.

b. Mwalimu anawasomesha watoto wake.
fundisha, chezesha

c. Daktari aliwaponya wagonjwa.
lalisha, ketisha

d. Mwuzaji atapunguza bei ya viatu.
pandisha, badilisha

e. Amemfurahisha rafiki kwa maua.
pendeza, changamsha

f. Mlinzi hodari aliwastusha wevi.
kamata, umiza

g. Kapteni aliamuru askari waingize mabeti kibandani.
bunduki, blanketi

h. Angalieni! Msiwaumize watoto mkicheza mpira.
angusha, sahau

2. Pattern response drills

a. Unajua kuendesha motokaa?
Ndio ninajua kuendesha motokaa.

b. Ndege ngapi zilikuja kuangusha mabomu?
Ndege tano zilikuja kuangusha mabomu.

c. Ulimi unatuwezesha kuonja?
Ndio, unatuwezesha kutamka maneno pia.

d. Utarudisha kitabu lini?
Nitakirudisha kesho.

e. Pombe itawalewesha watu wale?
Ndio itawalewesha.

f. Ungeweza kunikopesha pesa?
Ndio nitakukopesha sh. 100/-.

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework: Preparation of the story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the Morning) LESSON 81

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 81

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 81

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 81

1. Comprehension drills - These will be read orally, or on tape, and the student's comprehension will be checked.

   a. Alitaka kujilaza chini, lakini hathubutu.

   b. Bwana Chui alikoroma, "Kula majani, Bwana Mbuzi, ukiisha kushibisha tumbo lako vema, nitakula wewe."

   c. Alijiepusha taratibu kama alivyoweza, na akakimbia kwa kasi sana.

   d. Habari hii inanitatanisha sana, wala siwezi kuelewa nayo.

   e. Watu wale walimlisha mamba huyo kwa muda mrefu, hata akawazoea sana akawa rafiki mkubwa wa watu.

   f. Mwenye kiti alipaaza sauti yake ili wote wapate kusikia.

   g. Matunda hayo yalimburudisha sana.

   h. Rafiki yake alimkaribisha vizuri, akamwandalia wali na nyama, akamtengenezea kahawa na kila kitu cha kumburudisha.

   i. Ni nani wanaowatawala hata wafalme, naam, na kuwatiisha? Je! si wanawake?

   j. Nakusihi uitumize nadhiri ile uliyoitoa kwa kinywa chako mwenyewe.

   k. Hivyo akazitwaa zile barua, akaondoka, akauendea Babeli, akawapasha habari ndugu zake wote. Nao wakafanya karamu ya furaha, kwa vinanda na kwa changamko siku saba.

2. Following the comprehension drill, the instructor will then give the English of the above sentences and the student will give the Swahili equivalent.

6TH PERIOD LESSON 81

KIPINDI CHA 6 SOMO LA 81

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

1. The Causative Verb Form (-SHA, or -ZA)

The causative form expresses the concept or idea of compulsion. In simple words: someone or something was caused, compelled, or made to do something.

e.g. Alisimamisha kiti = He caused the chair to stand up.

Sasa kiti kinasimama = Now the chair is standing.

2. The causative suffixes are -SHA or -ZA. There is a rough rule to guide us as to when to use one or the other of these suffixes, and that is this: Use -SHA in all normal cases where the verb ends in one vowel, and use -ZA when the verb ends in 2 or more vowels. Now let us look at the first rule, where the ending is -SHA, and where the phonetic link I or E is used according to rules explained earlier:-

e.g. lala > lalisha = cause or make to lie down

pita > pitisha = cause to pass

funga > fungisha = cause to fasten

cheza > chezesha = cause to play

soma > somesha = cause to read

3. The student has learned that when there are 2 or more vowels at the end of a verb, then normally the phonetic link would be LI or LE. But the causative is irregular in this respect and omits the link completely in such instances, and the causative ending -SHA now becomes -ZA in 98% of such cases, and we get:-

e.g. kimbia > kimbiza = make to run

potea > poteza = cause to get lost, lose

pungua	>	punguza	= make less, decrease
jaa	>	jaza	= make full, fill
ingia	>	ingiza	= put inside
kataa	>	kataza	= forbid
zoea	>	zoeza	= get used to, practice
oa	>	oza	= cause to marry
umia	>	umiza	= cause to get hurt
legea	>	legeza	= to loosen

Some of the common exceptions to this rule are:

zaa	>	zalisha	= cause to bear, act as midwife
jua	>	julisha	= inform
sahau	>	sahaulisha	= make one forget
kaa	>	kalisha	= make one stay

4. Make note of the following irregular forms which also omit the phonetic link:

amka	>	amsha	= awaken
anguka	>	angusha	= cause to drop, drop
chemka	>	chemsha	= cause to boil
waka	>	washa	= to light, turn on a light
vuka	>	vusha	= make to cross over
ruka	>	rusha	= make fly

ogopa	>	ogofya	=	frighten, make afraid
pona	>	ponya	=	heal, make well
ona	>	onya	=	warn

5. Verbs ending in 'i' do not take a link and just add the causative ending, usually -SHA.

keti	>	ketisha	=	make sit, to seat
rudi	>	rudisha	=	give back, return
tii	>	tiisha	=	make to obey
zidi	>	zidisha	=	to make more, increase
furahi	>	furahisha	=	to make glad

6. Some adjectives can be drawn into a verbal construction by use of the causative, and so we get:

safi (clean)	>	safisha	=	make clean
fupi (short)	>	fupisha	=	to shorten
tajiri (rich)	>	tajirisha	=	make rich
tayari (ready)	>	tayarisha	=	make ready
sahihi (correct)	>	sahihisha	=	to correct
rahisi (cheap, easy)	>	rahisisha	=	to make easy, simplify
imara (strong)	>	imarisha	=	make firm or strong
sawa (equal)	>	sawazisha	=	make equal, level
refu (long)	>	refusha	=	lengthen

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 82

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The reciprocal verb form ending with ANA.

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from the book, "King Solomon's Mines" by H. Rider Haggard Part 1

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

almasi	(diamond)
anasa	(luxury)
ana wazimu	(he is mad)
dhaifu	(weak)
dharau	(despise, scorn)
gofu (ma)	(ruins)
hadithia	(narrate)
haidhuru	(never mind)
kabila (ma)	(tribe)
kulungu	(species of antelope)
maboromoko	(usually maporomoko ya maji = waterfalls)
mapokeo	(things received, often in the sense of traditions and customs.)
mchawi	(witch, sorcerer)
mnyonge	(a low, wretched person)
Mreno	(a Portuguese)
mtaa	(district, quarter, division of a town.)
ndovu	(elephant)
pofu	(eland)
suriama (ma)	(a half-caste)
ukoo	(relationship, descent, ancestry)

c. Lexical items continued

upande wa pili	(the other side)
zikwa	(to be buried)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 82

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 82

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on the Reciprocal Verb Form

   a. Unamjua Ali?
      Ndio, tunajuana.

   b. Juma anapenda ndugu yake?
      Ndio wanapendana.

   c. Mwalimu anasaidia mwanafunzi.
      Mwanafunzi anasaidia mwalimu.
      Wanasaidiana.

   d. Kilonzo anafanana na Juma.
      Juma na Kilonzo wanafanana.

   e. Njiani nilikutana na watu wawili.
      Watu hao walifuatana nami.

2. Drills using new expressions.

   a. Mapokeo
      Habari za mapokeo
      Habari za mapokeo na desturi

   b. Wazimu
      Ana wazimu
      Mtu yule ana wazimu

c. Haidhuru
Sina pesa, lakini haidhuru.

d. Maporomoko ya maji
Maporomoko ya maji ya mto Zambezi

e. Anasa za dunia
Watu wasiotamani anasa za dunia

f. Mashimo ya dhahabu
Mashimo ya almasi
Mashimo ya shaba nyekundu
Mashimo ya madini

g. Umepata kusikia habari?
Sijapata kusikia.

h. gofu - magofu
Magofu ya mji wa zamani
Alivumbua magofu ya mji wa zamani.

Mateuzi Kutoka
"Mashimo ya Mfalme Sulemani"
Kimetungwa na H. Rider Haggard

Sehemu ya Kwanza

I

Basi nikaanza kutoa hadithi yangu, "Kwa kawaida mwajua kuwa wawindaji ndovu ni watu wasiotamani anasa za dunia, wala hawashughuliki katika mambo ila yale yaliyo ya kweli ya dunia, wala desturi na mazoea ya watu weusi. Lakini pengine mwaweza kuonana na mtu mmoja mmoja anayejitia katika mambo ya kuandika habari za desturi na mapokeo na hadithi za watu weusi, na kujaribu kutunga habari zao za zamani za kale. Mtu aliyeniambia maneno haya alikuwa mmoja wa namna hiyo, na sasa tangu aliponiambia maneno haya yapata miaka thelathini iliyopita.

II

Ilikuwa hivi: katika safari yangu ya kwanza nilikwenda kuwinda ndovu katika nchi ya Matabele. Mtu mmoja jina lake aliitwa Evans ndiye aliyeniambia maneno hayo, naye masikini aliuawa na nyati kwa mwaka wa pili yake, akazikwa mahali palipokuwa karibu na maboromoko ya maji ya mto Zambezi. Nami namkumbuka sana kuwa siku moja nilikuwa nikimzungumza habari za kulungu na pofu katika mtaa moja wa Transvaal!

III

Evans akasema, "Ndiyo, lakini mimi nitakutolea hadithi iliyo ya ajabu sana kupita habari za nyama." Akaendelea kuhadithia jinsi alivyopata kuvumbua magofu ya mji wa zamani sana ambao alisadiki kuwa ni mji ule uliokuwa ukiitwa "Ophir" uliotajwa katika Agano la Kale, na tangu siku ile, watu wengi wenye maarifa kuliko marehemu Evans wamesema vile vile. Mimi nikakaa kusikiliza na masikio mawili, maana wakati ule mimi nilikuwa bado kijana, na hadithi zile za kale zilinipendeza sana, na mara akasema "Je, mwanangu, umepata kusikia habari za milima ya Sulemani iliyo kaskazini mwa nchi ya Mashukulumbwe?" Nikamwambia "Sijapata kusikia." Akasema, "Basi, haidhuru haidhuru, kwani hapa ndipo Sulemani alipokuwa na mashimo yake, yaani mashimo ya almasi."

LESSON 82-a



IV

Nikamwuliza "Je, wewe unayajuaje?" Akajibu, "Nayajuaje! Nayajua kwa jina lake lilivyo, na tena niliambiwa na mwanamke mmoja mchawi wa kabila la Isanusi katika nchi ya Manika. Alisema kwamba watu wanaokaa upande wa pili wa milima ile ni ukoo wa Amazulu, wanasema lugha inayofanana na Kizulu, ila wao ni wakubwa, kisha wazuri zaidi ya Amazulu. Lakini kuna wachawi wenye nguvu nyingi wanaokaa humo waliojifunza uchawi wao kwa watu weupe wakati "dunia ilipokuwa giza tupu," tena walikuwa na siri ya shimo la ajabu lenye mawe yale yanayong'aa."

V

Wakati ule nilicheka sana niliposikia hadithi hii nikaidharau, lakini ilinipendeza sana, maana wakati ule mashimo ya almasi yalikuwa bado kuvumbuliwa. Lakini yule marehemu Evans aliuawa, nami nikakaa muda wa miaka ishirini, bila kufikiri jambo lo lote. Baada ya miaka ishirini, na huo ni muda mrefu sana, maana mwindaji ndovu ana shida kuishi miaka ishirini katika kazi yake, nikasikia habari zaidi juu ya milima ya Sulemani na nchi iliyo upande wa pili yake.

VI

Hapo mimi nilikuwa katika nchi ya Manika, kwa mahali paitwapo Kwa Sitanda, napo ni mahali pabaya sana, maana sikuweza kupata chakula wala nyama hakuna. Nilishikwa na homa kali mno hata hali yangu ikawa dhaifu sana, na siku moja akafika Mreno mmoja pamoja na mwenziwe mmoja msuriama. Tukaongea kidogo pamoja, maana yeye aliweza kusema Kiingereza kidogo, nami pia nilijua kusema Kireno kidogo, akaniambia kuwa jina lake ni Jose Silvestre, na tena ana shamba karibu na Delagoa Bay. Lakini siku ya pili yake aliondoka pamoja na mwenziwe, akasema "Kwa heri." Katika kule kusema "Kwa heri," akasema "Bwana, tukionana tena natumaini mimi nitakuwa tajiri kuliko watu wote duniani, nami nitakukumbuka." Nikacheka kidogo, maana nilikuwa mnyonge kwa homa na kwa hivyo sikuweza kucheka sana, nikamwona akienda kuvuka jangwa lile kwenda upande wa magharibi, nikadhani kuwa ana wazimu, au anakwenda kutafuta nini huko?

LESSON 82b

3RD PERIOD | PATTERN DRILLS | LESSON 82

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 82

Step 1
Hatua ya 1 Drills on the Reciprocal Verb Form

1. Repetition drills

a. Watu wengi wamesongana sokoni.
barabarani, kanisani, skulini

b. Hamisi alifuatana na ndugu yake.
mwenzake, askari

c. Mimi sipatani na mtu yule.
sisi, wao

d. Sokoni nilikutana na watu watatu.
rafiki, mmoja, mwalimu

e. Karani na mke wake hugombana sikuzote.
saidiana, patana

f. Yawapasa mtu na mwenzake kusameheana.
achiliana, saidiana

g. Watoto walisalimiana leo asubuhi.
sisi, ninyi

h. Msigombane watoto, mpendane.

pigana, bishana

2. Completion drills

Give the reciprocal form of the verb in the vacant space. This drill may be written or oral, at the instructor's discretion.

a. Ambia:-
Jana sisi _____habari zote.

b. Shiriki:-
Heri wanafunzi _____katika mambo yote.

c. Piga:-
Mwezi uliopita askari wetu _____na adui.

d. Acha - Sikiliza
Labda watu wale _____bado kidogo kwa sababu____.

e. Saidia:-
Lazima wanadamu_____.

f. Kubali:-
Jana wanachama _____katika mashauri yote.

g. ona:-
_____ jana lakini hakuniambia hata neno moja.

h. Kuta:-
Sisi kesho _____na rafiki zetu sokoni.

3RD PERIOD | PATTERN DRILLS | LESSON 82

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 82

i. Andika:-
Rafiki yangu na mimi_____kila mwaka.

j. Wezekana:-
Tulikuwa na mipango ya kwenda Afrika ya Mashariki lakini_____sasa.

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework: Preparation of the story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the morning) LESSON 82

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 82

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 82

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 82

1. Comprehension drills - These will be read orally, or on tape, and the student's comprehension will be checked.

   a. Hivyo ndivyo marafiki wawezavyo kusaidiana.

   b. Alitazama kila pembe apate kuona kama kuna msaada wo wote wa kupatikana.

   c. Iwapo mamba kaletewa asichokitokea jasho, bila shaka hufurahi, maana atakapo samaki hana budi kutoka jasho akifukuzana nao.

   d. Wanadamu kwa wanadamu hawana budi kusaidiana.

   e. Alitangaza kwamba ikipatikana habari yo yote inayomhusu mwanawe aliyepotea, basi itatolewa zawadi kwa yeye atakayemwarifu.

   f. Pengine mwaweza kuonana na mtu mmoja mmoja anayejitia katika mambo ya kuandika habari za desturi na mapokeo na hadithi za watu weusi.

   g. Wakati ule mimi nilikuwa bado kijana, na hadithi za kale zilinipendeza sana.

   h. Wakati ule mashimo ya almasi yalikuwa bado kuvumbuliwa.

   i. Nilishikwa na homa kali mno hata hali yangu ikawa dhaifu sana.

   j. Kila mtu aandike aonavyo, ni kitu gani kilicho na nguvu hasa.

2. Following the comprehension drill, the instructor will give the English of the above sentences and the student will give the Swahili equivalent.

6TH PERIOD LESSON 82

KIPINDI CHA 6 SOMO LA 82

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

1. The Reciprocal Verb Form:

   This form shows common or connected action, and the ending is -ANA

   e.g.

fuata	-	fuatana	-	follow each other
kuta	-	kutana	-	meet together
penda	-	pendana	-	love one another
piga	-	pigana	-	hit one other, i.e. fight
haribu	-	haribiana	-	destroy each other
sahau	-	sahauliana	-	forget each other

2. Notice that these verbs are followed by NA when an object is mentioned:

   e.g. Nilikutana na rafiki yangu njiani.
   I met (with) my friend on the way.

   Walipigana na adui.
   They fought (with) the enemy.

3. Note: The reciprocal form of the stative is often used to imply possibility:

   e.g. onekana from oneka, means - to be visible
   wezekana from wezeka, means - to be possible
   patikana from patika, means - to be procurable.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 83

VOLUME VI | BLUE PRINT | LESSON 83

KITABU CHA VI | SOMO LA 83

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The Verbal nouns, KU class.

b. The Negative Infinitive form.

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting — Series of scenes from the book, "King Solomon's Mines" by H. Rider Haggard Part 2

b. Cultural Note: — None

c. Lexical Items:

babaika	(be confused in one's speech, as a sick person in delirium)
dhoofu, dhoofika	(become weak, lose strength)
fifia	(to be dying away)
fisi	(hyena)
hati	(written document)
kaburi (ma)	(grave)
kanyaga	(tread on)
kianga (vi)	(ray of light)
kilele (vi)	(top, peak)
koba (ma) mkoba (mi)	(bag, pouch, wallet)
konda	(grow thin)
mrithi (wa)	(heir)
mtelemko (mi)	(downward slope)
nitakuwa na wasaa	(I shall have opportunity)
paja (ma)	(thigh)
pambazuka	(get light, dawn)
papasa	(grope about)
payuka	(talk nonsense, be delirious)
pepesuka	(totter)
telemka	(go down)
ugua	(groan)
vimba	(to swell)
wahi	(to be in time)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 83

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 83

Note: Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Auditory perception and comprehension

Step 2
Hatua ya 2 Oral production of minimum utterances

1. Drills on the Verbal Noun

   a. Kufaulu ni shabaha yake.
      Kuwa tajiri ni shabaha yake.

   b. Kuimba kuzuri kwa watoto
      Kuimba kwao kunatufurahisha.

   c. Kuandika ni kazi ya mwandishi.
      Kujifunza ni kazi ya wanafunzi.

2. Drills on the Negative Infinitive Form

   a. Kuimba - Kutoimba

   b. Kusoma kitabu - Kutosoma kitabu

   c. Kunaswa mtegoni- Kutonaswa mtegoni

   d. Kuwa mwalimu - Kutokuwa mwalimu

   e. Kufika upesi, kutofika upesi ni mamoja kwangu.

3. Drills using new expressions

   a. Magoti na mikono
      Alitambaa kwa magoti na mikono.

b. Kutelemka
Alitelemka mtelemko.
Adhuhuri nitatelemka mjini.

c. Kilele kirefu
Kilele kirefu katika milima

d. Hati
Nitakupa hati.
Mwishowe tutapata hati zetu.

e. Kianga cha kwanza
Kianga cha kwanza cha jua

f. Kulipopambazuka
Kulipopambazuka nikaamka.

g. Mtoto ni mrithi wa baba
Amerithi mali nyingi kwa baba.

2ND PERIOD SWAHILI NARRATIVE LESSON 83

KIPINDI CHA PILI SOMO LA 83

Mateuzi Kutoka
"Mashimo ya Mfalme Sulemani"
Kimetungwa na H. Rider Haggard

I

Baada ya kupita juma moja, nikawa nimepona, na jioni nilipokuwa nimekaa nje ya hema yangu ndogo, nikitafuna paja la kuku wa mwisho niliyemnunua kwa mtu mmoja kwa bei ya kitambaa kimoja cha thamani ya kuku ishirini, nikitazama jua jinsi lilivyokuwa jekundu linavyoshuka nyuma ya jangwa hilo, na mara nikaona kitu kama mzungu kimevaa koti kikitelemka mtelemko kwa mbele yangu yapata mwendo wa hatua mia sita. Kwanza kitu hicho kilitambaa kwa magoti na mikono, kisha kikasimama na kupepesukia mbele kwa hatua chache, tena kikaanguka na kutambaa. Mradi nikaona kuwa ni mtu aliye taabani.

II

Nikapeleka mmoja wa wawindaji wangu kwenda kumsaidia, na baadaye kidogo akaja naye, je, wadhani alikuwa nani? Alikuwa yule Jose Silvestre, au kwa kusema kweli, mifupa yake, kwa maana amekonda kabisa. Uso wake ulikuwa wa rangi ya kimanjano unang'aa kwa homa aliyokuwa nayo, na yale macho yake meusi makubwa yalikuwa kama yatamtokea utosini, maana alikuwa hana nyama kabisa. Ngozi yake ilikuwa imekauka, na nywele zake zimegeuka rangi zimekuwa nyeupe, na mifupa yake ilikuwa imetokeza mwilini. Akawa anaugua huku akisema, "Nipeni maji! kwa ajili ya Kristo maji!" Nikaona kuwa midomo yake imepasuka na ulimi uliomtoka ulikuwa mweusi, tena umevimba.

III

Nikampa maji yaliyochanganywa na maziwa kidogo akanywa sana bila ya kupumzika, nikamzuia kusudi asinywe zaidi. Na mara homa ilimshika tena akaanguka na kuanza kupayuka juu ya habari za milima ya Sulemani, na almasi na jangwa. Nikamchukua na kumweka hemani mwangu nikamtunza kama nilivyoweza; lakini nilijua kuwa atakufa. Kupata saa tano ya usiku akatulia kidogo, nami ndipo nilipopata usingizi kidogo, nikalala. Kulipopambazuka nikaamka, nikamwona namna alivyokuwa amekonda sana, amekaa na macho yake ameyakodoa kutazama jangwa. Baadaye kile kianga cha kwanza cha jua kilipoonekana mawinguni, kikaangaza jangwa mpaka kufika kilele kirefu katika milima ya Sulemani, mbali mwendo wa maili mia moja na zaidi.

LESSON 83-a

IV

Mara yule mgonjwa akanyosha mkono wake mwembamba kulekeza kileleni na huko akisema kwa Kireno, "Ndipo, ndipo papo hapo, lakini mimi sitawahi kupafikia kamwe. Wala hapana atakayepafikia kamwe!" Mara akakaa kimya kidogo kama mtu anayewaza shauri moyoni, halafu akanigeukia akasema, "Rafiki bado ungalipo? Ama sasa naona macho yangu yaingia giza." Nikajibu "Ndiyo, nipo papa hapa. Lakini sasa afadhali ulale upumzike." Akasema,"Ndiyo nitapumzika sasa hivi, na tena nitakuwa na wasaa mwingi wa kupumzika, ndiyo hata milele. Nisikilize, nisikilize, ninakufa! Wewe umenitendea mema. Nitakupa hati. Labda utaweza kupafikia ikiwa utaishi kuvuka jangwa, ambalo limemwua mtumishi wangu na mimi!"

V

Akapapasapapasa katika mfuko wake akatoa kitu nilichokidhania kuwa koba la kuwekea tumbako lililotengenezwa kwa ngozi ya nyama. Koba hilo lilifungwa kwa uzi wa ngozi naye alijaribu kulifungua asiweze. Akanipa akisema, "Fungua." Nikalifungua nikatoa kipande cha kitambaa kikuukuu cha katani kilichokuwa kimeandikwa maneno, na ndani ya kitambaa hicho mlikuwamo karatasi. Kisha akasema kwa sauti ya kufifia, maana alizidi kudhoofu, akanena, "Juu ya hiyo karatasi kumeandikwa yote yaliyoandikwa juu ya kitambaa na hivyo ilinibidi kufanya kazi ya miaka hata kuweza kuisoma. Sikiliza: Babu yangu aliyelazimishwa kutoka mji wa Lisbon ambaye alikuwa katika Wareno hao wa kwanza waliofika katika nchi hii, aliandika maneno hayo wakati alipokuwa akifa katika milima ile ambayo hapana hata mtu mweupe aliyepata kuikanyaga kwa miguu yake mpaka hivi leo. Jina lake aliitwa Jose da Silvestre, naye aliishi zamani za miaka mia tatu.

VI

Mtumishi wake aliyekuwa akimngojea kwa upande huu wa milima aliona kuwa amekwisha kufa, naye ndiye aliyeleta maandiko haya mpaka Delagoa. Na tokea wakati huo yametunzwa na warithi wake, lakini hapana aliyetaka kuyasoma, mpaka mimi nilipofaulu. Nami nimepoteza maisha yangu kwa ajili yake, lakini labda mwingine ataweza kufaulu na kuwa tajiri wa kupita wote duniani. Lakini usimpe mtu mwingine, bwana, wewe nenda mwenyewe!" Akaanza kubabaika tena, na baada ya saa moja akafa. Mungu na ampe raha, amstareheshe. Nilimzika katika kaburi la kwenda chini sana, nikaweka na mawe makubwa juu ili kusudi asifukuliwe na fisi. Kisha nikaondoka pale."

LESSON 83-b

3RD PERIOD | PATTERN DRILLS | LESSON 83

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 83

Step 1
Hatua ya 1 Drills on Verbal Nouns and Negative Infinitives

1. Repetition drills using Verbal Nouns.

   a. Kuimba kuzuri kunaleta furaha.

   b. Kusafiri kunatufurahisha sana.

   c. Kusoma kitabu kunafaa.

   d. Kuchimba mahandaki kunaleta jasho.

   e. Kufaa hakudhuru.

   f. Kuandika kwa mwanafunzi si kuzuri.

2. Written drill on the negative infinitive.

   a. Find all the infinitives in Sections XXII - XXIV of lesson 79. "Adhabu ya Mtu Asiyekuwa na Shukrani" and change these to the negative infinitive form.

      e.g. kuuawa kutouawa

Step 2
Hatua ya 2 After the drills there will be a 20 minute clab session during which the students will listen to the story.

Step 3
Hatua ya 3 Homework: Study of the story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the Morning) LESSON 83

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 83

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. The choice of these will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 83

KIPINDI CHA 5 | SOMO LA 83

1. Comprehension drills - These will be read orally, or on tape, and the student's comprehension will be checked.

   a. Nami nimepoteza maisha yangu kwa ajili yake, lakini labda mwingine ataweza kufaulu na kuwa tajiri wa kupita wote duniani.

   b. Wengi huwa na desturi ya kutoandika majina yao vizuri.

   c. Kufika upesi, kutofika upesi ni mamoja kwangu.

   d. Kuimba kwa watoto kulinifurahisha.

   e. Kusema ni kuzuri, na kutosema ni kuzuri pia.

   f. Basi hii ndiyo adhabu aliyopewa kwa kutokuwa na shukrani.

   g. Uso wake ulikuwa wa rangi ya kimanjano unang'aa kwa homa aliyokuwa nayo.

   h. Nywele zake zimegeuka rangi, zimekuwa nyeupe.

   i. Kulipopambazuka niliamka.

   j. Siku ya pili yake aliondoka akasema, "Kwa heri."

   k. Katika kule kusema "Kwa heri" akasema, "Bwana, tukionana tena natumaini mimi nitakuwa tajiri kuliko watu wote duniani."

   l. Mara homa ilimshika tena akaanguka na kuanza kupayuka juu ya habari za almasi na milima ya Sulemani.

2. Following the comprehension drill, the instructor will give the English of the above sentences and the student will give the Swahili equivalent.

6TH PERIOD LESSON 83

KIPINDI CHA 6 SOMO LA 83

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on tape.

1. The Verbal Noun - KU Class

   a. The infinitive form of the verb "KU", e.g. Kufanya, may be used as a verbal noun. Verbal nouns are usually translated by the English form -ing, and there is only one form, as there is no reference to singular or plural.

      e.g. Kuandika hadithi ni kazi.
      Writing stories is work.

      Kuimba ni kuzuri.
      Singing is good.

      Kuona ni kuamini.
      Seeing is believing.

   b. The concords for this class are shown in the following table:

Adjective Concord	Possessives	Demonstratives	Subject and Object Prefixes
Before consonant -Ku- Kuimba kuzuri Before vowel -Kw- Kuimba kwote	Kw- Kuimba kwetu Kuimba kwa watoto	Kule Huku	Ku Kuimba kumekwisha Unakusikia kuimba kwako

2. The Negative Infinitive Form. You have learned that the prefix Ku is the sign of the affirmative infinitive.

   e.g. Kufanya - to do
   The prefix Kuto is the sign of the negative infinitive.

Kutofanya - not to do

Kutofika - not to arrive

Kuwa ama kutokuwa hilo ndilo swali.
To be, or not to be, that is the question.

Note: Occasionally the forms Kutoafanya or kutokufanya may be seen, but they are rare and Kuto is the usual prefix.

SWAHILI BASIC COURSE

LESSON 84

1. LANGUAGE STRUCTURE

a. The Compound tenses

Refer to Generalization for explanation of structural features of this lesson.

2. CONTENT STRUCTURE

a. Situational Setting: Series of scenes from the book "King Solomon's Mines." Part 3

b. Cultural Note: None

c. Lexical Items:

dhahiri	(evident, plain)
fahari	(grandeur, glory)
fariji	(comfort, console)
kiriba (vi)	(animal skin water bag)
lamba (ku)	(lick)
mchanga	(sand)
mgongo (mi)	(backbone, ridge)
paa	(small gazelle)
pazia (ma)	(curtain, screen)
penya	(penetrate)
shani	(a wonder, rare occurrence)
shtuka	(be startled)
shuku	(to suspect)
tone la maji	(a drop of water)
toweka	(vanish, disappear)
ububu	(speechlessness)
upeo	(furthest point)
upeo wa macho	(as far as the eye can see)
upuzi	(nonsense)
wayo (pl. nyayo)	(footprint, tracks)

1ST PERIOD | PERCEPTION DRILLS | LESSON 84

KIPINDI CHA KWANZA | MAZOEZI | SOMO LA 84

Note: Refer to the Generalization for explanation of the structural features in this lesson.

Step 1
Hatua ya 1 Introduction to the Compound Tenses, explaining the 3 main groups of possible combinations:

1. Relationship: TIME-ASPECT
   Relationship: ASPECT-ASPECT
   Relationship: ASPECT-TIME

Step 2
Hatua ya 2

1. Drills using new expressions

   a. Tone la maji
      Hatuna hata tone la maji.

   b. Wayo - nyayo
      Nyayo za paa
      Nyayo za wanyama
      Nyayo za wanyama katika mchanga

   c. Upeo wa macho
      Jangwa tupu mpaka upeo wa macho
      Mchanga mpaka mwisho wa upeo wa macho
      Upeoni mwa macho, jangwa tu

   d. Jua likaangaza pote
      Jua likaangaza pote kwa fahari

   e. Jua likatufunulia shani.
      Shani iliyotusahaulisha kiu.
      Fahari na utukufu wa shani

KIPINDI CHA PILI SOMO LA 84

Mateuzi Kutoka
"Mashimo ya Mfalme Sulemani"
Kimetungwa na H. Rider Haggard

I

Mara tulipoamka kabisa tulianza kuzungumza juu ya shida yetu. Hapana hata tone la maji. Tulipindua viriba vyetu tukalamba kingoni, lakini wapi! kavu kabisa. Bwana Henry akasema, "Tusipopata maji tutakufa." Nikasema, "Kama ile ramani ya yule mzee ni sahihi, maji yapo karibu tulipo sasa." Lakini maneno yangu hayakumfariji mtu, maana ilikuwa dhahiri kuwa hatuwezi kutumaini sana ile ramani. Sasa ikaanza kuwa kweupe kidogo kidogo, tukakaa tunatazamana tu, nikamwona Ventvogel, yule Hottentot aliondoka akaanza kutembea macho yaelekea chini, na mara akafanya sauti kama ya kukoroma, akaonyesha chini katika mchanga. Tukashtuka tukasema, "Nini, nini?" Tukaondoka sote tukamwendea tukatazama chini. Akasema, "Wako nyama wengi kama paa hapa. Tazameni nyayo zao." Nikamwuliza, "Je, hata kama ni wengi hapa, ya nini?" Akajibu, "Paa hawatembei mbali na maji." Nikasema "Kweli, nilisahau, Alhamdulilahi."

II

Basi shauri hilo lilitutilia uzima upya tena; ni ajabu sana ya kuwa kama watu wamo katika shida, hushikilia sana tumaini hata kama ni dogo, na kufurahi. Maana, usiku wa giza nyota moja ni bora kama si nyota.

Huko nyuma Ventvogel alikuwa akiinua pua yake akinusa hewa ile yenye moto kama anavyonusa paa mzee anayeshuku hatari. Mara akasema, "Naona harufu ya maji." Ndipo tulipozidi kufurahi, maana tulifahamu namna watu wanaozoea kukaa porini wanavyoweza kutumia fahamu zao kwa jinsi ya ajabu.

Mara ile jua likatoka likaangaza pote kwa fahari likatufunulia shani iliyotusahaulisha kwa muda ile kiu kali iliyotusumbua.

III

Pale kwa mbele yetu kadiri ya maili arobaini au hamsini tuliona vilele vya milima viitwavyo "Maziwa ya Sheba" viking'aa kama fedha katika mishale ya jua ya asubuhi, na kila upande kwa upeo wa maili mia nyingi mlima wa Sulemani ulienea. Hapo nilipo sasa siwezi kueleza fahari na utukufu wa shani ile ya ajabu, maana maneno yanipotea kabisa. Hata kuikumbuka hunitia ububu. Mbele yetu tuliona milima mirefu sana nafasi ya kati kati ya milima ilikuwa kama mwendo wa maili kumi na mbili, nayo iliunganishwa pamoja kwa mlima mrefu mfupi kama mgongo.

LESSON 84-a

IV

Kwa muda mdogo mishale ya jua ikacheza juu ya theluji na ukungu uliokuwa chini, na mara mawingu na ukungu ukazidi kuwa kama pazia kubwa yakatufichia milima mpaka tukaweza kuona alama tu ya milima ikitokeza katika pazia ya mawingu. Mara ile maziwa ya Sheba yalipotoweka, tukakumbuka tena kiu na taabu yetu.

Ni kweli ya kuwa Ventvogel alisema anaona harufu ya maji, lakini kila mahali tulipotazama hatukuona hata dalili ya maji. Pote pote tuliona mchanga mkavu na majani yale ya jangwa hata mpaka mwisho wa upeo wa macho.

V

Tulitembea tukazunguka kilima tukitafuta kila upande, lakini hatukuona dalili ya ziwa wala kisima, wala chemchemi. Nikasema, "Wewe Ventvogel, wewe ni mpumbafu kabisa, hapana maji hata kidogo." Lakini yeye alizidi kuinua pua na kunusa hewani akasema, "Bwana, naweza kuona harufu ya maji. Najua maji yapo."

Bwana Henry akapapasa ndevu zake akifikiri, akasema, "Labda maji yako juu ya kilima." Bwana Good akasema, "Upuzi, nani aliyesikia habari za maji kuwako juu ya kilima!" Nikasema, "Haya twende tukatazame." Tukaondoka tukapanda kilimani na Umbopa akatangulia. Mara alisimama kama amepagaa akaita, "Maji! Maji! Maji!"

VI

Tulikwenda kwa haraka na hakika na hakika, tuliona maji yako katika shimo. Namna yalivyokuwa katika mahali pale hatukungojea kuulizana, wala hatukusita kwa sababu yalikuwa meusi. Mara tukaruka tukaanza kunywa. Lo! jinsi tulivyokunywa! Tulipokwisha kunywa, tukavua nguo zetu tukakaa kitako katika yale maji ili yapenyeze ngozi zetu zilizokuwa zimekauka kabisa.

Baadaye kidogo tuliondoka tumekwisha burudika, tukala nyama kavu, maana kwa muda wa saa ishirini na nne tulishindwa kula, tukashiba. Kisha tulivuta tumbako tukalala mpaka saa sita kando ya maji yale yaliyotuponya.

LESSON 84-b

3RD PERIOD | PATTERN DRILL I | LESSON 84

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 84

Step 1
Hatua ya 1

1. Drills on the TIME - ASPECT Relationship of Compound Tenses.

   a. No specific time context: - "KI"

      (1) Nilikuwa nikisoma kitabu na Mama alikuwa akishona.
      I was reading a book and Mama was sewing.

      (2) Nitakuwa nikisoma kitabu, na Mama atakuwa akishona.
      I shall be reading a book and Mama will be sewing.

      (3) Ninakuwa nikisoma kitabu, na Mama anakuwa akishona.
      I am in the process of reading a book, and Mama is in the process of sewing.

   b. Specific time context - at that very moment: "NA"

      (1) Alipokuwa anasema, wakati huo huo wageni waliingia.
      While he was speaking, at that very moment the visitors came in.

      (2) Mama na mimi tulikuwa tunasoma, na mara mtoto alilia sana.
      Mama and I were reading and suddenly the child cried out.

   c. Resulting state: "ME"

      (1) Tutakuwa tumekaa katika nyumba yetu mpya muda wa mwaka mmoja.
      We shall have lived in our new house for a period of one year.

(2) Alikuwa amechoka na kazi.
He had become tired of the work.

2. Drills on the ASPECT - ASPECT Relationship of Compound Tenses:

a. -Me- in the auxiliary verb.

(1) Matunda haya yamekuwa hayaliki.
This fruit has become inedible.

b. -Ka- in the auxiliary verb.

(1) Mtoto anasoma kitabu.
The child is reading a book.

(2) Mtoto akawa anasoma kitabu.
And the child began to read a book.
"Ka-Na" have the meaning of "began".

(3) Mtoto akawa akisoma kitabu.
And the child continued reading the book.
"Ka-Ki" have sense of continuation.

(4) Mtoto akawa amesoma kitabu.
And the child finished reading the book.
"Ka-Me" have sense of completion.

c. -Hu- in auxiliary verb. Sense of "Usually"

(1) Saa hiyo askari huwa wanapiga mizinga.
At that hour the soldiers usually fire.

(2) Toka saa 2 mpaka saa 4 askari huwa wakipiga mizinga.
From 8 - 10 o'clock the soldiers usually continue with the firing.

(3) Saa 4 askari huwa wamepiga mizinga.
At 10 o'clock the soldiers usually have completed the firing.

d. -Ki- in the auxiliary verb.

(1) Wanafunzi wakiwa wakiondoka, waambie waningojee.
If the students are in the process of leaving, tell them to wait for me.

(2) Wanafunzi wakiwa wameondoka, usiwafuate.
If the students have already left, do not follow them.

e. -Ngali in the auxiliary verb.

(1) Wafanyi kazi wangalifanya kazi sana, wangalichoka.
If the workers would have worked hard, they would have been tired.

(2) Watu wangalikuwa wakifanya kazi sana, hawangalichoka mno.
If the people had been used to working hard, they would not have been so tired.

f. -nga in the auxiliary verb.

(1) Ingawa watu wamezoea kazi, kazi nzito hii imewachosha.
Even though the people are used to work, this hard work has tired them.

g. -Japo- in the auxiliary verb.

(1) Ijapokuwa analia, ni lazima aende.
In spite of the fact that he is crying, he must go.

3RD PERIOD | PATTERN DRILL I | LESSON 84

KIPINDI CHA 3 | MAZOEZI | SOMO LA 84

Step 2
Hatua ya 2 Homework: - Study of the story for retelling.

4TH PERIOD (First hour in the Morning) LESSON 84

KIPINDI CHA 4 SOMO LA 84

Step 1
Hatua ya 1 Recitation of the story.

Step 2
Hatua ya 2 Any idioms or special expressions arising out of the story will be discussed and practiced. These will depend upon the general ability of the particular class.

5TH PERIOD | RECOMBINATION DRILLS | LESSON 84

KIPINDI CHA 5 | MAZOEZI | SOMO LA 84

Step 1
Hatua ya 1 Continuation of drills on Compound Tenses

3. Drills on the ASPECT - TIME Relationship in Compound Tenses

a. -Ki- in the auxiliary verb.

(1) Ikiwa shamba lilitunzwa litaleta faida kubwa.
If it be that the field was cared for, it will bring much profit.

(2) Kila shamba huleta faida likiwa hutunzwa sana.
Every field that is habitually cared for brings profit.

b. -Nga- in the auxiliary verb.

(1) Shamba halikuleta faida ingawa lilitunzwa sana.
The field did not yield a profit even though it was cared for.

c. -Japo- in the auxiliary verb.

(1) Ijapokuwa utachelewa tutakupokea.
Even though you will be late, we shall receive you.

(2) Ijapokuwa hukufanya vizuri, tutakupa mshahara wako.
Even though you did not do well, we shall give you your pay.

4. Drills using other auxiliary verbs.

a. Kwisha - (Already)

(1) Amekwisha kuja - He has already arrived.

Note: Usually now this is shortened to Amesha kuja.
The "ku" is retained with one-syllable verbs and with "Kwenda", but is omitted with other verbs.

e.g. Amesha sema - He has already said.
Amesha kwenda - He has already gone.

(2) Alikuwa amekwisha kwenda, or Alikuwa amesha kwenda.
He had already gone.

(3) Alipokwisha sema, akaenda zake.
When he had spoken, he went off.

b. Ngali - (still)

(1) Angali akifanya kazi. - He is still working.

(2) Alipokuwa angali mbali, baba yake akamwona.
While he was still a long way off, his father saw him.

c. Kwenda - (now)

(1) Maji yamekwenda kuletwa.
The water is just now being brought.

(2) Hamisi amekwenda kuitwa.
Hamisi is now being called.

d. Kuja -

(1) Hamisi amekuja kuwa mtu maarufu.
Hamisi has come to be an important person.

6TH PERIOD

KIPINDI CHA 6

LESSON 84

SOMO LA 84

This period will be devoted to short comprehension exercises based on taped material.

Comprehension will be checked by means of True - False statements or Multiple Choice answers. In some cases the students will be asked to give the English equivalent of what was said on the tape.

1. Compound Tenses:

Supplementary tenses may be formed by using parts of Kuwa, to be, with parts of other verbs:-

e.g.	Nimekuwa nikienda	- I have been going.
	Nilikuwa nikienda	- I was (in the act of) going.
	Nilikuwa nimekwenda	- I had gone.
	Nilikuwa nimekwisha kwenda.	- I had already gone.
	Nitakuwa nikienda	- I shall be (in the act of) going.
	Nitakuwa nimekwisha kwenda.	- I shall have already gone.

2. To form the negative of compound tenses:

a. When the main verb is in the ME or KI tense, then the auxiliary (kuwa) takes the negative prefixes.

e.g.	Sikuwa nikienda	- I was not going.
	Sikuwa nimekwenda	- I had not gone.
	Sitakuwa nimekwenda	- I shall not have gone.

b. When the main verb is in the present (NA tense), then the auxiliary is not affected but the main verb takes on the negative construction.

e.g.	Nilikuwa sisomi	- I was not reading.
	Tutakuwa hatusomi	- I shall not be reading.

3. You will notice that in some of the examples the verb Kwisha is used as an auxiliary. It conveys the meaning that something has not merely been done, but that it is already done and finished with:

e.g. Amekwisha kula - He has already finished eating.
Wamekwisha fika - They have already arrived.

(Usually in modern speech this is shortened to "sha")

e.g. Amesha sema - He has already said.
Amesha kwenda - He has already gone.

"Ku" is retained with one-syllable verbs, and with "Kwenda", but is omitted with other verbs.

4. These compound tenses may be used with any class in the normal way:-

e.g. Ukichelewa tena, gari litakuwa limekwenda.
If you delay any longer, the car will have gone.

5. Notice the following idiomatic expressions using compound Tenses:-

Alikuwa si ndani - He was not inside.
Walikuwa hawajui - They were not knowing, they did not know.
Nitakuwa siendi - I shall not be going.
Alimkuta hayuko - He found he was not there.

Note: The following pages give a detailed summary of all of the possible uses of the compound tenses. It is intended for students who wish to go on to further study. The 3rd and 5th Period drills are based on this outline.

However, for the present course the preceding generalization gives the necessary points on compound tenses and lists the forms most commonly used.

SOME NOTES ON COMPOUND TENSES

1. It is not always possible to express an idea concerning an action with the simple tenses learned so far. Thus in addition to indicating the time of an action it may be necessary also to indicate the circumstance.

   e.g. Mwalimu alipoingia darasani wanafuuzi walikuwa wakisoma.

   "Walikuwa" is an auxiliary verb expressing the time of the action.

   "Wakisoma" describes the circumstance and the action which took place at that time.

2. An auxiliary verb accompanies the main verb, and these make it possible to indicate more clearly the circumstance of the action.

   Of particular importance as auxiliary verbs are:-

   "kuwa", "kwenda", "kwisha", "kuja" and "ngali".

3. We call these particular circumstances or conditions of the action an aspect.

Specific time of action	expressed by	na
Continued action	expressed by	ki
Completed action with a resulting state.	expressed by	me
Sequence of action	expressed by	ka
Customary action	expressed by	hu
Conditional action	expressed by	nge, ngali si, sipo
Sense of Concession	expressed by	nga, japo

4. The tense prefixes as a rule are limited to:

Present time span	na
Past time span	li
Future time span	ta
Indefinite time	hu

5. We will differentiate now the three groups of possible combinations. These are:-

   a. Relationship: TIME - ASPECT

      The auxiliary verb carries the tense prefix, and the main verb the aspect prefix.

      e.g. Alikuwa akinywa chai.
      He was drinking tea just then.

   b. Relationship: ASPECT - ASPECT

      Both the auxiliary and the main verb carry the aspect prefix.

      e.g. Akiwa amelala usimwamshe.
      If he is asleep don't wake him up.

   c. Relationship: ASPECT - TIME

      In this case the auxiliary verb carries the aspect prefix and the main verb the time-tense prefix.

      e.g. Ikiwa hatutapata chakula tutaumia njaa.
      If (it should be) we don't get food we'll starve.

6. A word of Caution: These compound forms in Swahili express fine points and shades of meaning for which we may not find the exact equivalent in English. The student has to acquire a feel for these forms which comes through extensive use of the language and much reading.

A. Relationship: TIME - ASPECT

Main Verb ---> -na-			-ki-		-me-	
Auxiliary	ninakuwa	ninasoma	ninakuwa	nikisoma	ninakuwa	nimesoma
	tunakuwa	tunasoma	tunakuwa	tukisoma	tunakuwa	tumesoma
-na-	ninakuwa	sisomi	-	-	-	-
	tunakuwa	hatusomi	-	-	-	-
	nilikuwa	ninasoma	nilikuwa	nikisoma	nilikuwa	nimesoma
	tulikuwa	tunasoma	tulikuwa	tukisoma	tulikuwa	tumesoma
-li-	nilikuwa	sisomi	sikuwa	tukisoma	sikuwa	nimesoma
	tulikuwa	hatusomi	hatutakuwa	tukisoma	hatukuwa	tumesoma
	nitakuwa	ninasoma	nitakuwa	nikisoma	nitakuwa	nimesoma
	tutakuwa	tunasoma	tutakuwa	tukisoma	tutakuwa	tumesoma
-ta-	nitakuwa	sisomi	sitakuwa	nikisoma	sitakuwa	nimesoma
	tutakuwa	hatusomi	hatutakuwa	tukisoma	hatutakuwa	tumesoma

B. Relationship: ASPECT - ASPECT

Main Verb ---->	-na-		-ki-		-me-	
Auxiliary -me-	-	-	amekuwa	akilia	-	-
	amekuwa	halii	-	-	-	-
-ka-	akawa	analia	akawa	akilia	akawa	amelia
	akawa	halii	-	-	-	-
-hu-	huwa	analia	huwa	akilia	huwa	amelia
	huwa	halii	-	-	-	-
-ki-	akiwa	analia	akiwa	akilia	akiwa	amelia
	akiwa	halii	asipokuwa	akilia	akiwa	hakulia
-nge-	angekuwa	analia	angekuwa	akilia	angekuwa	amelia
	angekuwa	halii	asingekuwa	akilia	asingekuwa	amelia
-ngali-	angalikuwa	analia	angalikuwa	akilia	angalikuwa	amelia
	angalikuwa	halii	asingalikuwa	akilia	asingalikuwa	amelia
-nga-	angawa	analia	angawa	akilia	angawa	amelia
	angawa	halii	-	-	angawa	hakulia
-japo-	ajapokuwa	analia	ajapokuwa	akilia	ajapokuwa	amelia
	ajapokuwa	halii	-	-	ajapokuwa	hakulia

C. Relationship: ASPECT - TIME

Main Verb ---->	-li-		-ta-		-hu-	
Auxiliary -ki-	ukiwa	ulifika	ukiwa	utafika	ukiwa	hufika
	ukiwa	hukufika	-	-	-	-
-nge-	-	-	-	-	-	-
	ungekuwa	hukufika	-	-	-	-
-nga-	ungawa	ulifika	-	-	-	-
	ungawa	hukufika	-	-	-	-
-japo-	ujapokuwa	ulifika	ujapokuwa	utafika	-	-
	ujapokuwa	hukufika	-	-	-	-

A

adhabu (78) - punishment
afadhali (74) - rather, preferably
ahimidiwe Mungu (81) God be praised
aidha (81) - further, moreover
akida (81) - leader, commander
ajali (76) - accident, also fate, destiny, appointed end
akina (77) - generalized plural - tribe, family, etc.
Alhamdulilahi (76) - Allah be praised
almasi (82) - diamond
ambatana (80) - cling together
ana wazimu (82) - he is mad
anasa (82) - luxury
andalia (78) - prepare for
angamia (80) - be destroyed, perish
asi (77) - to rebel

B

baadhi ya (77) - some of
babaika (83) - be confused in one's speech, as a sick person in delirium
badala ya (77) - in place of, instead of
banwa (79) - be squeezed
baradhuli (73) - simpleton, dupe
baridi kali (72) - frosty, fierce cold
bembeleza (80) - coax, soothe
-bichi (75) - unripe, green
binadamu (77) human beings
bure (73) - alive
busu (81) - kiss

C

changamko (80) - entertainment amusement
changarawe (77) - grit, small stones, fine gravel
chinja (76) - butcher, kill
chui (76) - leopard
chura (75) - frog

D

daima (78) - permanently
daka (77) - seize
dalili (80) - sign, token
deni (80) - debt
dhabihu (81) - sacrifice
dhahiri (84) - evident, plain
dhaifu (82) - weak
dharau (82) despise, scorn
dhiki (78) - distress)
dhoofu (83) - become weak, lose strength
dhoruba (72) - storm
dini (74) - religion, creed
dhuru (76) - hurt, harm
diwani (81) - councillors

E

elekea (81) - point or face toward
elewa (76) - comprehend
enzi (80) - power
epuka (75) - avoid, separate from

F

fadhili (76) - kindness, favor
fahari (84) - grandeur, glory
farasi (78) - horse
fariji (84) - comfort, console
fariki dunia (79) - die, depart this life
fifia (83) - to be dying away

fisi (83) - hyena
fukua (74) - to dig out
funika (74) - to cover
furika (72) - flow over, flood

G

gofu (82) - ruins
gusa (79) - to touch

H

hadithia (82) - narrate
hai (73) - alive
  uhai (73) - life
haidhuru (82) - never mind
hali ya hewa (72) - weather
hasha (76) - certainly not
hasira (76) - anger
hatamu (80) - bridle
hati (83) - written document
hatuna budi (73) - we must - we have no alternative
hekaheka (79) - confusion, much noise
hekalu (81) - temple
hekima (73) - wisdom
hudhurungi (71) - brown
hukumiwa (77) - be judged, sentenced
hurumia (76) - have pity or mercy
husu (79) - to concern, apply to
hutubu (71) - give a speech
huzuni (80) - grief

I

imara (72) - strong

J

jamani (73) - as an address: you folks
jasho (77) - sweat, perspiration
jiepusha (75) - keep oneself from
jilaza (75) - lay oneself down
jimbo (80) - district, province, state
jongea (77) - make a move, either approaching or going away
jua kali (72) - hot and sunny
jua kali leo (72) - a hot sunny day today

K

kaa kimya (71) - keep quiet or still
kaa raha mstarehe (74) - to live in perfect comfort and peace
kabila (77) tribe
kaburi (83) - grave,tomb
kadhalika (80) - in like manner, likewise
kamwe (76) - never - always used with negative preceding - "Singe-thubutu kamwe"
kanyaga (83) - tread on
kata roho (79) - die
kawaida (76) - habit, custom
kianga (83) - ray of light
kifo (77) - death
kilele (83) - top, peak
kilemba (80) - turban
kiriba (84) - animal skin water bag
kisa (76) - story
kitani (80) - flax, linen
kitanzi (79) - noose
kito (78) - precious stone
kiumbe (76) creature
kivuli (76) shade
koba (83) - bag, pouch, wallet
kodolea macho (80) - stare at
kokotea (76) - haul for, drag for

konda (83) - grow thin
konde (81) - cultivated piece of ground
koroma (75) - snort
kuhani (81) - priest
kulungu (82) - species of antelope
kuna (75) - scratch
kuna shwari leo (72) - it's calm today
kuna upepo leo (72) - it's windy today
kutanika (71) - assemble, gather together
kupita kiasi (74) - beyond measure
kwa kasi (75) - speedily, hastily
kwaa (80) - to stumble
kwato (75) - hoof
kwenda shoti (78) - to gallop

L

laani (78) - to curse
ladha (75) - taste
lamba (84) - lick
lea (80) - rear, bring up
levuka (80) - get sober
lia (76) - cry
liwali (80) - governor, headman

M

maarufu (77) - well known, famous
maboromoko (82) - usually maporomoko ya maji = waterfalls
machukio (75) - anger, hate
madaha (80) - airs, graces
madhabahu (81) - place of sacrifice
madhali (80) - since, because, seeing that
magoti (75) - knees
maiti (72) - corpse, dead body-human
makaa (76) - coal
malkia (79) - queen
mamba (77) - crocodile
mapokeo (82) - things received, often in the sense of traditions and customs.
marasharasha (72) - slight drizzle
marehemu (79) the deceased, the late
masharubu (71) - moustache
matofaa (78) - fruit of the rose-apple tree
maulana (76) - Lord, master
mawimbi (72) - waves
mawingu (72) - clouds
mbashiri (79) - fortune teller
mbingu (75) - sky, heaven
mchanga (84) - sand
mchawi (79) - witch
mfalme (73) - king
mfua dhahabu (78) - goldsmith
mfupa (73) - bone
mgongo (74) - back, backbone of a man or animal
mgongo (84) - backbone, ridge
mhalifu (79) - one who breaks the law
mhunzi (78) - blacksmith
milele (81) - always
milki (81) - dominion, kingdom
miongoni mwa (73) - among, in the midst of
mjinga (73) - ignorant, simpleton
mkufu (78) - light ornamental chain
mkungu (78) - Indian almond tree
mkutano (71) - gathering, meeting
mnara (79) - tower, lighthouse
mnyonge (82) - a low, wretched person
mpumbavu (76) - fool, dupe

mradi (75) - plan, intention
Mreno (82) - a Portuguese
mrithi (83) - heir
mshangao (75) - alarm, amazement
mtaa (82) - district, quarter, division of town
mtawa (74) - hermit, recluse
mtelemko (83) - downward slope
mto (80) - cushion, pillow
mustarehe (75) - comfortably settled
mvinyo (80) - wine, spirits
mvua ya mawe (72) - hail
mvuke (72) - steam, also the hot sun after a rain
mwandishi (71) - secretary
mwandishi mdogo (71) - 2nd secretary or under-secretary
mwenye kiti (71) - chairman
mwembe (76) - mango tree
mwewe (74) - hawk
mwovu (78) - a wicked person
mzimu (77) - spirit of dead person, spirits of ancestors or native place of worship
mzoga (72) - cadaver, dead animal

N

nadhiri (81) - vow, solemn promise
naswa (76) - get caught
ncha (75) - point, tip
ndipo (76) - there and then
ndovu (82) - elephant
nena (80) - speak, utter
ngozi (73) - skin
nguruma (76) - growl, roar
ngurumo (72) - thunder
nitakuwa na wasaa (83) - I shall have opportunity
nung'unika (76) - grumble, complain
nyamaza (71) - shut up
nyara (80) - booty, spoils, plunder
nyie watu (75) - you people
nyongwa (79) - to be harassed
nyosha (79) - stretch out
nyufa za macho (75) - slits of eyes

O

ota jua (72) - to bask in the sun

P

paa (84) - small gazelle
paaza sauti (71) - raise voice
paja (83) - thigh
pambazuka (83) - get light, dawn
papasa (83) - grope about
papasa (74) - stroke, rub lightly
pasha habari (81) - spread the news
payuka (83) - talk nonsense, be delirious
pazia (84) - curtain, screen
penya (84) - penetrate
pepesuka (83) - totter
piga chuku (80) - exaggerate
piga teke (75) - kick
piga yowe (78) - to shout
pigwa marungu(79) - to be beaten with a knobkerry
pishana (77) - allow each other to pass
pofu (82) - eland
ponyoka (74) - to slip

R

radi (72) - bolt of lightning
rukwa na akili (80) - lose one's head
rushwa (81) - bribe

S

sadaka (77) - sacrifice
sadiki (78) - believe
sali (74) - pray
shani (84) - a wonder, rare occurrence
shibisha (75) - fill up - feed to satisfaction
shinda (77) - overcome, conquer, surpass, excel, win, pass time, keep on, stay for a time
shtuka (84) - be startled
shughuli (78) - business
shughulika (75) - be occupied
shukrani (72) - thanks, gratitude
shuku (84) - to suspect
sihi (76) - plead, beg
sikitika (78) - be sorry
sonara (78) - jeweller, silversmith
staajabu (79) - to be astonished or surprised
subiri (79) - wait patiently
sultani (73) - sultan
sumbua (77) - annoy, trouble, vex, torment
suria (80) - concubine
suriama (82) - a half-caste

T

-taalamu (80) - educated, scholarly, well-informed
taji (80) - crown
tambaa (77) - creep, crawl
tambika (77) - to make an offering to the spirits
tambiko (77) - offering made to the spirits of the dead
tangulia (71) - precede, go on ahead
tatanisha (76) - complicate, puzzle
tawanyika (71) - scatter
telemka (83) - go down
tetemeka (75) - tremble
thabiti (81) - firm, constant
tia gerezani (79) - put in prison
tia muhuri (80) - seal, confirm, sign
tikisa (75) - shake
timiza (81) - fulfill, complete
tokeza midomo (80) - pout
tone la maji (84) - a drop of water
toswa (77) - be plunged into water, caused to sink
toweka (84) - vanish, disappear
towesha (80) - ruin
toza kodi (80) - collect taxes
tulia (73) - relax, be calm, be quiet
tumbili (78) - small light colored monkey
tumbikia (78) - tumble into
twaa (81) - take
twangwa kinuni (79) - be pounded in a mortar

U

Uajemi (80) - Persia

uawa (79) - to be killed
ububu (84) - speechlessness
udhalimu (81) - injustice, tyranny
udhia (76) - trouble, annoyance
ufafanuzi (80) - explanation, interpretation
uganga (73) - medical skill, including use of magical charms
ugua (83) - groan
uhodari (73) - bravery, skill
uhunzi (78) - work of a smith
ujenzi (81) - construction, building operations
ujumbe (74) - message
ukarimu (77) - generosity, hospitality
ukatili (77) - cruelty, bloodthirstiness
ukingo (75) - bank, edge of river
ukoo (82) - relationship, descent, ancestry
ukungu (72) - fog
ukunjufu (80) - cheerfulness, good temper
umati (71) - crowd
umeme (72) - lightning
unyevunyevu (74) - dampness
upande wa pili (82) - the other side
upanga (79) - sword
upendeleo (81) - favoritism
upeo (84) - furthest point
upeo wa macho (84) - as far as the eye can see
upuzi (84) - nonsense
urujuani (80) - violet (color)
utomvu (75) - sap, juice
utosi (75) - crown of head
utoto (73) - childhood
uzima (73) - life, well being

V

vimba (83) - to swell
vumbi (72) - dust

W

waama (79) - moreover, then
wahi (83) - to be in time
wayo (84) - footprint, track

Y

yatima (80) - orphan
yatupasa (73) - it is proper for us

Z

zahama (79) - confusion, noise
zikwa (82) - to be buried
zikwa mzima (79) - be buried alive
zuka (79) - suddenly appear, pop up